Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SABA

**Kikao cha Nne - Tarehe 5 Novemba, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Bodi ya Biashara ya Nje kwa Kipindi cha Julai, 2001 hadi Juni, 2002 *(The Annual Report and Accounts of the Board of External Trade (BET) for the Period of July, 2001 to June, 2002).*

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania kwa Mwaka Ulioishia tarehe 30 Juni, 2003 *(The Annual Report and Accounts of the Tanzania Engineering and Manufacturing Design Organization (TEMDO) for the year Ended 30th June, 2003).*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 45

**Ujenzi wa Barabara Mpya Vijijini**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa utaratibu wa sasa wa kushughulikia barabara na kuzigawia fedha unazingatia tu barabara zilizopo tayari na fedha hugaiwa kwa kuzingatia urefu wa barabara hizo katika kila Halmashauri *(Local Authority):-*

(a) Je, barabara mpya zinazoanzishwa na wananchi Vijijini na zinahitaji zana zilizo nje ya uwezo wao zitasaidiwa kwa njia gani?

(b) Kwa kuwa Serikali katika kujibu swali Na.187 hapo tarehe 17 Julai, 1997 kuhusu barabara ya Mashewa - Bumba, Mheshimiwa Waziri Mkuu alielekeza kuwa michoro ikiwa tayari (ambayo iko tayari muda mrefu) na vifaa vinavyohitajika kujulikana, basi namna ya kuvipatia itatafutwa, je, vifaa hivyo vitapatikana lini?

(c) Je, Serikali itakubaliana na ushauri kwamba, pana haja ya kuweka fungu maalum kwa barabara mpya za Vijijini au pengine kuanzisha Mfuko wa Barabara Vijijini ili zisishindane na barabara kuu na za Mikoa katika kupatiwa fedha?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikiri kwamba ni kweli kwamba swali hili liliulizwa mwaka 1997 na lilitolewa maelezo kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo ya Vijijini, zipo barabara zinazounganisha Vijiji na maeneo yanakopatikana huduma mbalimbali za kijamii na kiuchumi pamoja na barabara zinazounganisha Kijiji na Kijiji. Kimsingi barabara hizi ni muhimu kwa kuwa ubora wake huchangia katika jitihada za kupambana na umaskini. Barabara zinazoanzishwa na wananchi Vijijini zinajulikana kama barabara za Vijiji, hivyo ni mbali za Vijiji. Jukumu la kuzifanyia matengenezo barabara hizi kwanza ni la wananchi wenyewe kwa kushirikiana na Serikali za Vijiji husika pamoja na Halmashauri yao.

Aidha, Serikali kupitia programu mbalimbali za Wahisani kama vile *TASAF* na programu ya usafiri na uchukuzi Vijijini inaendeleza jitihada zake za kuzifanyia matengenezo barabara za aina hii.

(b) Mheshimiwa Spika, barabara ya Kijiji cha Mashewa - Bumba, yenye urefu wa kilometa tano ni mpya na inaunganisha Kijiji cha Bumba Wilayani Lushoto na Kijiji cha Mashewa Wilayani Korogwe. Kutokana na umuhimu wa barabara hii, mwaka 1997 Wizara ya Ujenzi ilitoa shilingi 500,000/= kwa Mhandisi wa Mkoa wa Tanga ili kuifanyia barabara hiyo upembuzi yakinifu yaani *feasibility study.* Ofisi ya Mhandisi wa Mkoa wa wakati huo ilifanya kazi hiyo na kuchora michoro ya awali yaani *preliminary design* pamoja na kutoa makadirio ya awali yaani *preliminary estimates* ya ujenzi wa barabara hiyo kuwa ni shilingi milioni 200 kulingana na makadirio ya mwaka 1999. Gharama hii ni kubwa lakini inatokana na hali ya barabara yenyewe ambayo inapita kwenye miamba na milima mingi na mikubwa.

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kutekeleza ahadi inazozitoa. Kwa kuwa uwezo wa Serikali kifedha ni mdogo, utekelezaji wa kazi za ujenzi wa barabara mpya Mashewa - Bumba haujafanyika kama ilivyotarajiwa. Hata hivyo, Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto, ikishirikiana na wanakijiji wa Bumba, itaweka matengenezo ya barabara hii katika mipango yake kuanzia mwaka wa fedha 2005/2006 ili iweze kutengenezwa kwa awamu.

Aidha, tunaishauri Halmashauri iendelee kutafuta Wahisani na hasa punde mpango wa *TASAF* utakapoanza ili waweze kuona kama wanaweza kusaidiwa kwa njia hiyo. Lakini wakati huo huo, Serikali bado inaendelea kutoa ahadi hii na tunaomba Mheshimiwa William Shellukindo na wananchi wa eneo hili wavumilie kidogo tusubiri mwakani tunaweza tukazungumza kuona kama tunaweza kuiweka katika sehemu ya Bajeti ya Maendeleo. *(Makofi)*

(c) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge kuhusu kuweka fungu maalum la barabara mpya za Vijijini au kuanzisha Mfuko wa Barabara za Vijijini. Tutaufanyia kazi ushauri huu ili kuona namna bora ya kuutekeleza ndani ya Serikali kwa ujumla wake.

**SPIKA:** Mheshimiwa William Shellukindo yuko tayari kusubiri. Namwona Mheshimiwa Joel Bendera, ana swali la nyongeza.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa barabara hii aliyozungumzia Mheshimiwa William Shellukindo, inaunganisha Lushoto na Korogwe na ni muhimu; je, kama Naibu Waziri alivyojibu, yuko tayari pia kusaidia kutoa fungu la ziada katika kufanikisha barabara hii ili iweze kusaidia kwa sababu inaunganisha Mkoa kwa Mkoa na hii iwe ya Mkoa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nadhani pengine sio vizuri sana kusema ndiyo tutaweka fungu la ziada katika mazingira tunayokuwanayo ya uhaba wa fedha. Lakini tumekubali kama Serikali kwamba tutaangalia jambo hili kupitia fungu dogo la *Development* mwakani, pengine tutakapokuwa tumeona hali halisi ndiyo tunaweza tukaona pengine tufanye nini kuhusiana na ombi lake.

**SPIKA:** Swali linalofuata Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali.

Na. 46

**Daftari la Makazi**

**MHE. AZIZA SLEYUM ALI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeandaa utaratibu wa wakazi wote kujiandikisha katika Daftari la Makazi ambao umeshaanza:-

Je, Serikali imeandaa utaratibu gani wa kuwaelimisha wananchi kuhusu Daftari hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa wakazi wote kujiandikisha katika Daftari la Makazi umeanza nchini kote. Madhumuni ya kuanzishwa kwa utaratibu huu ni kuiwezesha Serikali kuwa na orodha kamili ya wakazi wa eneo husika na hivyo kuwa na takwimu sahihi za wapigakura katika chaguzi za viongozi wa Vijiji, Mitaa na Vitongoji. Ili kuwa na uelewa juu ya zoezi hili, Ofisi yangu kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Uchaguzi imeitisha vikao na Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Makatibu Tawala wa Mikoa. Katika vikao hivi, viongozi hawa wameelimishwa juu ya umuhimu wa Daftari hili na kuwataka wakawahamasishe wananchi ili wajiandikishe katika Daftari la Makazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Ofisi yangu kwa barua Kumbukumbu Na.HB114/126/01 ya tarehe 14 Septemba, 2004 imewataka Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini kuwasilisha mahitaji yao ya Daftari hili. Aidha, Halmashauri zimetakiwa kutoa Elimu kwa Umma kuhusu umuhimu wa kujiandikisha kwenye Daftari hili. Katika barua hii imesisitizwa kwamba wananchi wasitishwe wala kubaguliwa wakati wa kutekeleza zoezi lao. Ili kuhakikisha kwamba zoezi hili linaeleweka kwa wananchi, Ofisi yangu imeanzisha kipindi kinachorushwa na Redio Tanzania pamoja na Televisheni.

Aidha, viongozi katika ngazi za Wilaya hufanya ziara za kuhamasisha wananchi juu ya umuhimu wa kujiandikisha katika Daftari hili. Baada ya zoezi la kuandikisha wakazi kukamilika, taarifa hizi zitawekwa katika mbao za matangazo ili wakazi wa maeneo husika waweze kuhakiki uhalali wa waliojiandikisha. Taarifa nilizonazo ni kwamba zoezi hili linaendelea vizuri na ninatoa wito kwa wananchi wote kujiandikisha kwa nguvu zote. *(Makofi)*

**MHE. AZIZA SLEYUM ALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kutokana na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu wananchi

wanaolalamika kuwa uandikishaji wa Daftari hili unabagua wananchi ambao ni wanachama wa Vyama vya Upinzani?

Swali la pili, je, Serikali inatoa kauli gani kwa wananchi ambao bado wanachanganyikiwa katika madaftari haya mawili, Daftari la Wakazi na Daftari la Kudumu? Serikali inatoa kauli gani ili kuweza kuwaelimisha wananchi waweze kuelewa tofauti ya madaftari haya mawili?

**SPIKA:** Majibu Naibu Waziri, kama kuna Waziri mwingine mwenye majibu ya nyongeza ajiandae. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu malalamiko kwamba utaratibu huu unabagua wananchi ambao ni wa vyama vingine, naomba kwanza niseme kwamba Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, haijapokea taarifa yoyote rasmi kupitia Ofisi yetu kwamba kuna jambo kama hili linaloendelea. *(Kicheko)*

Lakini pia, naomba kusema kwamba kama nilivyosema katika maelezo yangu, utaratibu huu umewekwa kwa namna ambayo inawawezesha watu kuweza kutoa malalamiko yao ili kurekebisha kasoro zozote ambazo zimo katika lile Daftari. Utaratibu huo ni ule wa kuweka majina yote yaliyoandikishwa katika Daftari kwenye mbao, kwenye miti, kwenye shule, kila mahali ili mtu yeyote ambaye ni *aggrieved* aweze kupata nafasi ya kuwasilisha malalamiko yake popote pale anapoona panafaa ikiwa ni pamoja na Serikali yenyewe. Kwa hiyo, hiyo ndiyo tunaweza tukasema ndiyo kauli tuliyonayo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kweli kwamba mazoezi haya mawili yanakwenda sambamba lakini malengo yake ni malengo mawili tofauti. Tuna uchaguzi wa Vitongoji na Vijiji na uchaguzi huu ndio unaohusishwa na Daftari la Wakazi. Daftari la Kudumu ni daftari ambalo linalenga Uchaguzi Mkuu wa mwaka kesho 2005. Katika maelezo ya Serikali kupitia viongozi, vyombo vya habari, jambo hili limekuwa linaelezwa wazi wazi na katika mikutano yote imewekwa bayana ili kuhakikisha kwamba hakuna utata katika mambo haya mawili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nafasi ya maswali mawili zaidi. Mheshimiwa Hadija Kusaga, atafuatiwa na Mheshimiwa Frank Maghoba.

**MHE. HADIJA K. KUSAGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa zoezi hili hasa katika uandikishaji wa wakazi limeonyesha kuwa ni gumu na tunaelekea kwenye uandikishaji wa Daftari la Wapigakura na kwa kuwa zoezi hili linahusu sana ngazi ya Mtaa, Vitongoji na kadhalika, je, Serikali inatamka nini kuhusu kuwawezesha Wenyeviti wa Mitaa ama Wenyeviti wa Vitongoji kwa kuwawezesha kipesa ili waweze kuifanya kazi hii kikamilifu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika maelezo yangu, zoezi linaloendelea hivi sasa kwa taarifa tulizonazo, halina ugumu ambao ni *insurmountable,* ambao hauwezi kutatuliwa. Kila Halmashauri imepewa maelekezo ya kutosha na viongozi wote katika kila Halmashauri wameelimishwa vya kutosha juu ya jambo hili ikiwa ni pamoja na Madiwani wote.

Kwa hiyo, kama kuna utata ambao pengine ulikuwepo katika maeneo fulani fulani, hilo linazungumzika tunaweza tukapokea rai lakini itakuwa ni *specifically* kwa ajili ya eneo hilo kutokana na hali ambayo pengine haieleweki katika Halmashauri husika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Frank Maghoba, zamu yako.

**MHE. FRANK G. MAGHOBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unakaribia sana na kwa kuwa maeneo mengi wananchi hawana taarifa kabisa kwamba kuna Daftari la Wapigakura wa Mtaa na sasa Waziri anatamka kwamba zoezi linakwenda vizuri, je, Serikali haioni umuhimu wa kuishirikisha Tume husika kushiriki moja kwa moja kwenye Vijiji hivyo na kutoa elimu ya msingi kwa watu ambao hawajui kuhusu taarifa hizo?

**SPIKA:** Tume husika maana yake Tume ya Uchaguzi. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza sio kweli kwamba wananchi wengi eti hawajui juu ya suala hili. Maelezo ambayo yamekuwa yakitolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kauli mbalimbali za Serikali kupitia vyombo vya habari na utekelezaji mzima unavyoendeshwa hivi sasa, Wakuu wa Mikoa wote, Wakuu wa Wilaya wote, Halmashauri zote zinaelewa waziwazi mazoezi yote mawili yanayokwenda hivi sasa sambamba.

Kwa upande mwingine Mheshimiwa Frank Maghoba, yeye kama Mbunge lakini vile vile kama Diwani na kama yeye ni mmoja wa watu ambao wamepata fursa kama hii ya kuelewa zoezi hili, nilitarajia na yeye angekuwa mstari wa mbele kuwasaidia wananchi kama wapo ambao hawaelewi jambo hili. *(Makofi)*

Lakini mwisho nataka niseme kwamba Tume ya Uchaguzi kwa maana ya Uchaguzi wa Vitongoji na Serikali za Vijiji haina uhusiano wa moja kwa moja, ni mazoezi mawili tofauti. Kwa hiyo, Tume inangoja jukumu lake, sisi Serikali za Mitaa ndio tunaendelea na zoezi la Vitongoji na Vijiji. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Maswali kwa Wizara ya Elimu na Utamaduni, Mheshimiwa Joel Bendera.

Na. 47

**Tatizo la Kuvuja kwa Mitihani**

**MHE. JOEL N. BENDERA** aliuliza:-

Kwa kuwa mitihani ni njia mojawapo muhimu inayotumiwa Vyuoni na Taasisi mbalimbali katika kupima uwezo, ujuzi, akili na ufahamu wa mwanafunzi popote duniani; lakini jambo la kusikitisha ni kwamba katika nchi yetu kumejitokeza tatizo la kuvuja kwa mitihani na baadhi ya shule kuwaonyesha wanafunzi mitihani na matokeo yake Serikali huchukua hatua za kuzifutia shule hizo matokeo ya mitihani kwa wanafunzi wa shule husika:-

(a) Je, hali ya kuvuja kwa mitihani nchini inasababishwa na nini wakati Waziri wa Elimu na Utamaduni alikwishakiri Bungeni kwamba Baraza la Mitihani limeimarishwa na kwamba mitihani haiwezi kuvuja?

(b) Je, Serikali haioni kuwa tabia hiyo ikiachwa kuendelea nchi yetu itakuwa na wanafunzi dhaifu kitaaluma na matokeo yake ni kupata wataalamu wabovu na viongozi dhaifu wa kuliendesha Taifa hili?

(c) Je, Serikali katika kukomesha tabia hiyo isiendelee kabisa, ina mikakati gani kwa Shule, Vyuo na Taasisi zitakazorudia tendo hilo la aibu kwa nchi yetu?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joel Nkaya Bendera, Mbunge wa Korogwe Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza wakati nikijibu swali namba 25 la Mheshimiwa Masoud Abdulla Salim, Mbunge wa Mtambile, katika Mkutano wa Kumi na Tatu na swali namba 34 la Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar, Mbunge wa Mkunguni katika Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge hili kuwa kufuatia uvujaji wa kupita kiasi uliotokea mwaka 1998 na Serikali ikafuta mtihani wote wa Kidato cha Nne wa mwaka huo, hatua madhubuti zilizochukuliwa na Serikali zimefanikiwa kudhibiti hali hiyo isitokee tena.

Tangu mwaka 1999 hadi sasa hakujakuwepo na tukio lolote la uvujaji wa mtihani ukiwa mikononi mwa Baraza la Mitihani Tanzania. Makosa ambayo bado yanatokea ni yale ya udanganyifu unaotokea baada ya wasimamiaji kukabidhiwa ngazi ya Wilaya hadi ndani ya vyumba vya mitihani na baadhi ya watahiniwa kusaidiwa au kusaidiana wakati wa kufanya mtihani.

Aidha, upo udanganyifu wa kuuza mtihani bandia unaofanywa na matapeli na kufanya idhaniwe kuwa mitihani inaendelea kuvuja. Mwaka huu tayari kuna baadhi ya

watu waliotiwa mbaroni na Polisi kwa kosa la mitihani bandia na hatua za kisheria zinachukuliwa dhidi yao kwa ulaghai wa aina hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, athari za kuvuja kwa mitihani na aina nyingine za udanganyifu katika kufanya mitihani zikiachiwa ziendelee, ni nchi yetu kuwa na wanafunzi dhaifu kitaaluma, kitaalam na wasiojiamini. Wizara yangu kupitia Baraza la Mitihani la Taifa, huchukua hatua za haraka na makini kurekebisha kasoro kama hizo zinazojitokeza.

Aidha, ningependa kuchukua fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi wema kutoa taarifa za kweli kwa vyombo vya dola juu ya uvujaji na udanganyifu wowote katika mitihani ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya wahalifu hawa.

(c) Mheshimiwa Spika, ili kukomesha hali hii isiendelee kabisa, Wizara yangu inaimarisha ulinzi wa mitihani na mafunzo kwa wasimamizi. Aidha, wadanganyifu wanaogunduliwa hupewa adhabu kali ya kufutiwa matokeo na wahusika wote kuchukuliwa hatua za kisheria na mwenye Shule anaweza kufutiwa usajili na Shule husika kuondolewa kwenye orodha ya vituo vya mitihani.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini nina swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa hali hii na majibu ambayo amejibu Mheshimiwa Waziri yanaonyesha bado iko kazi ya ziada ya kufanya katika kuhakikisha kwamba mitihani haivuji kama ambavyo imejitokeza hata leo nadhani wengi tumesikia katika vyombo vya habari kwamba mitihani imevuja sana katika Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha na Mwanza na bado jana kuna mitihani ambayo imewekwa kwenye chumba na askari akavamiwa na mitihani ikaibiwa, je, katika kuokoa hali hiyo, Wizara ama Serikali ina mikakati gani madhubuti ya kuweka usalama hasa baada ya mitihani kufika katika maeneo yanayohusika ili isivuje na kuokoa Taifa hili?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa matukio aliyoyazungumzia Mheshimiwa Mbunge, tuna kazi ya ziada ambayo tunaendelea kuifanya. Lakini kwa taarifa ambazo nimepewa mpaka sasa, ile mitihani inayodaiwa kuuzwa Dar es Salaam, sio mitihani yenyewe inayofanywa na wanafunzi, ni mitihani bandia. Kwa hiyo, napenda kuchukua nafasi hii kuwatahadharisha wananchi waepukane na kuinunua mitihani hiyo, wanapata hasara ya bure. *(Makofi)*

Tukio la Arusha, nimeomba niletewe taarifa kwa sababu sio la kawaida, hatujawahi kuwa na tukio la namna hiyo la majambazi kuvamia na kuiba mitihani ambayo imekwishafika. Kwa hiyo, nisingependa kusema neno lolote la uhakika mpaka nitakapokuwa nimeletewa taarifa na wenzetu walio *on the spot.*

**SPIKA:** Nadhani nilikuona Mheshimiwa Dr. Masumbulo Lamwai au umeridhika?

**MHE. DR. MASUMBUKO R.M. LAMWAI:** Nimeridhika.

**SPIKA:** Sawasawa. Basi, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali. Kwa kuwa imeelezwa kwamba mitihani imeibiwa na hicho ni kitu rahisi cha kuhakiki, ni kupiga simu tu na kuhakiki, kwa nini Serikali kama kweli inahakiki isisimamishe mitihani?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, matukio haya ambayo yametokea ni matukio ambayo sio makubwa sana. Naomba Mheshimiwa Mbunge afahamu kwamba mitihani hii tunaiendesha kwa gharama kubwa sana. Kwa hiyo, kama tutasimamisha zoezi zima la mitihani kwa sababu ya tukio moja, kwa kweli tutakuwa tunaingia katika gharama ambazo sio za lazima. Naomba aamini kabisa kwamba uchunguzi unafanywa na mpaka sasa hakuna sababu yoyote ya kuamini kwamba kumekuwa na wizi wa mitihani kama ule uliotokea mwaka 1999 ilipolazimika kufuta matokeo ya mitihani yote. Tunadhani hizi ni *isolated cases* hazitaathiri ufanyaji wa mitihani wa watahiniwa walio wengi.

**SPIKA:** Swali linalofuata Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga.

Na. 48

**Sekondari Zinazoongoza Kufaulisha Wanafunzi wa Kidato cha Nne**

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna uthibitisho kwamba Sekondari binafsi kadhaa zinazotangazwa kuongoza nchini kwa kufaulisha wanafunzi wa Kidato cha Nne kila mwaka hufanya hila ili kufikia malengo hayo ya kutangazwa washindi:-

(a) Je, Serikali inafahamu kwamba uongozi wa baadhi ya shule za sekondari binafsi huwalazimisha wanafunzi wanaowaona hawawezi kupata daraja la kwanza kurudia madarasa, kuacha shule au kujiandikisha kufanya mitihani kama *Private Candidates* ili wasichafue sifa za shule hizo kwa kupata daraja la II, III au IV?

(b) Je, Serikali haioni kwamba huo ni ubaguzi, uonevu na kuwanyima haki wanafunzi hao ambao kwa kupata daraja la II, III au IV bado wanakuwa wamefaulu na wanaweza kufika mbali kimasomo au katika masuala mengine ya kujiendeleza na kujitegemea kimaisha?

(c) Kwa kuwa hata Serikali imefuta utaratibu wa kuwa na shule kwa ajili ya wanafunzi wenye vipaji maalum, je, Serikali inatoa tamko gani kwa shule hizo ambazo zinaendeleza utaratibu wa kufanya shule zao kuwa za wanafunzi wenye vipaji maalum kinyume cha sera za Serikali?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga, Mbunge wa Ukonga, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema wakati nikijibu swali namba 368 la Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mbunge wa Mbarali katika Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge hili kuwa kitendo cha kuzuia watoto wasifanye mtihani kwa jina la shule wanayosoma ni kuwanyima haki yao wanafunzi hao na kwa kweli ni kuwaibia wanafunzi na wazazi wao karo waliyolipa. Aidha, ni kinyume na maelekezo yaliyotolewa na Afisa Elimu Kiongozi katika Waraka wa Elimu Na.5 wa mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie tena kupitia Bunge lako Tukufu kutamka kuwa kwa mujibu wa maelekezo ya Waraka huo, ni marufuku kabisa wanafunzi wa shule kufanya mtihani kama watahiniwa binafsi, yaani kama *Private Candidates.*

Aidha, ni marufuku pia kuwalazimisha kukariri au kuwaachisha kabla ya kuhitimu wanafunzi ambao walifaulu mtihani wa Kidato cha Pili wa kuingia Kidato cha Tatu. Hivi sasa Wizara yangu inaandaa utaratibu wa *Computer* utakaohakiki kuwa wanafunzi wote wa Kidato cha Tatu watafanya mtihani wa Kitaifa wa Kidato cha Nne katika shule zao walizoingia Kidato cha Tatu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, ameridhika. Tunaendelea na maswali kwa Wizara ya Kilimo na Chakula. Mheshimiwa John Singo.

Na. 49

**Uvunaji wa Maji ya Mvua kwa Umwagiliaji**

**MHE. JOHN E. SINGO** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula mapema mwaka 2003 alitembelea Bonde la Kilimo cha Umwagiliaji kwa kutumia maji ya mvua kule Makanya, Wilayani Same/Kilimanjaro na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri alifurahishwa sana na juhudi za wananchi hao zilizowezesha kupata mavuno mazuri ya mahindi *(bumper harvest)* na kwa kuwa huko Hedaru pia lipo Bonde zuri la Kilimo cha Umwagiliaji kwa kutumia maji yaliyovunwa kutokana na mvua.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha wananchi wapatao 50,000 wanaotegemea kilimo cha kuvuna maji ya mvua katika Miji ya Hedaru na Makanya?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzishirikisha Wizara za Ujenzi, Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mawasiliano na Uchukuzi na Ofisi ya Makamu Rais (Mazingira) katika kuvuna maji hayo ya mvua ili yasilete mafuriko na kuharibu barabara kuu ya Dar es Salaam - Arusha, Reli ya Tanga - Moshi na kuharibu hifadhi ya ardhi ya mimea?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwakopesha wakulima matrekta ya kulimia ili kuwawezesha kutifua ardhi wakati wa kulima badala ya kilimo cha sasa cha kukwangua shamba?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Singo, Mbunge wa Same Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Uchunguzi uliofanywa na Chuo Kikuu cha Sokoine kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula, kati ya mwaka 2002 na 2004 kuhusu njia zinazofaa kuvuna maji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji katika maeneo ya Makanya na Hedaru, umebaini kuwa maeneo haya yanafaa kwa ujenzi wa mabwawa madogo ya kuhifadhi maji.

Mheshimiwa Spika, gharama za ujenzi wa mabwawa katika Kijiji cha Makanya zimekadiriwa kuwa shilingi milioni 120; Kavangere, shilingi milioni 100 na Sisamu, shilingi milioni 70. Mabwawa hayo yakijengwa yatakuwa na uwezo wa kumwagilia maji mashamba yenye jumla ya hekta 600. Baada ya uchunguzi huo kukamilika, Serikali inatafuta fedha kutoka kwenye vyanzo mbalimbali kwa ajili ya kujenga mabwawa hayo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Halmashauri ya Same inashauriwa kuzingatia ujenzi wa mabwawa hayo katika mipango yake ya maendeleo ya kilimo.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo na Chakula haina mpango wa kuzishirikisha Wizara za Ujenzi na Mawasiliano na Uchukuzi katika kuvuna maji ya mvua katika maeneo yanayohusika kwa kuwa Wizara hizo zimechukua hatua za kuhakikisha kwamba miundombinu inazozihusu hayataathiriwa na maji ya mvua.

Aidha, kujengwa kwa mabwawa hayo kutadhibiti wingi wa maji na kwa kufanya hivyo kupunguza athari ambazo yangeweza kusababisha kwenye barabara na reli.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana kwamba kuna haja ya kushirikisha Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) ili kuhakikisha kwamba mabwawa hayo yanatumika kunywesha mifugo na hayatasababisha uharibifu wa mazingira.

(c) Mheshimiwa Spika, kuanzia msimu wa mwaka 2002/2003 Mfuko wa Taifa wa Pembejeo ulianza kutoa mikopo kwa ajili ya kununulia zana za kilimo yakiwemo matrekta na kukarabati matrekta. Utaratibu huo bado unaendelea.

Wakati huo huo, Serikali iko tayari kudhamini mikopo itakayochukuliwa na vikundi vya wakulima kutoka kwenye mabenki kwa ajili ya kununulia zana za kilimo yakiwemo matrekta.

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kufahamu kwamba Wizara yake ina mpango gani na ni lini ambapo zitapatikana fedha kwa ajili ya kujenga hayo mabwawa ili kuboresha kilimo katika hayo maeneo ya Makanya na Hedaru?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, mipango itakamilika pale tutakapoweza kupata fedha za kujengea hiyo.

Mheshimiwa Spika, vile vile, wakati huo huo tumeomba Halmashauri ya Same nayo ijishirikishe katika kukusanya na kwa kushirikiana tutafikia lengo hili.

**SPIKA:** Tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Job Ndugai.

Na. 50

**Ugawaji wa Chakula cha Msaada**

**MHE. JOB Y. NDUGAI** aliuliza:-

Kwa kuwa katika hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Kilimo na Chakula aliyoitoa Bungeni hapo tarehe 28 Juni, 2004 alisema kuwa, katika mwaka 2003/2004 Serikali ilipokea chakula cha msaada kutoka Serikali ya Japan kiasi cha tani 17,000 za mchele na tani 3,000 za ngano na kwa kuwa Serikali ya India nayo ilitoa tani 5,000 za ngano na kwamba chakula hicho kimehifadhiwa kwenye maghala ya *SGR:-*

Je, chakula hicho yaani mchele na ngano kiligaiwa wapi au kinatarajiwa kugaiwa wapi na ni kiasi gani na Mkoa wa Dodoma hususan Wilaya ya Kongwa ilipewa mgao gani wa chakula hicho kwa mwaka 2003/2004?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba katika mwaka wa 2003/2004, Serikali ilipokea msaada wa tani 17,000 za mchele na tani 3,000 za ngano kutoka Serikali ya Japan na tani 5,000 za mchele na tani 5,000 za ngano uliotolewa na Serikali ya India kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka wa 2004/2005. Msaada huo wa chakula uliotolewa na Serikali ya Japan, ulitolewa chini ya mpango wa *Kennedy Round I (KR I)* unaolenga kuongeza upatikanaji wa chakula nchini kwa ajili ya kupunguza upungufu wa chakula. Msaada wa India ulitolewa kwa Serikali ya Tanzania baada ya ziara ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, aliyoifanya nchini India mwezi wa Novemba, 2003.

Mheshimiwa Spika, mpango wa *Kennedy Round I* umekuwa ukitekelezwa tangu mwaka wa 1978 chini ya makubaliano kati ya Serikali ya Japan na Serikali ya Tanzania ambayo yamekuwa yakifanyiwa marekebisho kila mwaka kulingana na mahitaji ya chakula kwa ajili ya kuziba pengo la chakula lililojitokeza. Kulingana na makubaliano hayo, chakula kinachotolewa huuzwa kwa utaratibu wa uwazi ili kudhibiti mazingira ya rushwa na fedha zinazopatikana hutumiwa katika miradi mbalimbali ya maendeleo ya uchumi na jamii ikiwa ni pamoja na ya uzalishaji wa chakula.

Mheshimiwa Spika, chakula cha msaada kilichotolewa na Serikali za Japan na India katika mwaka wa 2003/2004 kiliuzwa kwa wafanyabiashara kwa utaratibu wa Serikali wa zabuni za uwazi. Wafanyabiashara walioshinda katika zabuni hizo walisambaza chakula hicho katika maeneo mbalimbali ya nchi yaliyokuwa na upungufu wa chakula. Hakukuwepo na utaratibu wa kugawa chakula hicho kwa Mikoa na Wilaya na kwa hiyo, wilaya ya Kongwa haikupewa mgao maalum.

Jambo muhimu kwetu kama Taifa, ni kutumia raslimali nyingi tulizonazo kujitosheleza kwa chakula na kuondokana na vyakula vya msaada kutoka nje ya nchi.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. La kwanza kwa kuwa Serikali za India na Japan walitoa mchele na ngano kama sehemu ya kuitikia wito wa ombi la Serikali ya Tanzania kwa ajili ya shida ya njaa kwa wananchi wake. Kwa nini chakula kile wananchi hawakupewa kama sehemu ya programu ya njaa badala yake kikaenda katika taratibu ya kuuzwa?

La pili, kama alivyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri, katika juhudi za kujitosheleza kwa chakula Wilayani Kongwa kuna kijiji kinaitwa Hembahemba. Kijiji hiki kwa mwaka huu peke yake wamenunua trekta mpya 25. Kwa kuwa kijiji hiki ndicho kijiji pekee Tanzania nzima kilichoweza kufanya juhudi kiasi hicho, je, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula mwenyewe atakuwa tayari baada ya Bunge hili tukafuatana naye ili kwenda kujionea mwenyewe mapinduzi ya kilimo makubwa kiasi hicho Wilayani Kongwa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli chakula kilitolewa kwa msaada. Kama nilivyoeleza katika jibu kuwa *Kennedy Round I* ndiyo wana utaratibu kuwa chakula kikifika hasa mchele hakigaiwi moja kwa moja, bali kinauzwa kwa utaratibu ule wa *tender,* fedha ikipatikana zinawekwa katika mfuko unaoitwa *Food Counterpart Funds* na unafanya kazi mbalimbali ikijumlisha na uzalishaji wa chakula. Chini ya utaratibu wa *Kannedy Round 1* na hicho chakula cha India kilipofika kilikuwa ni mchele na ngano na kwa utaratibu tulionao baada ya kuuza fedha hizo zilipelekwa *SGR* kusaidia kununua mahindi kwa ajili ya matumizi hayo hayo kupambana na njaa na sasa hivi kutokana na fedha hizo tumeshanunua tani 63,000 na hiyo tumeongeza uwezo wa *SGR* kuwa na chakula mpaka kufikia tani 90,000. Kwa hivi imefanya kazi na ikitokea dharura nchi inaweza kusaidia kudhibiti hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutembelea huko, ninaamini Mheshimiwa Waziri yuko tayari hata mimi niko tayari kushiriki. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, usikubali kwenda kwa kushinikizwa. Panga ratiba yako mwenyewe. *(Makofi)*

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika jibu la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri, amesema kwamba chakula hiki kilikuwa cha msaada ili kuongeza idadi ya chakula cha nchi hii. Halafu kimeuzwa kwa wafanyabiashara binafsi. Kwa kuwa Serikali imejitoa katika mpango wa biashara, wafanyabiashara kwa nini wasingeagiza wenyewe ili Serikali isimamie vyakula vya msaada kwa ukaribu zaidi? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, utaratibu uliowekwa hapa ni kwa lengo hasa la kuhakikisha kuwa tunawasaidia wananchi chakula cha mahindi siyo mchele wala ngano. Kwa sababu kwa wengi wetu suala la chakula hasa ni la mahindi. Lakini ukiuza, ukipata fedha ndiyo unapata uwezo zaidi wa kununua mahindi na hivyo kukidhi taratibu hizi. Lakini papo hapo wafanyabiashara hawakatazwi nao kununua mahindi na kufanya biashara na hao wanaohitaji.

Na. 51

**Utoaji wa *Tax Holiday***

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA** aliuliza:-

Kwa kuwa *Tax Holiday* zinazotolewa kwa baadhi ya wawekezaji zinatumiwa vibaya kwa vile baadhi yao wanajitangaza kushindwa au kufilisika wanapokaribia kuanza kulipa kodi husika wakati sio kweli na kwa kuwa baadhi yao hubadilisha jina na menejimenti tu lakini bado ni watu hao hao na kwa kuwa, wengi huamua kuuza mali/kiwanda na kujiingiza katika shughuli nyingine halafu huomba *Tax Holiday* mpya kwa shughuli mpya na aliyeuziwa naye hupewa *Tax Holiday* vivyo hivyo:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba huo ni mchezo mbaya ambao unaikosesha Serikali mapato yake?

(b) Je, inakuwaje mwekezaji wa pili katika eneo/kiwanda hicho hicho au mgodi huo huo naye apewe *Tax Holiday* ya miaka hiyo hiyo?

(c) Je, Serikali haioni kwamba utoaji wa *Tax Holiday* sasa upunguzwe muda na uzingatie mambo kadhaa ya stahili au la?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mbunge wa Mbozi Magharibi, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Kama sehemu ya sera zake za kukuza uchumi, Serikali imekuwa ikitoa vivutio mbalimbali kwa wawekezaji wa ndani na wa nje ya nchi ili kuwapa fursa ya kuchangia katika maendeleo na ukuaji wa uchumi wetu. Nia ya Serikali ni kuwezesha uwekezaji kuongeza ajira, upatikanaji wa utaalamu na teknolojia ya kisasa na kupanua masoko ili kuongeza uzalishaji na hivyo kuchangia kwenye Pato la Taifa. Hivyo, katika vipindi mbalimbali Serikali imekuwa ikiangalia njia muafaka ya kutoa vivutio hivi, kwa namna ambayo inawavutia wawekezaji lakini bila kuinyima Serikali mapato.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa *Tax Holiday* ulitumika zaidi katika kipindi cha mwaka 1990 hadi 1997. Kwa sasa Serikali haitumii tena utaratibu huu isipokuwa kwa wawekezaji katika maeneo ya uwekezaji maalum kama vile *EPZ* na kwa miradi mikubwa inayotambulika kama *Strategic Investments* chini ya Sheria ya uwekezaji ya mwaka 1997.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mbunge wa Mbozi Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika maelezo yangu ya utangulizi, Serikali haitumii tena utaratibu wa *Tax Holiday* badala yake vivutio vinatolewa kwa utaratibu wa kuhasibu gharama ya raslimali inayowekezwa. Hivyo iwapo wawekezaji watapokezana miradi, kila mmoja atapata unafuu kulingana na kiasi alichowekeza.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa kuna haja ya kuangalia upya kila mara aina na matumizi ya vivutio vya uwekezaji kwani vinaweza kutoa mwanya wa uvujaji mapato na hivyo kuinyima Serikali mapato yake halali. Kwa kuzingatia hilo Serikali imekuwa ikijaribu kwa nyakati tofauti kuangalia njia bora za kutoa vivutio vya uwekezaji. Kama nilivyoeleza awali, *Tax Holidays* hivi sasa hazitumiki isipokuwa katika maeneo hayo mawili ambapo zinaonekana bado ni muhimu zinafaidi wachache sana na zinaweza kusimamiwa kwa karibu.

Hata hivyo msamaha huo wa muda haubadiliki kampuni inapouzwa au kubadili wenye mali bali huendelea hadi hapo kipindi kitakapomalizika kwa mujibu wa mkataba au sheria husika.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Je, kuna uwezekano basi wa kuondoa hivyo vivutio kwenye *Tax Holiday* kwenye hivyo vivutio asiwemo kama kivutio. Kuna uwezekano wa kuondoa hilo?

La pili, wananchi wetu wanafaidi nini *Tax Holiday* zote ambazo zimepita kama swali lilivyojieleza hapa, wamefaidika kitu gani wananchi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda nimpongeze Mheshimiwa Eliachim

Simpasa, kwa jinsi anavyoshughulikia kero mbalimbali katika jimbo lake zikiwepo kero za wafugaji wa kabila la Kisukuma walioko katika jimbo lake kama vile katika Tarafa ya Kamsamba na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo kwa Mheshimiwa Mbunge, kama nilivyosema utaratibu wa *Tax Holiday* sasa hivi hautumiki. Isipokuwa katika maeneo machache ambayo zinaonekana hizi *Tax Holidady* bado ni muhimu. Hazitumiki lakini yamechaguliwa maeneo kama *EPZ* na maeneo kwenye miradi mikubwa yanayotumika kama *Strategic Investments.* Kwa hiyo, tutaendelea kutumia katika maeneo hayo mawili.

Mheshimiwa Spika, la pili, wananchi wamefaidika vipi na *Tax Holiday* hizi ni kwamba uwekezaji huu umeongeza ajira, umeongeza kodi kutokana na *income tax* na kodi zingine ambazo wawekezaji hawa wananunua kama ni *VAT* na kadhalika na pia imekuza Pato letu la Taifa na faida nyingine nyingi.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kuongezea majibu ya Naibu Waziri kwa kusema kwamba kama mwekezaji anazingatia kwanza na juu ya yote siyo haya mambo ya *insentives* anazingatia uongozi bora katika nchi. Amani katika nchi, soko katika nchi, mambo yale ambayo akiingia mle yanamwezesha kutengeneza hela haraka haraka. Ni mazingira bora na hasa uchumi mpaka ambao hauyumbi, uchumi mpana unaokuwa na ambao hauyumbi.

Lakini kama hayo yapo bado inawezekana uwekezaji wake usiwe na tija. Kwa hiyo, anaomba vivutio vya ziada na ndiyo hapo tumekuja na dhana hii ya *strategic investor* na dhana ya *EPZ* na ndani ya *EPZ* mwekezaji anaomba unafuu wa kodi kwa mfano kwa miaka 10 na huwa anapewa huo unafuu kwa miaka 10 ndani ya *EPZ.* Kwa hiyo, tusidharau hiyo dhana ya vivutio lakini tujue kwamba kubwa zaidi ni hali ya uchumi na hali ya amani na utengamano katika nchi.

Na. 52

***Payroll Levy***

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA** aliuliza:-

Kwa kuwa waajiri wanalazimika kisheria kulipa *payroll levy* ya asilimia 6 kwa Serikali.

(a) Je, kuanzia mwaka 2000 hadi sasa Serikali imekusanya kiasi gani kutokana na *payroll levy?*

(b) Je, fedha zilizokusanywa zilitumika kwa kazi gani?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mbunge wa Nkenge, napenda kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kodi anayozungumzia Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamalam ni ya kuendeleza ustadi *(Skills Development Levy)* ambayo hutozwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Mafunzo na Majaribio ya Ufundi ya mwaka 1994 *(Vocational Education and Training Act, 1994).* Kodi hii ni muunganiko wa kodi mbili yaani kodi ya nyumba iliyokuwepo awali *(Housing Levy)* na hiyo ya *VETA* na ilianza kutozwa Julai 1, 2001.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo haya, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mbunge wa Nkenge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kutokana na chanzo hiki cha mapato Serikali ilikusanya shilingi bilioni 25.5 katika mwaka wa fedha 2001/2002, shilingi bilioni 29.6 katika mwaka wa fedha 2002/2003 na shilingi bilioni 37.8 mwaka 2003/2004.

(b) Mheshimiwa Spika, fedha hizo hugawanywa kama ifuatavyo kutokana na utaratibu wa sasa:-

(i) Theluthi moja ya mapato hutengwa kwenye mfuko wa kuendeleza mafunzo na majaribio ya ufundi katika Mamlaka ya *VETA* na theluthi mbili huingizwa kwenye mfuko mkuu wa Serikali kwa matumizi yake ya Bajeti za miaka husika.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa kodi hii maana yake inamwambia mwajiri akitaka kulipa kidogo asiongeze mishahara na vile vile aajiri wafanyakazi wachache na vile vile ikiwezekana waajiriwa wote wawe vibarua, je, Serikali haioni kuwa kuendelea kutoza kodi hii ni kuendelea kutumia kodi iliyopitwa na wakati na kuendelea kudumaza uchumi? *(Makofi)*

Kwa kuwa hoja kubwa ya kodi hii ni *skills development levy* lakini inaonekana ni fedha kidogo zinapelekwa huko na fedha nyingine zinapelekwa kufanya kazi zisizoeleweka, je, kwa nini Serikali isihakikishe fedha zote zinazotozwa kwa kodi hii zinapelekwa *VETA* ili iweze kwenda mpaka vijijini na hivyo kuweza kusaidia kukuza uchumi kwa haraka?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, nijibu kwamba theluthi moja huenda kwenye mafunzo ya kuendeleza ujuzi *skill development levy.* Ujuzi huu unahitajika na waajiri wote na wenye viwanda ambao wanatoa kodi hii kwa sababu watapata wapi watu ambao wana ujuzi kama hawasomeshwi. Ni mchango ambao umekubalika na umepitishwa Bungeni, siyo mchango ambao umetolewa na Serikali peke yake.

Pili, sehemu ya kodi hii huenda kwenye mfuko mkuu wa Serikali kwa ajili ya matumizi ya Bajeti za miaka husika. Kwa hiyo, siyo kweli kwamba zinakwenda kufanya kazi kusikoeleweka. Unakwenda ku-*finance budget* na miradi mbali mbali ambayo imepitishwa na Bunge lako Tukufu.

Na. 53

**Uvuvi katika Ziwa Tanganyika**

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA** aliuliza:-

Kwa kuwa Sekta ya Uvuvi katika Ziwa Tanganyika hasa Kusini mwa Mkoa wa Kigoma katika mpaka wa Tanzania na nchi za Zambia na Kongo *(DRC)* haitiliwi maanani na Serikali hii kwa kutotafutiwa wawekezaji kwa ajili ya kuvua dagaa na samaki wengine kwa kutumia vyombo vya kisasa kama ilivyo nchini Zambia:-

(a) Je, ni lini Serikali itasaidia kupata wawekezaji ili kuwasaidia wananchi wa Mpanda Magharibi, Nkasi na Kalambo kuondokana na umaskini?

(b) Je, si busara kwa Serikali kujishughulisha na utafiti wa uvuvi wa samaki katika eneo hilo na kujenga kiwanda cha kusindika samaki katika eneo la Kasanga ili kuepusha samaki wanaovuliwa Tanzania kupelekwa Mpulungu bila kulipiwa ushuru wa aina yoyote?

**WAZIRI WA MALISILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mbunge wa Kalambo, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyowahi kulieleza Bunge lako Tukufu wakati nikijibu swali namba 367 mnamo tarehe 03 Agosti, 2003 wakati wa Mkutano wa 12 wa Bunge la Bajeti la mwaka 2003/2004 ambalo liliulizwa na Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Serikali imeweka mazingira mazuri kwa wawekezaji wa ndani na nje kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(i) Kufuta ushuru wa forodha kwa zana za uvuvi zinazonunuliwa kutoka nje pamoja na malighafi ya kutengeneza zana.

(ii) Kutoa *Certificate of Incentives* ambayo inampa mwekezaji nafuu ya kodi ya asilimia 50 *(capital allowance)* kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu ya uwekezaji.

(iii) Kutoa huduma mbalimbali kama vile utoaji wa *health certificate* kwa uuzaji wa mazao ya uvuvi, mafunzo, ujenzi wa mialo bora ya kupokelea samaki na ujenzi wa barabara ndogo ndogo ziendazo kwenye mialo ya samaki.

(iv) Kuandaa mwongozo wa uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi ambao unaelekeza maeneo mbalimbali ambayo yanaweza kutumika kwa uwekezaji katika sekta.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendeleza utafiti wa uvuvi kwenye maeneo yote ya maji nchini kwa awamu chini ya Taasisi yake ya Uvuvi ya Taifa *(TAFIRI). TAFIRI* inacho kituo cha utafiti mjini Kigoma ambacho kinafanya tafiti za aina mbalimbali ndani ya Ziwa Tanganyika Kitaifa na Kimataifa kwa kushirikiana na nchi zinazomiliki ziwa hilo.

Mheshimiwa Spika, sehemu kubwa ya raslimali ya samaki iliyoko Ziwa Tanganyika ni aina ya dagaa ambao wanaweza kutumika kwa kusindikwa na kufungwa kwenye makasha *(packets)* na makopo *(canning).* Kwa kutambua uwezekano huo, Wizara yangu imetoa kibali kwa kampuni moja ijulikanayo kwa jina la *USA MANAGED RESOURCES LIMITED,* kufanya uvuvi mkubwa wa dagaa Ziwa Tanganyika eneo la Kasanga. Matokeo ya uvuvi huo yatatoa maamuzi ya kujenga kiwanda cha kusindika dagaa watakaovuliwa na mwekezaji huyo. Hali kadhalika kiwanda kitakapojengwa na kukamilika kitatoa ajira kwa wananchi wa eneo hilo na dagaa watakaovuliwa watauzwa ndani na nje ya nchi hivyo kuiingizia Serikali mapato na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kuhusu samaki kupelekwa Mpulungu bila kulipiwa ushuru, Serikali chini ya mkakati wa kuimarisha doria za uvuvi kitaifa, imeanzisha kanda lya doria katika Ziwa Tanganyika ambapo imeweka kituo cha doria Kigoma na tumepeleka watumishi kwenye kituo na tutanunua boti ya doria ili kusaidia jitihada za kudhibiti utoroshaji wa mazao ya uvuvi kutoka Ziwa Tanganyika.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Ninashukuru Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna raslimali nyingi kwenye bahari na Maziwa, nataka kuiuliza Serikali ina meli ngapi kubwa za uvuvi katika maeneo hayo kwa ajili ya kuongeza uchumi wa nchi hii?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, Serikali haina meli za uvuvi kwa sababu uvuvi unafanywa kibiashara. Kwa hiyo, Serikali ina meli za kuangalia kwamba uvuvi huu unafanyika kihalali, kwa hivyo *surveillance system,* kwa hivyo Serikali haina kwa sababu haifanyi biashara hii. Hivi sasa kuna meli za uvuvi katika maeneo haya ya *deep sea* zaidi ya 68.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Katika hili zoezi la *National Economic Empowerment* Serikali itakubaliana na mimi sasa kwamba ni wakati muafaka wa kuanzisha mfuko wa mikopo wa zana za uvuvi ili wavuvi hawa wavue kisasa ili waweze kuinua uchumi wao?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, hivi juzi nilijibu swali hapa Bungeni nilieleza kwamba kuna programu hii ambayo itashughulikia maeneo ya bahari, eneo la Mkulala, programu ambayo itatoa pia mikopo kwa wavuvi wadogo ili wawe na zana za kisasa za uvuvi. Lakini pia sheria ambayo tulipitisha hapa Bungeni ina eneo ambalo inazungumzia juu ya mfuko wa uvuvi. Kwa hiyo, hilo Serikali inalishughulikia.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa katika eneo la Ziwa Tanganyika upande wa Jimbo la Kalambo na Jimbo la Nkansi inaonekana kuna meli inayovua ya kutoka Zambia na ambapo huwa wanauza samaki pamoja na dagaa katika eneo hilo, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba meli hiyo inazuiwa isiendelee kuvua na huyo aliyepewa kibali cha kuvua ambaye ni Mtanzania ndiye apewe nafasi ya kuvua tu?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, Serikali haina taarifa kwamba uvuvi ambao unafanyika na meli hiyo. Lakini tunachojua ni kwamba meli hii ya *USA MANAGED RESOURCES LIMITED* ndiyo ambayo ilipewa kibali. Lakini napenda kumuahidi Mheshimiwa Ponsiano Nyami, kwamba tutalifuatilia.

Na. 54

**Tatizo la Tembo - *West Kilimanjaro***

**MHE. LEKULE M. LAIZER** aliuliza:-

Kwa kuwa Ukanda wa *West Kilimanjaro* katika vijiji vya Siha, Kata ya Tingatinga, Blerai, Kitendeni na Kata ya Olmolog Tarafa ya Enduimet kuna tembo wanaoharibu hifadhi ya wananchi na kusababisha baadhi ya maeneo kuwa jangwa kutokana na tembo hao kuvunjavunja miti na kusababisha uharibifu mkubwa:-

(a) Kwa kuwa tembo wameongezeka kutoka 200 hadi 600 kwenye eneo hilo kwa hesabu ya walinzi wa tembo hao, je, Serikali itachukua hatua gani kuokoa msitu huo?

(b) Kwa kuwa wananchi wameacha kulima mashamba kwa ajili ya tembo hao kula mazao, je, Serikali itachukua hatua gani ili wananchi wasikose chakula?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inachukua hatua zifuatazo kuokoa msitu husika:-

Halmashauri ya Wilaya ya Monduli na vijiji vya Kitendeni na Irkaswa kwa kushirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali la *African Wildlife Foundation* lenye Ofisi zake Mjini Arusha, wametenga eneo kwa ajili ya mapito ya wanyamapori ikiwa ni sehemu ya msitu tajwa. Ili kulinda eneo hili, Halmshauri ya Wilaya ya Monduli imepata hati miliki ya eneo hilo ambalo litaongeza ukubwa wa eneo kwa matumizi ya kuchungia mifugo na malisho ya wanyamapori, ikiwa ni pamoja na tembo wanaohama kutoka Hifadhi ya Amboseli iliyopo Kenya kupitia vijiji tajwa kwenda *West Kilimanjaro.*

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua umuhimu wa maeneo yanayotumiwa na wanyamapori wahamao *(Ushoroba Corridor).* Katika Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori Na. 12 ya mwaka 1974 inayopitiwa, suala la kutenga maeneo ya mapito ya wanyamapori limezingatiwa kwa kuyatambua maeneo hayo kisheria.

Vijiji vya Sinya, Tingatinga, Elerai, Olmolog na Kitendeni vipo katika *Pilot Wildlife Management Area (WMA)* ya Enduimet. Kwa vile *WMAs* zinatokana na maeneo ya vijiji, hii ina maana kwamba maeneo zaidi yatapatikana kwa ajili ya uhifadhi wa tembo kwa kuongeza eneo la malisho yao. Kulingana na Mpango wa Kuhifadhi Tembo wa mwaka 2001 wananchi watashirikishwa kuhifadhi tembo kupitia mpango wa *WMAs.* Kanuni za *WMAs* zinaelekeza namna wananchi watakavyofaidika na uhifadhi wa wanyamapori katika maeneo hayo. Hivyo basi wananchi waishio kwenye vijiji vinavyounda *Pilot WMA* ya Enduimet watatumia kanuni hizo kuhifadhi na kufaidika na wanyamapori, ikiwa ni pamoja na tembo.

(b) Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba wananchi wameacha kulima mashamba yao kwa ajili ya tembo. Wananchi wanaendelea na shughuli za kilimo kama kawaida, isipokuwa kuna baadhi ya wananchi ambao wamevamia maeneo ya hifadhi ya msitu ambao pia ni maeneo ya malisho ya wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo ili kukabiliana na hali hii, Wizara yangu inachukua hatua mbalimbali zifuatazo:-

(i) Kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kuhifadhi tembo na mbinu za kujihami na kuwafukuza pale wanapovamia maeneo ya mashamba yao. Mbinu hizo ni pamoja na kutumia risasi za baridi kuwatishia na kutumia sauti ambazo wanyama hawa hawakuzizoea.

(ii) Kuhimiza Halmashauri kuajiri watumishi wa kutosha kwa ajili ya kutoa ulinzi dhidi ya uharibifu wa mali na maisha ya wananchi.

(iii) Kuendeleza taratibu za kuhakikisha kuwa shughuli za uhifadhi wa tembo zinazowanufaisha wananchi walengwa kwa kuweka mpango wa kugawana mafao yanayotokana na matumizi endelevu ya tembo na kuwasaidia wananchi kwenye shughuli za maendeleo ya maeneo yanayozunguka hifadhi za Taifa.

(iv) Kutenga shoroba za wanyamapori kwa ajili ya kudumisha uhifadhi endelevu wa wanayamapori.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza na pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ningependa kuuliza kwamba kwa kuwa tembo wamekuwa wengi sana katika maeneo hayo na ni kweli kama nilivyosema wananchi siku hizi hawalimi na hawa tembo wamesababisha umaskini mkubwa kwa wananchi na nadhani Serikali inawapenda wananchi kuliko hawa tembo. *(Kicheko)*

Je, Serikali itawasaidiaje wananchi hawa waliokuwa maskini kabisa na Serikali wanajitahidi kupunguza umaskini na hawa tembo wanazidisha umaskini? *(Kicheko)*

Swali la pili, kwa kuwa wanyama wanapokuwa wengi Serikali inaruhusu *cropping,* kuna wakati wanaruhusu *cropping* ya pundamilia na wanyama wengine na kwa kuwa hawa tembo nao wamezidi, wamekuwa wengi, je, Serikali haiwezi ikaruhusu *cropping* ya tembo wapunguzwe ili wananchi waweze wakaanza kilimo kama miaka mingine? *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wa Makunduchi, Unguja naomba mvumilie matumizi neno tembo. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lekule Laizer, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Makunduchi lazima wavumilie lakini Mjini Magharibi wanatumia tembo.

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Lekule Laizer, kwa pamoja.

Kwanza kabisa ni kweli kwamba tembo wameongezeka Tanzania. Wameongezeka kwa sababu tumeweza kujitahidi sana katika Masuala ya Ujangili. Kwa mfano tembo mwaka 1989 walikuwa tembo 55,000. Hivi sasa tunapozungumza tembo wako kama 120,000 na tunajua kwamba kweli tembo hawa wanaingia katika maeneo ya mashamba ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo ambayo wananchi wamekuwa na mashamba na nyumba katika maeneo ya mashoruba yaani *corridors.* Kwa hiyo, hata tembo wakikaa miaka mingapi wanakumbuka sehemu ile ambayo waliokuwa wanapita miaka ya nyuma na wanapita katika sehemu ile na kufanya uharibifu mkubwa. Nimeeleza kwamba tunachofanya mahali ambapo tunasikia kuna matatizo tunapeleka askari lakini tunaomba pia Halmashauri nao pia waweke fedha zile pembeni hasa hasa katika upande wa uwindaji asilimia 25 wanayopata ili waweze kununua risasi za kuweza kuwadhibiti hawa tembo.

Lakini niseme kwamba hivi majuzi suala hili la *crooking* tuseme, tumekuwa kwenye Mkutano kule Bangkok wa *site* na tunategemea kupeleka hoja kwenye Mkutano huu ili Serikali ya Tanzania iweze kuruhusiwa kuhamisha tembo kutoka daraja la kwanza kuingia daraja la pili. Daraja la kwanza ni pale ambapo hakujaruhusiwa biashara yoyote ya meno ya tembo na daraja la pili ni pale ambapo kwa kweli itaruhusiwa kwa maana hiyo *crooking* itawezekana pamoja na kuruhusiwa biashara lakini kwa udhibiti maalum.

Kwa hiyo, tumeamua pamoja na hayo kwamba tutakuwa na Mkutano wa Afrika nzima katika Kanda nne, Afrika Mashariki, Kusini, Kanda ya Kati na Kanda ya

Kaskazini mwezi Mei, 2005. Kwa upande wa Tanzania Mkutano huu tunategemea tutaufanya Arusha kwa hiyo, tutazungumzia hasa hasa masuala mazima ya tembo na jinsi gani ambavyo wanaathiri mashamba na binadamu nchini kwetu. Ahsante sana.

Na. 55

**Ujenzi wa Kituo cha Polisi Vikokotoni - Mlandege**

**MHE. FATMA SAID ALI** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika Mkutano wa Bajeti ya mwaka 2004/2005 Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuimarisha usalama wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005; na kwa kuwa, fujo za kisiasa mara nyingi huanzia kwenye eneo la Darajani - Zanzibar:-

Je, Serikali haioni kuwa ipo haja ya kujenga kituo cha Polisi kwenye eneo la Vikokotoni?

**WAZIRI WA MAMBO YANDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Said Ali, Mbunge wa Mlandege, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatarajia kuwa Uchaguzi Mkuu wa mwakani utafanyika kwa amani, uhuru na ustaarabu wa kiwango cha juu nchini pote pamoja na Zanzibar . Hata hivyo kwa watu wenye nia mbaya ya kufanya fujo kwa kisingizio cha uchaguzi kama hao aliowaeleza Mheshimiwa Mbunge, Serikali imejiandaa kwa ukamilifu kuzima fujo hizo.

Kwa upande wa eneo la Darajani, mwaka huu Serikali haina mpango wa kujenga kituo kipya. Hata hivyo endapo fujo zitatokea katika eneo hilo, vituo vya jirani vya Malindi, Mwembe Madema na Kituo Kidogo cha Mkunazini vimepewa uwezo mkubwa wa kudhibiti hali yoyote ya uvunjaji wa amani unaoweza kujitokeza.

Napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba njia ya uhakika zaidi ya kupata Kituo cha Polisi katika eneo la Darajani ni kuwahamasisha wananchi waanze hiyo kazi na baadaye Serikali iweze kusaidia nguvu zao.

**MHE. FATMA SAID ALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Vikokotoni ipo mpakani baina ya Jimbo la Mlandege na Jimbo la Mkongo na kwa kuwa makao makuu ya vyama vyetu vikuu vya siasa yapo karibu na Vikokotoni yaani *CUF* iko Mtendeni Makao Makuu yake ambayo ni karibu na Vikokotoni na CCM Makao Makuu yake yako Kisiwandui karibu na Vikokotoni; kwa kuwa, Vikokotoni ni mahali pa makutanio ya wananchi na wafanyabiashara ndani na nje ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, je, Mheshimiwa Waziri bado haoni umuhimu wa hoja hizi kwamba Serikali ifikirie mpango wa kujenga Kituo cha Polisi Vikokotoni?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fatma Said Ali, Mbunge wa Mlandege, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba makao makuu ya CCM na *CUF* kule Zanzibar yote yamo katika eneo la Vikokotoni katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge, ana bahati kubwa sana. Nataka nimhakikishie kwamba hali hiyo tunaielewa na huu mpango tulioupanga ambao nimeueleza katika jibu langu la msingi umezingatia uelewa huu. Lakini bado naendelea kutoa wito kwamba eneo la Vikokotoni linastahili kuwa na Kituo cha Polisi ni kweli kabisa. Lakini ni kama nilivyomweleza kwamba tusaidiane aanze na wananchi na sisi tusaidiane.

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika nashukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni kawaida kwa Jeshi la Polisi wakati wa sherehe za Serikali kuleta vitendea kazi kwa ajili ya kuzidisha ulinzi pale Zanzibar lakini baada ya kumalizika sherehe vifaa hivyo urejeshwe tena Dar es Salaam.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni kuna upungufu mkubwa wa vifaa hivyo kuna umuhimu wa vifaa hivyo vikabakia pale pale Zanzibar?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mohammed Rajabu Soud, Mbunge wa Jang'ombe, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba inapotokea dharura maalum zikiwemo sherehe na mambo mengine hata shughuli za uchaguzi, Jeshi la Polisi uongeza nguvu kule Zanzibar na si Zanzibar tu mahali popote ambapo tuna kila sababu ya kuamini kuwa panaweza pakatokea rabsha. Hiyo huwa ni kwa dharura maalum kwa tukio maalum ambalo limepangwa kwa sababu vifaa tayari huwa vimesambazwa kwa usawa unaolingana katika nchi nzima. Kwa hiyo, inavyotokea dharura unahamisha vifaa kutoka sehemu fulani unavipeleka pale ikimalizika dharura ile ni vema kuvirejesha kunako husika ili ule usawa uendelee kubaki. *(Kicheko)*

**MHE. MOHAMED ALI SAID:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali godo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa inaonekana kwamba Polisi ndiyo chanzo cha vurugu hasa katika suala la uchaguzi pale taratibu za uchaguzi zinapovunjwa kama kuchukuliwa visanduku katika vituo vya kupigia kura kama iliyotokea 2000.

Je, Serikali inatoa tamko gani pale itakapobainika kwamba Polisi wamechukua visanduku na kuvihamisha kupeleka sehemu nyingine? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mohamed Ali Said, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, natofautiana naye na nakanusha kabisa kwamba Polisi inahusika kwa vyovyote katika kuleta vurugu au kufanya lolote ambalo ni baya. Polisi kazi yake ni kurejesha amani pale ambapo kuna vurugu na hiyo ndio kazi ambayo Polisi inafanya tena kwa uwezo mzuri, mkubwa na kwa ufanisi. Kwa sababu hiyo nadhani wanastahili pongezi za Bunge lako. *(Makofi)*

Katika mazingira hayo mimi siwezi na wala sina sababu ya kutoa kauli yenye kutia wasiwasi kama labda Polisi wanaweza wakafanya jambo kama hilo alilolizungumzia Mheshimiwa Mbunge. Lakini sheria na taratibu za Jeshi la Polisi kwa yeyote ambaye anakiuka taratibu za kijeshi za Jeshi lao huwa nazichukua na likitokea popote pale wataendelea na hatua zao.

Na. 56

**Kuimarisha Kituo cha Polisi Nyanguge**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Polisi wa Kata ya Nyanguge wanapambana sana na wahalifu wa mali na ulinzi wa raia; na kwa kuwa kituo hicho cha Polisi hakina hadhi na madaraka ya kutoa maamuzi mpaka waende Magu Mjini na hadi sasa kituo hicho hakina *Investigation Register* ambayo ni *code number:-*

(a) Je, Serikali itakiimarisha lini kituo hicho kwa kukipa hadhi ya kujiendesha chenyewe kwa kuwasaidia wananchi hapo kituoni badala ya kwenda Mjini Magu?

(b) Je, Serikali haioni kuwa usumbufu wa kwenda Magu Mjini, umekuwa kero kwa askari hao na ni hatari kwa usalama wao na wananchi?

(c) Je, ni lini kituo hicho kitapatiwa usafiri wa uhakika ili kuondokana na hali ya kuomba omba kwenye mabasi?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kituo kidogo cha Polisi Nyanguge ni moja ya vituo vilivyojengwa kwa nguvu za wananchi na kilifunguliwa rasmi tarehe 20 Juni, 2004 wakati wa sherehe za Mbio za Mwenge. Ujenzi wa kituo hiki bado haujakamilika ikiwa ni pamoja n ujenzi wa vyoo kwa ajili ya askari na mahabusu, sehemu ya kuhifadhi silaha na nyumba za askari. Tunamwomba Mheshimiwa Mbunge na viongozi wengine wa

eneo hilo, waendelee kuhamasisha wananchi wa Nyanguge ili waendeleze ujenzi wa kituo hicho hadi kifikie hadhi ya Daraja C chenye uwezo wa kuwa na idadi ya askari 20 ndipo kiweze kupewa *Investigation Register(IR)* ya kujitegemea kama inavyotakiwa kwa mujibu wa Kanuni za Jeshi la Polisi *(PGO)* Na. 112(c).

Mheshimiwa Spika, kituo hicho *(Polisi Post)* kipo kando kando ya barabara kuu itokayo jiji la Mwanza kwenda Musoma na ni kiasi cha kilometa 30 tu kwenda Magu. Umbali huu si mkubwa sana hivyo askari wa Nyanguge hawapati usumbufu wala kero katika utendaji wa kazi zao ukilinganisha na vituo vingine ambavyo vipo mbali sana kutoka Makao Makuu ya Wilaya. Kuhusu gari kwa sasa Serikali haina uwezo wa kutoa gari kwa ajili ya vituo vidogo kama cha Nyanguge. Kipaumbele hivi sasa ni kuimarisha usafiri kwenye Vituo vya Polisi vya ngazi ya Wilaya.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali yangu mawili ya madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini naomba niulize kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa askari wa Nyanguge, wamefanya kazi nzuri sana ya kuhakikisha kwamba raia wa pale, wahalifu wote wanawachukua na kuwapeleka Magu kwa uharibifu wao. Sasa ni kwani nini Serikali kama bado inasubiri utaratibu wa kuwapatia usafiri wakatenga angalau fungu dogo la kuweza kuwapa wakakodi gari kuwafikisha wahalifu kule Magu?

(ii) Kwa kuwa askari hao wa Nyanguge wanafanya kazi nzuri kwa kweli, kwani nini basi Serikali isiwaangalie hata kuwapandisha vyeo kuwapa motisha?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Nyawazwa, kama ifuatavyo:-

Kwanza napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza askari wetu wa kituo cha Nyanguge kuweza kupata pongezi ya Mheshimiwa Mbunge, si kazi rahisi inaonyesha wanafanya kazi nzuri sana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi kuhusiana na usafiri tunakwenda hatua kwa hatua. Katika Bajeti yetu ya mwaka huu Bajeti mliotupatia katika Bunge hili kwenye Bajeti ambayo tunaendelea nayo sasa hivi tutakuwwa na uwezo wa kununua magari kwa ajili ya Wakuu wa Polisi wa Wilaya. Bila shaka kama pale ambapo wanazo gari, hivi sasa hivi zitaweza kutumika kwa matumizi ya kuhudumia vituo vya chini zaidi na ninaamini inaweza kufaidika kwa njia hiyo Kituo Kidogo cha Nyanguge.

Kuhusu kuwapandisha vyeo napokea huu ushauri ingawa utaratibu huo wa kupandisha vyeo hauendi kwa kutazama kituo kimoja kimoja, huenda kwa kutazama kwa upeo mzima wa Jeshi la Polisi.

Na. 57

**Fedha za Ukarabati wa Majengo ya Kambi ya 14 KJ - Wawi**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ya mwaka 2004/2005 imeelezwa kwamba zimetengwa fedha kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya askari na Hospitali ya Jeshi iliyopo katika Kambi ya 14KJ - Wawi, Pemba:-

(a) Je, ni fedha kiasi gani zimetengwa kwa ajili ya majengo ya askari na ni kiasi gani kwa ajili ya ukarabati wa hospitali hiyo?

(b) Je, ni mwezi gani kazi hiyo itaanza rasmi?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Wawi, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, vikosi vingi vya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kikiwemo kikosi namba 14 KJ kilichoko Wawi vinakabiliwa na uhaba mkubwa wa majengo ya kuishi maafisa na wapiganaji. Majengo yaliyopo mengi ni machakavu na yanahitaji ukarabati mkubwa. Kama ambavyo nimekuwa nikiliarifu Bunge lako Tukufu, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kutumia fedha za Bajeti kukarabati baadhi ya majengo machakavu na kumalizia baadhi ya viporo vya majengo katika Kambi za Jeshi vilivyoachwa miaka mingi, kama vile Ihumwa - Dodoma, Sofa - Arusha na Makoko - Musoma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha 2004/2005, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imetengewa shilingi bilioni 7.1 kwa ajili ya kukarabati majengo na kukamilisha viporo vya ujenzi wa nyumba katika makambi, ukarabati/ujenzi wa maghala ya kuhifadhia vifaa na zana na ukarabati na uimarishaji majengo ya karakana na eneo la kuegeshea ndege katika Kikosi cha Usafirishaji wa Anga. Viporo vya makambi vinavyokusudiwa kukamilishwa ni katika Mikoa ya Kagera, Mara, Morogoro, Tabora, Tanga, Ruvuma, Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Pwani, Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Spika, huu ni mpango kabambe wa mipango endelevu ya miaka 15 ya uboreshaji na uimarishaji wa Jeshi *(Force Modernisation)* awamu ya kwanza ya miaka 5 iliyoanza 2003.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Wawi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Jumla ya shilingi milioni 350 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba mpya 50 za kuishi familia za maafisa na wapiganaji katika kambi hiyo, shilingi milioni 15 zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa Bwalo la Maafisa na shilingi milioni 10 zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa Hospitali ya 14 KJ.

(b) Mheshimiwa Spika, maandalizi ya awali ununuzi wa vifaa na kuandaa michoro, yameanza na kazi ya ujenzi inatarajiwa kuanza katikati ya mwezi Desemba, 2004. Kazi ya ujenzi itafanywa Kikosi cha Ujenzi cha Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania Brigedia Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge akiwemo Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Wawi, kwa kufuatilia kwa karibu utatuzi wa matatizo ya wapiganaji wetu katika vikosi vilivyoko Majimboni mwao. *(Makofi)*

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake yenye ukweli ndani yake.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi, inatekeleza vizuri Ilani yake ya Uchaguzi ya mwaka 2000 kwa kuwaondoshea wananchi matatizo na mfano mzuri ni huu ambao ameuzungumza hapo kwamba katika Kikosi changu cha Jeshi cha 14 JK kitajengwa nyumba, hospitali na bwalo. Kwa hiyo, kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Wawi wakiwemo askari Jeshi napenda kuishukuru sana Serikali hii. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, napenda kupokea pongezi maalum lakini naomba pongezi hizo ziende kwa Amri Jeshi wetu Mkuu na Rais wetu na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, kwa sababu yeye ndiye asimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Na. 58.

**Ugonjwa wa Mwenendo wa Moyo kwa Binadamu**

**MHE. EDSON M. HALINGA** aliuliza:-

Kwa kuwa, magonjwa ya mwenendo wa moyo kwa binadamu yanahitaji tiba ya uhakika na ya haraka; na kwa kuwa, Serikali huzipatia mashine za *Ultra Sound* hospitali zote za Wilaya jambo linalofaa kupongezwa lakini hakuna watumishi wanaotambulika kitaalamu ili kuzitumia mashine hizo:-

(a) Je, kwa kuwa yupo Mhisani katika Hospitali ya *KCMC* anayejitolea kuwafundisha watumishi hao kwa kiwango cha *Diploma;* je, Serikali ina tatizo gani la kutoitambua elimu hiyo na kuwa na *scheme* ya ajira zao?

(b) Je, Serikali ipo tayari sasa kuwatambua na kuwawekea *scheme* za kazi na madaraja yake watumishi hao?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: (k.n.y. WAZIRI WA AFYA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Edson Mbeyale Halinga, Mbunge wa Mbozi Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa matibabu ya magonjwa ya moyo yanahitaji tiba ya uhakika na haraka. Aidha, napenda nikubaliane na Mheshimiwa Edson Halinga, kuwa Serikali imemudu kuzipatia hospitali takriban zote za Serikali mashine za *X-ray* na *Ultra Sound.*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo naomba nisikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kuwa, hakuna watumishi wanaotambulika kitaalamu wakizitumia mashine hizo. Mashine hizi yaani *X-ray* na *Ultra Sound* huendeshwa na mafundi sanifu na *X-ray Radiographers.* Watumishi hawa huchukua mafunzo ya Stashahada ya miaka mitatu katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Tiba Muhimbili. Serikali inawatambua watumishi hao na wanao muundo wao wa Utumishi.

Aidha, wapo Madaktari Bingwa wa Rediolojia ambao ni wataalamu wa kutumia mashine hizi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli pia kuwa Hospitali ya *KCMC* inatoa mafunzo haya. Mafunzo haya hutolewa kwa madaktari wasaidizi ili kuwafanya wawe na ujuzi wa ziada wa Rediolojia. Wizara haina tatizo la kuitambua elimu hii kwani mafunzo haya yameanzishwa na Wizara yenyewe. Wahitimu wa mafunzo haya hurekebishiwa maslahi yao ya mshahara mara wapatapo ujuzi huu wa ziada na kuwa Madaktari Wasaidizi wa Rediolojia *(Assistant Medical Officers - Radiology)*

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri ni mazuri. Lakini anaweza kukubaliana na mimi kwamba pamoja na kuona umuhimu wa hali hii na hatari ya mionzi inayotumiwa ana *X-ray* zilizoko pale na *Ultra Sound* pamoja majengo yanayotumika hayawapi usalama wale wasimamizi wa shughuli hizi na kwani nini kusiwe na muundo wa mmoja katika hii nchi nzima ili iweze kuwa salama kwa wale wanaotumia au wasimamizi wa shughuli hizi katika hospitali zetu za Wilaya kwa pamoja?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (k.n.y WAZIRI WA AFYA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Edson Halinga, kama ifuatavyo:-

Serikali kabla ya kufunga mashine ambazo nimeelezea kwa sababu ya uchunguzi wa magonjwa mbalimbali uhakikisha usalama katika majengo ambapo mashine hizo zitafungwa. Kama kuna sehemu kuna matatizo ni jukumu la Mheshimiwa Mbunge, ama wananchi, ama Daktari kutoa taarifa lakini hata hivyo, ukaguzi unafanywa mara kwa mara kuhakikisha kwamba kuna usalama wa kutosha na wakaguzi hao kutoka katika Kitengo cha Tiba Wizara ya Afya. Namwomba Mheshimiwa Edson Halinga, tuonane naye kama kuna tatizo hilo katika hospitali yake ili tatizo hilo liweze kurekebishwa mara moja.

**MHE. MOHAMED ABDULLY ALLY:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa matatizo ya ugonjwa wa moyo nchini ni makubwa na ni wananchi wengi wanaoathirika na matatizo haya na kwa kuwa niliwahi kusikia Serikali kwamba imewaalika wataalamu kutoka Marekani kwa ajili ya kujenga kliniki maalum ya moyo hivi sasa ni muda mrefu.

Kwa kuwa nimesikia vile vile kwamba hivi sasa wanakuja Wachina kwa ajili ya kujenga kitu hicho hicho, je, Serikali ni wapi hasa imeshika kwa Wachina au kwa Wamarekani au tumefikia wapi? Ahsante.

**SPIKA:** Naona ni swali jipya, lakini naona uko tayari kulijibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (k.n.y. WAZIRI WA AFYA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dr. Mohammed Abully Ally, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo la ugonjwa wa moyo Serikali inalichukulia kwa uzito wake ndio maana kuna hospitali mbalimbali za watu binafsi ambazo zimeanza kutoa matibabu hayo. Kwa mfano Hospitali ya Dr. Massawe, Michokeni imeanza kutoa tiba ya moyo katika upasuaji lakini siyo upasuaji mkubwa hata Muhimbili kuna mpango wa kuleta Wachina kuja kutusaidia. Lakini tatizo la kushirikiana na wataalamu, haina tatizo na hatuwezi kutofautisha wataalamu hao wametokea wapi, wametoka Korea, wametoka China au wametoka India. Suala la tiba ni *universal* ni sawa kabisa .

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishieni kwamba Serikali inafanya jitihada kuhakikisha kwamba baada ya mwaka mmoja miaka miwili tutaweza kutibu wagonjwa wa moyo hapa hapa nchini badala ya kuwapeleka ng’ambo.

Na. 59

**Huduma za Afya ya Akili**

**MHE. JUMA S. KIDUNDA** aliuliza:-

Kwa kuwa binadamu wote wana asili ya uendawazimu kwa mtazamo wa kina; na kwa kuzingatia maana hiyo Wizara ya Afya inacho Kitengo cha Huduma za Afya ya Akili:-

(a) Je, kuna taasisi ngapi za kijamii *(NGOs* na *CBOs)* zinazotoa huduma kwa wagonjwa wa akili nchini?

(b) Kwa kuwa, Shirika la Kimataifa la *Basic Needs* lenye Makao yake Makuu Uingereza limefungua tawi nchini Mkoani Mtwara kama eneo la kuanzia; je, Serikali inalisaidiaje katika kujiimarisha na kujiendeleza?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (k.n.y. WAZIRI WA AFYA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika,napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Kidunda, Mbunge wa Kilindi, kama ifuatavyo:-

(a) Kuna taasisi kadhaa za kijamii *(NGOs* na *CBOs)* zinazotoa huduma kwa wagonjwa wa akili nchini. Taasisi hizo ni pamoja na:-

(i) *CORDAID* toka Uholanzi ambayo hushiriana na *Mental Health Association of Tanzania (MEHATA)* katika kueneza huduma za Afya ya Akili na kutibu waathirika wa madawa ya kulevya.

(ii) Hospitali ya Lutindi, Korogwe inayotoa huduma kwa wagonjwa wa akili. Hospitali hii inamilikiwa na Kanisa la Kilutheri Tanzania na ina vitanda 120.

(iii)Kituo cha Magonjwa ya Akili cha Irente huko Lushoto kinachomilikiwa na Kanisa la Kilutheri Tanzania.

(iv) Shirika la *Basic Needs* toka Uingereza ambalo limefungua ofisi zake hapa nchini na makao yake makuu yako Mtwara wana mpango wa kuanzisha huduma hizo Dar es Salaam.

(v) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kupitia Wizara ya Afya imekuwa na ushirikiano mzuri na *Basic Needs* ikiwa ni pamoja kulikaribisha Shirika hilo kuja Tanzania. Serikali imefanya yafuatayo ili kulisaidia Shirika hili:-

(a) Kutoa mwongozo wa sera hususan kwenye masuala ya ubora wa huduma, usimamizi, rufaa, matumizi ya dawa na sheria za kulinda haki za wagonjwa wa akili.

(b) Wizara inatoa Madaktari Bingwa wa magonjwa ya akili ambao husaidia kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi wa Afya ngazi ya Wilaya, vituo vya afya na zahanati.

(c) Wizara inafuatilia kwa karibu na kusimamia utendaji wa kazi wa *Basic Needs* hapa nchini.

(d) Wizara imeiandalia *Basic Needs* mwongozo wa kuhudumia wagonjwa wa akili ngazi ya msingi kwa lugha ya kiswahili ambao unatumiwa na *Basic Needs.*

**SPIKA:** Mheshimiwa Juma Kidunda, umeridhika. Muda wa maswali umekwisha, kwa hiyo, tunaendelea na mengine. Sasa ni muda wa matangazo Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo yafuatayo:-

Kabla sijafika kwenye Vikao vya Kamati, nitoe matangazo yafuatayo:-

Kwanza semina, kesho ni Jumamosi na tumepanga semina ambayo tutapata maelezo ya Mradi wa Kupeleka Umeme Vijijini hiyo inaitwa *Rural Electrification* hapa hapa kama kawaida kuanzia saa tatu.

Pili, kesho kutwa yaani Jumapili tutakuwa na semina kuanzia saa tano asubuhi ambapo tutapata maelezo kutoka kwa *Unity Trust of Tanzania* kuhusu shughuli zao na jinsi wanavyoziendesha.

Kwa hiyo, ziko hizi semina mbili kesho saa tatu na kesho kutwa saa tano mahali penyewe hapa hapa. Halafu kesho hiyo hiyo Jumamosi kuna mchezo wa mpira wa miguu baina ya Timu ya Wabunge na Timu ya Benki ya *CRDB.* Mchezo huo utaanza saa kumi jioni na lengo lake ni kuchangisha fedha kwa ajili ya wenye shida, watoto waliofiwa na wazazi wao kutokana na ugonjwa wa UKIMWI, Wilaya ya Makete na vilevile kuna watoto hapa Dodoma wenye mtindio wa akili na wao watasaidiwa kutokana na mapato ya mechi hiyo ya kesho.

Kwa hiyo, ni mechi ina lengo nzuri Waheshimiwa Wabunge watakao kuwa na nafasi ni vizuri wakafika kuitia moyo timu yetu na wananchi wengine vile vile watakuwepo.

Sasa vikao vya Kamati. Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Makamu Mwenyekiti wake Mheshimiwa George Lubeleje, anaomba kikao cha Kamati hiyo kifanyike leo katika chumba namba 133 ghorofa ya kwanza baada ya kipindi cha maswali. Mara baada ya kipindi cha maswali Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala mnaombwa kukutana kuhushughulikia Azimio ambalo niliwapelekea.

Kamati nyingine ni Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC),* Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. David Mwakyusa, anaomba wajumbe wa Kamati wa *PAC* wakutane leo saa tano asubuhi chumba namba 227 ghorofa ya pili.

Kamati ya tatu ni ya Uwekezaji na Biashara, Mwenyekiti wake Mheshimiwa William Shellukindo, anaomba wajumbe wakutane kuanzia saa tano asubuhi chumba namba 219 ghorofa ya pili.

Kamati nyingine ni ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, anawatangazia wajumbe kwamba leo saa tano asubuhi kutakuwa na kikao chumba namba 231. Kamati ya Fedha na Uchumi.

Mwisho ni Kamati ya Miundombinu Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo, Mwenyekiti wa Kamati hiyo anawatangazia kwamba kutakuwa na kikao saa tano asubuhi katika ukumbi namba 231 ghorofa ya pili.

Kwa hiyo, tumepanga hivyo kwa sababu hatujaweka Miswada kwenye *Order Paper* isipokuwa ule mmoja wa kwanza sababu yake ni kwamba Kamati zilikuwa hazijakamilisha kushugulikia Miswada hii. Kwa hiyo, tukawapa nafasi wiki yote hii wawe wanakutana kukamilisha kazi yao ili wiki ijayo tutoe kipau mbele kwa Miswada. Wiki hii mnao tulikuwa tunashughulikia Maazimio sababu yake ni hiyo Miswada ilikuwa haijatoka kwenye Kamati. Sasa tunaomba Kamati zikamilishe kazi ili kuanzai Jumatatu ipaumbele kiwekwe kwenye Miswada kuingizwa kwenye *Order Paper.* Mwisho wa matangazo, Katibu endelea na *Order Paper.*

## KAULI ZA MAWAZIRI

### Ufafanuzi Kuhusu Hali Mbaya ya Usalama Wilayani Kasulu

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, tarehe 3 Agosti, 2004 wakati wa Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge yaani Bunge la bajeti, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mbunge wa Kasulu Magharibi, alitoa maelezo binafsi na kutaka ufafanuzi kuhusu hali mbaya ya usalama Wilayani Kasulu.

Mheshimiwa Mbunge alitaka pia kujua hatua zitakazochukuliwa na Serikali katika kudhibiti hali hiyo mbaya. Katika kuthibitisha hali mbaya ya usalama wa watu na mali zao Wilayani Kasulu, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, alitoa mifano ya matukio ya ujambazi wa kutumia silaha ambapo watu mbalimbali walipigwa risasi na kuporwa mali zikiwemo simu za mikononi na fedha taslimu.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa kati ya Januari, 2004 hadi Julai, 2004 kulitokea matukio 14 ya unyang'anyi wa kutumia silaha. Matukio haya yaliwapa wananchi wa Wilaya ya Kasulu wasiwasi mkubwa kuhusu usalama wao na mali zao.

Hata hivyo si kweli kuwa wakati na baada ya matukio ya ujambazi kufanyika, Jeshi la Polisi halikuchukua hatua zozote kukabiliana nayo kama Mheshimiwa Mbunge alivyoeleza. Ukweli ni kwamba wakati wote wa matukio ya ujambazi, polisi wamekuwa wakipambana na majambazi na kuwadhibiti na kwamba doria ziliimarishwa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, ifuatayo ni mifano michache inayothibitisha jitihada za Jeshi la Polisi katika kupambana na uhalifu wa kutumia silaha wilayani Kasulu:-

(a) Tarehe 16 Juni, 2004 majira ya saa nne usiku huko Kasulu, Juma Hungu akiwa nyumbani kwake alivamiwa na majambazi wapato wanne wakiwa na silaha aina ya

gobore, mapanga na marungu na kupora shilingi 100,000/=. Majambazi yalifyatua risasi moja hewani na kumjeruhi ndugu Hungu kwa mapanga pamoja na mke wake.

Baada ya tukio hilo askari waliokuwa doria mjini Kasulu walifika kwenye eneo la tukio na kuokoa maisha ya majeruhi kwa kuwapeleka hospitali. Katika tukio hilo majambazi wawili walikamatwa na kufikishwa Mahakamani Kasulu ambako walifunguliwa mashitaka, kesi Na. CC164/204. Kesi hiyo bado inaendelea kusikilizwa.

(b) Tarehe 16 Juni, 2004 majira ya saa nne na nusu usiku huko kijiji cha Mudyanda, majambazi wanne walivamia nyumba ya Dekasi Petro na kufyatua risasi na kunyang'anya vitu vyenye thamani ya shilingi 430,000/=. Askari waliokuwa doria walikimbilia kwenye eneo la tukio na wahalifu walikimbia baada ya kuwaona askari. Uchunguzi bado unaendelea.

(c) Tarehe 28 Julai, 2004 saa tatu usiku huko Kasulu Bwana Dunia Saya, alivunjiwa duka lake na wezi na kuibiwa bidhaa za dukani pamoja na mali mbalimbali. Kabla hawajabeba mali hizo, polisi waliokuwa doria walifika kwenye eneo la tukio na wezi walipowaona polisi walitoroka bila kubeba kitu chochote. Mali ilirudishwa kwa mwenyewe baada ya kushindwa kuwapata wahalifu. Uchunguzi bado unaendelea.

(d) Tarehe 28 Julai, 2004 yapata saa saba usiku eneo la Mlima Suma, kilometa tisa kutoka Kasulu Mjini, gari lenye namba za usajili T334ABT mali ya Fanuel Mutayabalibwe, likiwa na abiria 14 wakitokea Manyovu kuelekea Kasulu walisimamishwa na majambazi waliokuwa na silaha. Majambazi hao waliwashusha abiria wote na kuwanyang'anya mali mbalimbali zenye thamani ya shilingi 1,100,000/=. Abiria Pascal Kababae alijeruhiwa kwa risasi mguuni. Polisi walifika na walikagua eneo la tukio na waliokota maganda mawili ya risasi kwenye eneo la tukio, mapanga mawili, visu viwili na marungu mawili. Uchunguzi bado unaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika uchunguzi wa matukio yote hayo polisi Wilayani Kasulu walipata taarifa kuwa majambazi yanayojihusisha na uharifu huo ni Mei Rashi, Kasiani Rashid, Rajabu Rashid na Andrew Kemenga. Hawa wote ni wakazi wa Kasulu Mjini wametambuliwa kuhusiana na matukio yote hayo na wamekamatwa na kufikishwa mahakamani kesi Na. CC168/204. Kesi hii inaendelea mahakamani.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, ameendelea kutoa ufafanuzi wake kuwa wakati matukio ya uhalifu wa kutumia silaha unaendelea, polisi waliendelea kutofanya kazi yao ipasavyo akito mfano alieleza kuwa doria inafanywa na polisi kuanzia saa moja na nusu hadi saa mbili usiku tu na vituo vya polisi vinavyopaswa kuwa wazi siku zote hufungwa saa moja na nusu usiku hali inayowafanya majambazi waendelee na vitendo vya ujambazi bila vizuizi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni za utumishi wa Jeshi la Polisi *(PGO)* kifungu Na. 280 askari walioko kwenye doria hufanya kazi kwa muda wa saa sita hadi nane ambapo huruhusiwa kupumzika na askari wengine kuanza zamu ya doria. Kwa utaratibu huo doria inapaswa kufanywa usiku wote na si kwa nusu saa tu.

Mheshimiwa Spika, katika maelezo yake Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, alieleza pia kuwa vituo vya polisi hufungwa saa moja na nusu usiku. Napenda kufafanua kwamba kiutaratibu tunavyo vituo vya aina mbili, aina ya kwanza ni ya vituo vinavyofunguliwa kwa saa ishirini na nne na aina ya pili vituo vinavyofunguliwa mchana tu. Mji wa Kasulu una vituo viwili. Kipo kituo kimoja kikubwa ambacho hufanya kazi saa ishirini na nne kwa siku na hata siku moja hakijawahi kufungwa.

Kituo kingine kidogo kipo kwenye kituo cha mabasi ambacho kwa mujibu wa kanuni za utumishi wa polisi hutakiwa kufungwa saa kumi na mbili jioni. Hata hivyo kutokana na kituo cha mabasi kuwa mbali na kituo kikubwa cha polisi na kwa kuzingatia hali ya usalama Mjini Kasulu kituo cha polisi kwenye *bus stand* kimepewa kibali maalum cha kufanya kazi kkwa saa ishirini na nne ili kusogeza huduma karibu na wananchi. Kwa hiyo, sasa vituo vyote viwili vya polisi Wilayani Kasulu vinafanya kazi saa ishirini na nne kwa siku.

Katika ufuatiliaji wetu tumeridhika kwamba huo ndio utaratibu unaofuata. Hhata hivyo namwomba Mheshimiwa Mbunge atusaidie zaidi ushahidi wa polisi kushindwa kutekeleza wajibu wao katika suala hili ili tuweze kuchukua hatua zipasazo

Mheshimiwa Spika, jitihada mbali mbali zilizofanywa na Serikali zimeweza kupunguza uhalifu Wilayani Kasulu na hivi sasa hali ya usalama Wilayani huko ni afadhali. Aidha, katika kudhibiti uhalifu Wilayani Kasulu na sehemu nyingine za nchi Serikali inaendelea kuchukua hatua zenye lengo la kuimarisha utendaji wa jeshi la polisi ikiwa ni pamoja na hizi zifuatazo:-

(i) Kuimarisha doria na kuhakikisha wahalifu hawapati mwanya wa kufanya uhalifu.

(ii) Kusambaza vyombo vya kisasa vya mawasiliano kama *radio call* katika vituo vya polisi na kuhakikisha kuwa askari wawapo kwenye doria wanakuwa na vyombo vya mawasiliano.

(iii) Kuimarisha ushiriki wa raia katika ulinzi kama mgambo, sungusungu na makampuni binafsi ya ulinzi. Vyombo hivyo vitahamasishwa na kupewa mafunzo muhimu ili vishiriki kikamilifu katika ulinzi wa raia na mali zao chini ya utaratibu wa polisi jamii.

(iv) Kuhamasisha raia wema washirikiane na polisi katika kuwafichua wahalifu.

(v) Kuendelea na mpango wa kupeleka askari wa nyongeza katika Mikoa na Wilaya zenye makambi ya wakimbizi ikiwemo Kasulu ili kuhakikisha usalama wa maeneo hayo.

(vi) Kuendeleza juhudi za kuwarudisha makwao wakimbizi wote wa Burundi na Kongo *(DRC)* waliobakia. Hatua hii itapunguza wimbi la uhalifu katika mikoa ya Kigoma na Kagera.

(vii) Kuimarisha usafiri kwa Jeshi la Polisi ili liweze kupambana na uhalifu kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe na Bunge lako Tukufu kwa kuidhinisha ongezeko la Bajeti ya Jeshi la Polisi mwaka hata mwaka. Ongezeko la Bajeti tunalopata linatuwezesha kununua vyombo vya usafiri na mawasiliano, sare za askari na kuajiri askari wapya na hivyo kupunguza pengo la upungufu wa askari. Hayo yote yataliwezesha Jeshi la Polisi kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi na litawaongezea askari nguvu na uwezo wa kupambana na wahalifu.

Ni matumaini yangu kuwa kwa kadri Bajeti ya Wizara yangu itavyokuwa bora zaidi Wizara itaweza kudhibiti uhalifu kwa ukamilifu zaidi. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge kwa kutembelea sehemu mbalimbali nchini na kutoa maelekezo juu ya namna bora ya kuimarisha usalama wa raia na mali zao. Maelekezo hayo yamekuwa msaada mkubwa sana kwa Wizara katika kutekeleza majukumu yake. Kwa mfano, hivi karibuni Kamati hiyo imetembelea Mkoa wa Kigoma na tayari imetupatia maelezo mahususi ya kuimarisha usalama katika Wilaya ya Kasulu na Mkoa mzima wa Kigoma.

Mwisho napenda kutumia nafasi hii kumwomba Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mbunge wa Kasulu na Magharibi na Waheshimiwa Wabunge wote waendelee kuhamasisha wananchi washirikiane na Jeshi la Polisi katika kupambana na wimbi la uhalifu linalotishia usalama wa raia na mali zao humu nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Asante, Katibu *agenda* inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

## M AAZIMIO

**SPIKA:** Namwita mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, awasilishe Maazimio ya Wizara yake.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kuwa Bunge lako sasa likubali kuridhia Maazimia yafuatayo:-

Azimio la Kuridhia Upanuzi wa Hifadhi ya Arusha.

Azimio kuhusu Kuanzishwa kwa Hifadhi Mpya ya Taifa ya Kitulo.

Azimio kuhusu Kupanua Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro.

Azimio la Kuridhia Upanuzi wa Hifadhi Mpya ya Taifa ya Saadani.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa pia kumshukuru Mheshimiwa Anna Makinda, Mbunge na Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira pamoja na wajumbe wote wa Kamati ambao wamejadili hoja na Maazimio haya na kuchangia katika uboreshaji wa hoja hizi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha hoja na Azimio moja moja kwa mtiririko ufuatao:-

Kwanza kuhusu Kupanua Hifadhi ya Taifa ya Arusha.

Mheshimiwa Spika, misitu ya asili ya Meru na Ngurudoto ipo katika Mlima Meru na ina ukubwa jumla kilometa za mraba 415. Misitu hii inasimamiwa na sheria ya misitu ya mwaka 2002. Hoja hii inataka kwamba misitu tajwa inasimamiwa na sheria ya Hifadhi ya Taifa sura 412 na iunganishwe na Hifadhi ya Taifa ya Arusha. Mlima Meru unaongezeka umaarufu wake kutokana na kukua kwa shughuli za utalii kwa kupanda Mlima na kuwa ni chanzo cha maji kwa maeneo yanayozunguka mlima huo na yale ya tambarare.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya kisheria katika usimamizi wa misitu tajwa hakutaathiri makazi na shughuli za kiuchumi za wananchi kwa sababu kisheria misitu hii ilikuwa ni misitu ya hifadhi, hivyo wananchi walikuwa hawaruhusiwi kuishi humo au kuitumia.

Mheshimiwa Spika, kupanuliwa kwa hifadhi ya Taifa ya Arusha kutawezesha kuboresha ardhi owevu zilizopo katika maeneo ya tambarare za Wilaya ya Arumeru na bonde la Mto Pangani hivyo kuzipa ardhi owevu hizo uwezo wa kutoa huduma za kijamii na kiuchumi inavyostahili. Kutunzwa kwa vyazo hivi vya maji kutachangia ubora na wingi wa maji yanayoingia bwawa la Nyumba ya Mungu na maporomoko ya Hale.

Maporomoko ya Hale na bwawa la Nyumba ya Mungu hutoa nishati inayotumika katika sehemu kubwa ya nchi yetu. Maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, kilimo, viwanda na biashara katika miji ya Arusha na Moshi na vijiji vinavyozunguka Milima hii yatapatikana kwa uhakika na kwa uendelevu. Vile vile kupanua hifadhi kutaboresha shughuli za utalii katika mlima Meru.

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza kwamba ni muhimu Hifadhi ya Taifa ya Arusha ikapanuliwa ili kutoa ulinzi kwa vyanzo vya maji na kuboresha utalii kwa kupanda mlima katika Mlima Meru.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha Azimio la Kuridhia Kupanua Hifadhi ya Taifa ya Arusha.

KWA KUWA sera ya Taifa ni kudumisha hifadhi endelevu kwa kuanzisha na kuboresha maeneo wakilishi yaliyohifadhiwa na kulinda maeneo hayo katika mtandao wa hifadhi za Taifa;

NA KWA KUWA pia ni sera ya Taifa kutunza maeneo yote muhimu kwa vyanzo vya maji;

NA KWA KUWA hayo yote yatafanikiwa ikiwa maeneo husika yatasimamiwa na sheria ya hifadhi ya Taifa;

NA KWA KUWA imebainika kuwa Misitu ya Meru na Nguludoto imepoteza uwezo wake wa kuwa vyanzo vya maji kutokana na uharibifu unaoendelea;

NA KWA KUWA hifadhi ya Taifa ya Arusha kwa ajili ya udogo wake haikidhi hitaji la uhifadhi endelevu;

NA KWA KUWA msitu ya Meru na Nguludoto ikipandishwa hadhi na kujumuishwa katika Hifadhi ya Taifa ya Arusha haja zote za utuzaji wa vyanzo vya maji na uhifadhi endelevu zitahakikishiwa;

NA KWA KUWA ili misitu ya Meru na Nguludoto kupandishwa Hifadhi ya Taifa ya Arusha ridhaa ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inahitajika.

HIVYO BASI Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa kifungu cha tatu na nne cha sheria ya Hifadhi ya Taifa sura 412 katika kikao chake cha Kumi na Saba kilichoketi tarehe 5 Novemba, 2004 kimeridhia Hifadhi ya Taifa ya Arusha ipanuliwe kutoka kilometa za mraba 137 hadi kufikia kilomeita za mraba 552 kwa kujumuisha na kupandisha hadhi misitu ya asili ya Nguludoto na Meru yenye ukubwa kilometa za mraba 415 hivyo kufanya Hifadhi ya Arusha kuwa na mipaka mipya.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ni kuomba kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili na hatimaye kuridhia kuanzisha hifadhi mpya ya Taifa ya Kitulo yenye ukubwa kilometa za mraba 405.

Mhesimiwa Spika, hifadhi mpya ya Kitulo itaanzishwa katika maeneo yafuatayo:-

(i) Eneo la Kitulo ambalo lipo katika Uwanda wa Juu wa Nyanda za Juu Kusini. Uwanda huu wenye ukubwa wa kilometa za mraba 135 ni sehemu ya pekee kabisa Tanzania kwa kuwa na mimea inayotoa maua yenye thamani kubwa ambayo hayapatikani sehemu yoyote ya nchi hii.

(ii) Msitu wa Livingstone una kilometa za mraba 243 na ni sehemu ya Mlima ya Livingstone inayoaminika kuwa kilele chake ni cha tatu kwa urefu katika Tanzania baada ya Mlima Kilimanjaro na Meru. Aidha, misitu wa Livingstone na uwanda wa Kitulo ni makazi ya ndege aina ya *blue swallow* ambao hapa nchini wanapatikana sehemu hii pekee ndege hao wamekwa katika daraja la wanyama walioko katika hatari ya kutoweka katika ukanda wa Afrika wa Mashariki.

Kutokana na makazi yao kuharibika na kupotea, eneo hili linalo ndege wapatao 600,000 mpaka 800,000 tu na taarifa za kisayansi zinaonesha kwamba makazi yake katika eneo la Kitulo haya kuhifadhiwa na yanaathiriwa na kilimo wakati makazi ya msitu wa Livingstone yanaathiriwa na ukataji miti. Msitu asili wa Numbe wenye ukubwa wa kilometa za mraba 27 msitu huu unahifadhi maporomoko na ni chanzo kikuu cha Mto Ruaha.

Mheshimiwa Spika, Uwanda wa Juu wa Nyasi kwa pamoja na msitu wa asili wa hifadhi ya Livingstone na ule wa Bonde la Numbe ni vyanzo muhimu sana vya maji kwa ardhi owevu za Uwanda wa Nyasi kwa Usangu Bonde la Mto la Ruaha, Mabwawa ya Mtera na Kidatu na Bonde la Mto Rufiji kwa upande wa Kaskazini na kwa upande wa Kusini maeneo hayo yote yanadumisha ardhi owevu ya Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa maeneo haya hivi sasa unaathiri kwa kiwango kikubwa na matumizi yasiyo endelevu katika maeneo hayo, matumizi hayo ni pamoja na kilimo kisicho endelevu cha viazi kinachosababisha mmomonyoko wa udongo, uvunaji haramu wa misitu ya asili, uvunaji na usafirishaji haramu wa mimea kipekee aina ya *Osheets*.

Mheshimiwa Spika, hoja hii inalenga maeneo ambayo yanazo sifa zote za kuwa kivutio kikubwa cha utalii Ukanda wa Kusini mwa Tanzania. Mandhali nzuri ya eneo hilo, ndege wapatikanao eneo hilo tu na mimea pekee hata katika hali halisi ya sasa inawavutia watalii waliobahatika kufika au kuelewa eneo hilo.

Ongezeko la mtandao wa maeneo ya kufanyika utalii katika Ukanda wa Kusini mwa nchi utaboreshwa sana ikiwa hifadhi mpya itaanzishwa eneo la Kitulo.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa hifadhi inayopendekezwa kutawezesha nchi yetu kutekeleza Mikataba Kimataifa ya Wanyamapori wahamao pamoja na Mikataba mingine mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na wananchi wa vijiji vinavyozunguka na mamlaka mbalimbali zilishirikishwa katika kuandaa hoja hii. Katika kuanzisha hifadhi hii italazimu kuwahamisha watumishi wa mifugo iliyoko Kitulo Na. 5 cha shamba la mifugo na kuwaweka sehemu ya shamba ambayo haitajumuisha katika eneo la hifadhi inayopendekezwa.

Vilevile shirika la hifadhi la taifa latekeleza programu ya ujirani mwema ambapo wananchi watahamasishwa na kuhakikishiwa kwamba wanafaidika na kuwepo kwa hifadhi hiyo.

Mheshimiwa Spika, ningependa kusisitiza kwamba hifadhi mpya kitulo itachangia katika kukua kwa utalii kusini mwa nchi yetu itatoa ajira kwa wananchi wanaozunguka eneo hilo na itachangia kukua kwa uchumi pamoja na kuhifadhi mazingira na mali asili kwa ujumla kwa kulinda vyanzo vya maji.

Baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha Azimio la Kuanzisha Hifadhi hiyo.

KWA KUWA ni sera ya taifa kutambua na kuanzisha mfululizo wa mtandao wa maeneo ya Hifadhi ya Maliasili wakilishi yaliyohifadhiwa kisheria kwa hadhi ya juu kabisa;

NA KWA KUWA Hifadhi ya Taifa ni mtandao wa maeneo yaliyohifadhiwa kwa hadhi ya juu kabisa kisheria kwa ajili ya uhifadhi wa mali ya asili kwa ajili ya manufaa ya jamii ya sasa na urithi wa vizazi vijavyo;

NA KWA KUWA ili jamii ya sasa inufaike kwa kuwezesha kwa uendelevu kwa nchi nzima ni muhimu kuwepo mtandao wa kutoshereza wahifadhi ya Taifa;

NA KWA KUWA kuanzishwa Hifadhi ya Taifa Kitulo kutaboresha mtandao wa maeneo ya utalii wenye mzunguko unaojumuisha Mwambao wa Bahari ya Hindi, Magofu ya kihistoria Bagamoyo na Kilwa, Pori la Akiba la Selu, Hifadhi za Taifa za Mikumi, Ruaha na Katavi;

NA KWA KUWA eneo lote la Kitulo linahifadhi vyanzo muhimu vya maji ya Mito ya Ruaha na Rufiji;

NA KWA KUWA ili hifadhi hiyo ianzishwe ni budi Bunge la Jamhuri la Muungano wa Tanzania liweze kuridhia;

KWA HIVYO BASI Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa kifungu cha tatu na cha nne cha sheria ya Hifadhi ya Taifa sura 412 katika Kikao chake cha Kumi na Saba kilichoketi kati ya tarehe 5 Novemba, 2004 mpaka 11 Novemba, 2004 limeridhia Hifadhi mpya ya Taifa ya Kitulo yenye ukubwa wa kilometa za mraba 405 lianzishwe kwa kujumuisha msitu wa Hifadhi wa Livingstone wenye ukubwa wa kilometa za mraba 243 msitu wa Hifadhi wa Bonde la Numbe wenye ukubwa wa kilometa za mraba 27 na sehemu ya shamba la ng'ombe wa maziwa la Kitulo lenye ukubwa kilometa za mraba 127.

Mheshimiwa Spika, hoja ya tatu ni ile ya Kuridhia Kupanua Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, msitu wa asili wa Mlima Kilimanjaro una ukubwa kilometa za mraba 912 na unasimamiwa na sheria ya misitu ya mwaka 2002. Hoja hii nataka kwamba msitu tajwa usimamiwe na sheria ya Hifadhi za Taifa sura 412 na iunganishwe na Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro. Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro ilianzishwa Mwaka 1973 na ni maarufu nchini na ulimwenguni kwa utalii wa kupanda Mlima na ya tambuliwa Kimataifa kama eneo la urithi wa dunia.

Kutokana na urefu wa mlima huu ipo manuai ya kipekee kabisa ambayo haipatikani katika sehemu nyingine kwenye Bara la Afrika misitu ya asili katika Mlima huu inahifadhi vyanzo vya maji ambayo ni muhimu kwa uchumi wa wananchi wanaoishi

kuzunguka hifadhi. Hata hivyo upo uharibifu mkubwa wa mazingira unaosababishwa na uvunaji haramu wa misitu. Uvunaji wa wanyama pori na ulishaji wa mifugo kinyume cha sheria, matumizi haya husababisha mioto mikali na kuharibiwa kwa udogo hivyo kupunguza uwezo wa udogo kuhifadhi maji.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya kupanua Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro ni kuboresha uhifadhi wa vyanzo vya maji na udogo kwenye miteremko mikali kulinda manuai na kuongeza wigo wa utalii katika mlima huu.

Misitu husika, msitu husika uko chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Wadau wote ikiwa na wananchi na mamlaka mbalimbali zilihusishwa katika maandalizi ya hoja na ambao walitoa ridhaa. Makazi ya wananchi hayatahathiriwa kwa sababu kisheria msitu wa Kilimanjaro ni msitu wa hifadhi. Hivyo wananchi hawaruhusiwa kuishi humo.

Mheshimiwa Spika, Kupanuliwa kwa Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro utawezesha yafuatayo:-

(i) Kutoa ulinzi madhubuti kwa vyanzo vya maji na hivyo kuboresha aridhi owevu zilizopo katika maeneo ya tambarare za Mkoa wa Kilimanjaro na Bonde la Mto Pangani na kuzipa uwezo wa kutoa huduma za kijamii na kiuchumii inavyostahili.

(ii) Kupatikana kwa uhakika na kwa uendelevu wa maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, kilimo, viwanda na biashara katika mji wa Moshi na vijiji vinavyozunguka mlima huu.

(iii) Kuboresha shughuli za utalii, mazingira na Banuai za Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, wananchi hawakuwa wanategemea mazao ya miti kutoka msitu huu kwa sababu eneo la nusu maili linalotumiwa na wananchi kwa ajili ya kujipatia mazao ya misitu halitajumuishwa katika Hifadhi inayopendekezwa.

Vile vile Shirika la Hifadhi ya Taifa litaendelea kutekeleza programu za ujirani mwema inayojumuisha kuwezesha wananchi kupanda miti katika ardhi yao ili kuhifadhi mazingira yanayozunguka hifadhi hiyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza kwamba Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro ndio kivutio kikubwa cha utalii katika nchi yetu na tunahitaji kuhakikisha kwamba tunaendelea kupata matunda ya mlima kiendelevu. Pamoja na kupata faida nyingine ususani maji ambayo ndio uhai wa bonde la Mto Pangani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha Azimio lifuatalo:-

KWA KUWA sera ya Taifa ni kudumisha Hifadhi endelevu kwa kuanzisha na kuboresha maeneo wakilishi yaliyohifadhiwa na kulindwa Banuai katika mtandao wa Hifadhi za Taifa;

NA KWA KUWA pia ni sera ya Taifa kutunza maeneo yote muhimu kwa vyanzo vya maji;

NA KWA KUWA hayo yote yatafanikiwa ikiwa maeneo husika yatasimamiwa na sheria za Hifadhi ya Taifa;

NA KWA KUWA umebainika kuwa msitu wa Kilimanjaro umepoteza uwezo wake wa kuwa vyanzo vya maji kutokana na uharibifu unaoendelea;

NA KWA KUWA hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro kwa ajili ya udogo wake haukidhi hitaji la uhifadhi endelevu na kutoa ulinzi madhubuti kwa vyanzo vya maji;

NA KWA KUWA msitu wa asili wa Kilimanjaro ukipandishwa hadhi ya kujumuishwa katika hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro haja zote za utunzaji wa vyanzo vya maji ya uhifadhi endelevu zitahakikishiwa;

NA KWA KUWA ili msitu wa kilimanjaro upandishwe hadhi na kujumuishwa katika hifadhi ya taifa Kilimanjaro, ridhaa ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linahitajika;

HIVYO BASI Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Kikao chake cha Kumi na Saba kilichoketi tarehe 5 Novemba, 2004 imeridhia Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro ipanuliwe kutoka kilometa za mraba 756 hadi kilometa za mraba 1668 kwa kupandisha hadhi na kujumuisha msitu wa asili wa Kilimanjaro wenye kilometa za mraba 912 hivyo kuifanya Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro kuwa na mipaka mipya.

Mheshimiwa Spika, Azimio la mwisho la nne ni mapendekezo ya kuanzisha Hifadhi mpya ya Taifa ya Sadani sio kupanua, lakini ni kuanzisha Hifadhi mpya ya Taifa Sadani.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja tena kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili hatimaye kuridhia kuanzisha Hifadhi hii mpya ya Taifa ya Sadani.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi mpya ya Taifa ya Sadani inapendekezwa ipo kando kando mwa Bahari ya Hindi lilipo pori la akiba la Sadani, ambalo linasimamiwa na sheria hifadhi ya wanyama pori namba 12 ya 1974. Hifadhi inapendekezwa kuanzishwa itajumuisha maeneo yafuatayo: Hifadhi ya Msitu wa Zaraninge unaosimamiwa na sheria ya Serikali za mitaa ya 1982 *Ranch* ya mifugo ya Mkwaja ambayo imenunuliwa na Wizara ya Maliasili kutoka kwa mwekezaji Ufukwe, Madete na eneo la Kisauke mahali Mto Wami unapoingia Baharini. Kuanzisha Hifadhi mpya ya Taifa inajumuisha maeneo haya utafanya maeneo haya kusimamiwa na sheria hifadhi ya Taifa sura 112.

Mheshimiwa Spika, hifadhi inapendekezwa ndio eneo la Hifadhi ya Wanyama Pori pekee nchini ambayo inapakana na ufukwe wa Bahari. Wanyama pori waliopo katika eneo hili ni pamoja na wale waliotokana na kupandikizwa 1968 ilipoanzishwa Pori la Akiba la Sadani. Eneo la Sadani ambalo linajumuisha kijiji cha Sadani ni maeneo yenye hazina kubwa ya historia na utamaduni.

Wizara inaona kwamba eneo hili ni muhimu sana katika kuendeleza utalii na katika uhifadhi wa wanyama pori na mazingira yao mambo ya kale na historia na kutokana na hayo eneo la Sadani linahitaji ulinzi madhubuti na mikakati maalum ya kuendeleza utalii kwa kuunganisha eneo hili na maeneo mengine maarufu ya utalii nchini.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili sehemu ya Wadete ni eneo la kipekee kutokana na umuhimu wake Kimataifa. Hii ni eneo katika Pwani ya Bahari ya Tanzania na ufahamika kuwa na viumbe adimu kama tasa wa kijani wa Baharini ambao hutaga na kuangua mayai humo, maeneo yatakayounda hifadhi ya Taifa ya Sadani.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza awali hifadhi mpya ya Taifa Sadani inapendekezwa itajumuisha pori la akiba la Sadani lenye ukubwa wa kilomita za mraba 250 na maeneo mengine ambayo kwa pamoja yanafanya hifadhi inapendekezwa kuwa na ukubwa wa Kilomita za mraba 1210. Inayojumuisha makazi mbalimbali ya wanyama pori kama ifuatavyo: Ranchi ya Mkwaja yenye ukubwa wa Kilomita za mraba 460 yenye wanyama wengi hususan tembo, nyati na kudu. Sehemu ya kijiji cha Mkange Kwamsisi lenye ukubwa wa Kilomita za mraba 115.

Mheshimiwa Spika, ufukwe wa Madete wenye ukubwa wa Kilomita za mraba 80 unaojumuisha eneo la ufukwe wenye upana wa Km 6. Eneo hili la Bahari ambalo lina urefu wa kilomita za mraba 10 kuingia Baharini na upana wa Km 10 kwa upande wa Bahari ni eneo muhimu kwa ulinzi wa kasa wachanga.

Kisauke sehemu ya Mto Wami lenye ukubwa wa Kilomita za mraba 50 za msitu aina ya Mikoku. Hii ni eneo muhimu kama masalia ya kamba na viumbe wengine wa Baharini.

Mheshimiwa Spika, majadiliano na Wadau. Ili kupata maeneo ambayo hivi sasa yanatumiwa na Wananchi kwa mahitaji mbalimbali, Wizara ilifanya majadiliano na wadau hususan Wananchi na Madiwani wa Halmashuri za Wilaya za Handeni, Pangani na Bagamoyo na kamati za maendeleo za kata kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, faida itakayopatikana kwa kuanzisha Hifadhi mpya ya Saadani.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa hifadhi mpya ya Sadani kutatoa nafasi ya Wananchi wa Wilaya ya Handeni, Pangani na Bagamoyo kupata ajira katika hifadhi. Wigo wa uwekezaji utapanuka na nafasi itaongezeka ya kuendeleza utalii hususan ule wa utamaduni, historia na utamaduni wa Pwani.

Mheshimiwa Spika, hifadhi inayoundwa itawezesha kukua na kuboreshwa kwa utalii Kusini mwa Tanzani. Visiwa vya Pemba na Zanzibar na watalii wanaotembelea nchi yetu wataweza kuona vivutio vingi na kuandaa safari za kitalii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo napenda sasa kusoma azimio kama ifuatavyo:-

**Azimio la Kuridhia Kuanzisha Hifadhi mpya ya Taifa ya Sadani**

KWA KUWA ni sera ya Taifa kutambaua na kuanzisha mfululizo wa mtandao wa maeneo ya hifadhi ya Maliasili wakilishi yaliyohifadhiwa kisheria kwa hadhi ya juu kabisa na kwa kuwa Hifadhi ya Taifa ni mtandao wa maeneo yaliyohifadhiwa kwa hadhi ya juu kabisa kisheria kwa ajili ya uhifadhi wa Maliasili kwa ajili ya manufaa ya jamii ya sasa na urithi wa vizazi vijavyo.

KWA KUWA ili jamii ya sasa inufaike kwa kuweza utalii ufanyike kwa uendelevu kwa nchi nzima ni muhimu kuwepo mtandao wa kutosheleza wa Hifadhi za Taifa, na kwa kuwa kuanzishwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Sadani kutaboresha mtandao wa maeneo ya utalii wenye mzunguko unaojumuisha mwambao wa Bahari ya Hindi, magofu ya kihistoria Bagamoyo na Kilwa, pori la akiba la Seluu, Hifadhi za Taifa Mikumi, Ruaha na Katavi, na kwa kuwa eneo hili la Sadani ni eneo la kipekee wakilishi katika ukanda wa Pwani inajumuisha eneo la ufukwe wa Bahari unaoungana na eneo la hifadhi ya wanyama pori kujumuisha katika mtandao wa Hifadhi wa Taifa kwa urithi wa vizazi vijavyo.

KWA KUWA, ili hifadhi hiyo ianzishwe ni budi Bunge la Jamhuri la Muungano wa Tanzania kuridhia.

HIVYO BASI, Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mujibu wa kifungu cha 3 na 4 sura ya 412 katika kikao chake cha 17 kilichoketi tarehe 5 Novemba, 2004 liweze kuridhia Hifadhi ya Taifa ya Sadani yenye ukubwa wa Kilomita za mraba 1210 ianzishwe kwa kujumuisha pori la akiba la Sadani, Hifadhi ya Misitu ya Zaraninge, Ranchi ya Mkwaja, sehemu ya kijiji cha Makange Kwamsisi, sehemu ya Madete Kijiji cha Mkwaja, Kisauke, Mto Wami na sehemu ya kijiji cha Chanyuki.

Mheshimiwa Spika, Kwa pamoja naomba kuwasilisha.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**Maoni ya Kamati kuhusu Maazimio manne ya Bunge kuridhia yaliyowalishwa na Waziri wa Maliasili na Utalii.**

**MHE. HASSAN R. KHATIB (k.n.y. MHE. ANNE S. MAKINDA - MWENYEKITI KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA):**Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kuchukua fursa hii kwa niaba ya Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, kushukuru kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni ya Kamati kuhusu Maazimio manne kurithia yaliyowasilishwa mbele ya Kamati na Waziri wa Maliasili na Utalii kwa kuzingati kanuni ya 889 (Kanuni ya Bunge toleo la 2004). Aidha namshukuru Mheshimiwa Zakia H. Meghji Waziri wa Maliasili na Utalii, Katibu Mkuu wake Bwana Solomoni Udungo na watendaji wake wakuu wa Wizara hii, kwa kazi nzuri waliofanya kuandaa Maazimio hayo na hivyo kuifanya kazi yetu ya kujadili na kuchambua ndani ya Kamati yetu kuwa rahisi sana.

Mheshimiwa Spika, Maazimio hayo ni kama yafuatayo:-

* Azimio la kuridhia kuanzishwa kwa Hifadhi mpya ya Taifa ya Sadani.
* Azimio la kuridhia upanuzi wa Hifadhi ya Arusha.
* Azimio la kuridhia upanuzi wa Hifadhi ya Kilimanjaro.
* Azimio la kuridhia kuanzishwa kwa Hifadhi mpya ya Taifa Kitulo.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali yetu kwa kuamua kuridhia Maazimio hayo ya kulinda mazingira ya Hifadhi hizi za Taifa. Ili kuepukana na madhara mbalimbali ambayo yameanza, yatakayoweza kutokea endapo hatuyaridhii kama ipasavyo. Kwani kwa kufanya hivyo nchi yetu na Wananchi wake kwa ujumla watanufaika vya kutosha.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati, Kamati imepongeza Serikali kuhusiana na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kuendelea na juhudi zake kulinda mazingira ya Hifadhi zetu za Taifa kwani mchango mkubwa katika pato la Taifa unaendelea. Unaendelea kuongezeka kwa mwaka kutokana na utunzaji mzuri wa Hifadhi mbalimbali nchini mwetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu inakubaliana na hoja ya Waziri wa Maliasili na Utalii kuhusu mapendekezo ya kuanzisha Hifadhi mpya ya Taifa ya Sadani yenye ukubwa wa Kilomita za mraba 1210 inayojumuisha pori la akiba la Sadani, Hifadhi ya misitu ya Zaramige, Ranchi ya Mwakaja, sehemu ya kijiji cha Mkange Kwamsisi, sehemu ya Padete kijiji cha Mkwaja, Kasauke, ambayo ni mdomo wa Mto Wami na Chunyiko. Kamati imeona kuwa kweli ipo lazima kubwa ya historia ya uchumi katika maeneo hayo ya Hifadhi yanayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukweli huo eneo hili ni muhimu sana katika kuendeleza utalii na uhifadhi wa wanyama pori na mazingira yao na mambo ya kale. Pia Kamati inapongeza Wizara kwa kufanya mawasiliano na wadau na kupata ridhaa yao kabla ya kuamua kuanzisha hifadhi hii. Yaani Wananchi, Madiwani na Halmashauri ya Wilaya za maeneo husika. Kwani kwa kufanya hivyo Wananchi wa Wilaya husika watapata ajira, wigo na uwekezaji utapanuka. Aidha nafasi itaongezeka na kuendeleza utalii katika ukanda wa Pwani wa Bahari ya Hindi. Kwa hiyo tunaishauri Wizara kuweka ulinzi na mikakati madhubuti ili kuendeleza Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, hoja ya Waziri kuhusu mapendekezo ya kupanua Hifadhi ya Taifa ya Arusha ni ya msingi kabisa, hivyo basi Kamati yetu imeridhia na sababu za Serikali kuamua kufanya hivyo. Ni ukweli usiofichika kuwa kupanua kwa Hifadhi hii kutokana na Kilomita za mraba 137 hadi kufikia 552 kutawezesha misitu na Mngurudoto na Meru kuhifadhi vyanzo vya maji na kuhifadhi udongo kwenye miteremko mikali ya milima Meru. Maeneo hayo yana utajiri mkubwa wa aina mbalimbali za mimea na wanyama pori. Aidha Kamati inapongeza Wizara kwa juhudi zake za kuchangia ubora wa wingi wa maji kutokana na milima hii yatakayokuwa yakiingia katika Bwawa la Nyumba ya Mungu na maporomoko ya Hale ili kuongeza nishati inayotumika katika sehemu kubwa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha upatikanaji wa ajira kutokana na kupanuka kwa shughuli za Utalii katika maeneo yaliyotajwa ya Azimio hili Kamati inaishauri Wizara kupanga utaratibu mzuri zaidi kwa watalii kupanda milima Meru, na kuimarisha ulinzi wa misitu Nangurudoto na Meru. Kwa kufanya hivyo tuna hakika kuwa pato la Taifa litaendelea kukua kutokana na shughuli za utalii katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia imekubaliana na madhumuni ya hoja inayopendekezwa na kupanua Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro kutoka Kilomita za mraba 756 hadi 1668 ili kuongeza umaarufu nchini na Ulimwenguni kwa ujumla wa utalii na kwa kupanda milima. Aidha manufaa mengine yatakayotokana na kuridhia Azimio hili ni kuhakikisha uhifadhi wa vyanzo vya maji na udongo kwenye miteremko mikali ikiwa ni pamoja na kulinda bainiwai na uvunaji haramu wa misitu na kusongwa na makazi ya mashamba.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa ongezeko la eneo la misitu hii pia itapanua wigo wa utalii, ambao ni muhimu kwa uchumi wa nchi yetu kwa kuwa hifadhi ya mimea Kilimanjaro ndio kivutio kikubwa cha utalii nchini. Basi hatuna budi kuridhia makusudio ya Azimio hili ili kujihakikishia kuendelea kupata matunda mazuri ya mlima huu kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kuridhia Azimio hilo la mwisho ambalo linahusu kuanzishwa kwa hifadhi mpya ya Kitulo, yanayofanyiwa na Kamati yetu ili kulinda umuhimu wa maeneo yaliyotajwa katika Azimio hili ambayo yanaendelea kuathiriwa kwa kiwango kikubwa kutokana na matumizi yasio endelevu kiasi cha kuporomosha uwezo wa kutunza mazingira yake pia Kamati inaunga mkona hoja.

Hoja hii kwa kuwa itatekeleza mkakati wa Sera ya kulinda bainiyai kukuza maendeleo kijamii na kiuchumi na Watanzania, ikiwa ni pamoja na kukuza utalii katika ukanda wa Kusini mwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha uhifadhi wa Maliasili Azimio katika hifadhi hii Kamati inashauri Serikali kuwa, kuweka ulinzi wa uhakika katika uwanda wa Usangu, Mto Ruaha, Mabwawa ya Mtera, Kidatu na Mto Rufiji. Mwisho.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maoni na ushauri huu sasa naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Kamati ya Maliasili na Mazingira imejadili na kuchambua Maazimio yote haya ambayo yamezingatia mahitaji ya nchi.

Kwa hiyo, basi Kamati inaomba Waheshimiwa Wabunge kuyaridhia Maazimio hayo na hatimaye kuyaridhia ili Serikali iweze kutekeleza ipasavyo kwa manufaa ya nchi yetu na Wananchi wake kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. SALIM OMAR ALI (k. n. y. PHILLEMON NDESAMBURO - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII):** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwasilisha maoni ya kambi ya upinzani kuhusu hoja ya Waziri wa Maliasili na Utalii kwa mujibu wa kanuni ya Bunge kifungu cha 43 na 45c.

Mheshimiwa Spika, kambi ya upinzani haina pingamiza na kuridhia upanuzi wa Hifadhi ya Arusha kwa kuwa Wananchi wa maeneo husika wako radhi kwa hilo na Serikali imefuata taratibu zinazotakiwa kwa hilo. Maoni ya kambi ya upinzani kuhusu hoja ya Waziri kuanzisha Hifadhi mpya ya Taifa ya Kitulo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuipitia hoja ya Waziri kwa kundani kifungu cha pili kinachoelezea chimbuko na madhumuni ya hoja, kipengele kinachosema kuwa kilimo kisichoendelevu cha viazi kinachosababisha mmomonyoko wa udongo.

Mheshimiwa Spika, uhai wa Wananchi wa maeneo hayo unategemea kiasi kikubwa cha kilimo cha viazi. Je, Serikali imewatengea maeneo mapya wananchi wa maeneo hayo ili yaendelee na shughuli zao za kilimo?

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ni kwamba Tanzania tuna Chuo Kikuu Cha Kilimo na vyuo vingine vinavyofundisha jinsi ya kutumia mbinu bora za endelevu za kilimo, na isitoshe kila mwaka kuna wahitimu wa shahada na stashahada za kilimo. Sasa Mheshimiwa Waziri anavyotoa hoja ya kilimo kisichoendelevu ina maana ya kuwa Waziri mwenzake wa kilimo bado hajafanya homework yake kama inavyotakiwa. Kama mpaka sasa miradi na mashirika yasiyo ya Kiserikali yanayoshughulikia kilimo Iringa yanatoaje tathmini ya utendaji kazi zao? Na nani anayetakiwa kuwasaidia katika kufanya kilimo kiwe endelevu na kuzuia mmomonyoko.

Mheshimiwa Spika, katika hoja ya Mheshimiwa Waziri haisemi kuwa Wananchi au wanakijiji wanaozunguka Hifadhi Taraji kuwa wamekubali na wamelipwa fidia bali inasema watumishi wa Serikali tu na mifugo yao. Kwa nini Waziri hazungumzii Wananchi wengine ambao watahamishwa katika makazi yao na kulipwa fidia. Huu ni ubaguzi kitu ambacho kambi ya upinzani haikubaliani nacho.

Mheshimiwa Spika, kambi ya upinzani inaona kuna umuhimu wa Serikali kuieleza Bunge lako Tukufu ridhaa ya wanavijiji wanaozunguka Hifadhi Taraji ambayo maeneo yao yametengwa kuwa Hifadhi na fidia yao iko tayari au bado. Kwani hoja hii ikisharidhiwa na Bunge lako basi hata fidia yao itakuwa ni ngumu na vyombo vya dola vitafanya kazi yake ya kuhamisha na ikibidi kuchoma mashamba na nyumba kama inavyotokea katika msitu wa Hifadhi ya kazi Mzimbwi Wilaya ya Kisarawe, Ipagala, Nzega na kadhalika.

Maoni ya kambi ya upinzani kuhusu hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kuhusu kupanua Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, kambi ya upinzani haina sababu yeyote ile ya kuzuia kuridhia kwa Azimio hili la kupanuliwa kwa Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro na tunaipongeza kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, tuna jambo moja katika suala hili kuhusu kusitishwa kwa shughuli za kilimo kwenye maeneo hayo yaliyotengwa kama Hifadhi. Nadhani wote tunaelewa hali halisi ya uhaba wa ardhi kwa ndugu zetu wa Mkoa wa Kilimanjaro, sasa kama maeneo machache waliyokuwa nayo kwa ajili ya shughuli zao za kuongezea kipato yanachukuliwa na Serikali. Je, hawa Wananchi watakwenda wapi na watafanya nini?

Mheshimiwa Spika, kambi ya upinzani inaihasa Serikali suala la ardhi Mkoani Kilimanjaro ni sawa na mbogo aliyejeruhiwa. Hivyo basi Wananchi waliokuwa wanapata ridhiki zao bila ya kuvunja Sheria watafutiwe utaratibu mwingine na wa kudumu. Kwani miaka yote sheria zilikuwepo na watu walianza kukaa na kufanyakazi zao Serikali ilikuwa kimya, walikwisha kujimilikisha na kwa hilo wanasheria watatusaidia.

Maoni ya kambi ya upinzani kuhusu kuridhia kuanzisha kwa Hifadhi mpya ya Taifa ya Sadani.

Mheshimiwa Spika, katika chimbuko na madhumuni ya hoja kambi ya upinzani inashukuru sana kwa Serikali kuliona tatizo hilo lililopo sasa na uharibifu unaotokea katika baadhi ya maeneo yanayotakiwa kuwa Hifadhi.
Mheshimiwa Spika, kitu ambacho Serikali inajaribu kukifanya ni kuhamisha matatizo katika sehemu moja na kwenda sehemu nyingine, wananchi wa maeneo hayo walikuwa wanaendesha maisha yao na familia zao kwa kufanya shughuli hiyo. Sasa eneo hilo lilikuwa Hifadhi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kambi ya upinzani inamwomba Waziri mwenye dhamana hiyo aieleze Bunge lako Tukufu Wananchi ambao walikuwa wanaendesha maisha yao kwa kutegemea hapo wataenda wapi na watafanyakazi gani? Tuna wasiwasi hiyo inaweza kuwa ni kibali na tiketi ya kuwahamishia familia zao mjini na kuanza kukimbizana na askari wa Mheshimiwa Yusuph Makamba.

Mheshimiwa Spika, kambi ya upinzani inaamini kabisa kuwa kabla ya kutekelezwa mipango hii Serikali ilikuwa na uwezo wa kutafuta shughuli mbadala kwa wale waliokuwa wanaendesha maisha yao kwa kutegemea Hifadhi Taraji.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 3 kinachohusu maeneo yanayounda Hifadhi ya Taifa ya Sadani kuna maeneo ya sehemu ya kijiji cha Mpange na Kwamsisi lenye ukubwa wa Kilomita za mraba 115 tunaamini kuwa ni kijiji, basi watu wanaishi kwa tafsiri sahihi ya kijiji. Sasa tunamwomba Waziri atuondolee utata huu kuhusu makazi ya watu kuhamishwa na kupewa wanyama, na kama kuna faida yoyote ya Wananchi hao kuhamishwa na kupewa eneo jipya la makazi na kilimo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kama nitakuwa sijakosea katika bonde la Ngorongoro kuna watu waishio vilevile na Hifadhi ya Taifa, sasa hapo watu wanaishije bila ya kuwaathiri wanyama? Kambi ya upinzani inashauri kabla ya kuanza kukurupuka kufanya mambo yake, watu wa maeneo husika wanaelewa mazingira yao vizuri kuliko Serikali inavyowafahamu. Hivyo ushauri wao ni muhimu na kuwapa elimu ya kutosha kuhusu nini Serikali inakusudia kukifanya.

Kwa mfano, kama uvuvi wa kamba ulikuwepo hata kabla ya Tanzania haijapata Uhuru na jamii ni ileile inayorithishana mbinu za kuwatunza na kuwavua hao kamba na hao palahala walikuwepo toka zamani sio kama wamekuja jana, ni wa asili Wananchi wanaelewa vizuri hivyo ushirikishwaji wa Wananchi ni muhimu sana.Kifungu cha 4 kinachohusu mawasiliano na wadau inaendesha kuwa kijiji cha Mkwaja kinachotakiwa kutoa eneo la Kilomita za mraba 80, hakikukubaliana na mapendekezo hayo. Hata hivyo ngazi mbalimbali za Serikali pamoja na Baraza la Mawaziri liliamua kwamba eneo hilo lijumuishwe kuwa sehemu ya Hifadhi inayopendekezwa. Huku ni kudharau maoni ya haki ya Wananchi ambao wameishi katika eneo hilo kwa miaka nenda rudi.Kwa hayo niliyoyanukuu toka kwenye Azimio lenyewe, inaonyesha dhahiri elimu na ushirikishwaji haukuwepo na siku zote Serikali inatumia nguvu kuwanyima Wananchi haki zao. Kambi ya upinzani inaamini kabisa sisi Waheshimiwa Wabunge ndio msaada wao wa mwisho. Je, na sisi tutawatupa na kuwadharau kama Serikali yao ilivyofanya? Na mpaka sasa fidia bado haijatolewa kwa vijiji na Wananchi watakaoathirika na mpango huo wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi ili niweze kuchangia kidogo kuhusu suala hili hili la Maazimio haya yote.

Mheshimiwa Spika, kwanza nikubaliane kwamba tunahitahi wanyama waendelee kuwepo na tunahitaji watalii waendelee kuja kwa ajili ya uchumi. Lakini vilevile tusisahau kwamba sisi binadamu tunapashwa kuwepo na tunapaswa kuishi.Tunakubaliana kwamba hizi hifadhi zilikuwepo, kwa mfano Kilimanjaro zilikuwepo na Wananchi wameongezeka maradufu kuliko hata hao wanyama. Nilikuwa nafikiri kwamba ili kwenda sambamba na Maazimio kama haya, tungepashwa kuja na Maazimio vile vile yanayosema kwamba hawa Wananchi wa Tanzania ambao

wameongezeka kwa wingi na wao tuwaendelezeje je kiuchumi? Hasa ukizingatia mambo ya kilimo.

Tunajenga Maazimio ya upande mmoja bila kuangalia upande wa pili, kama hatuwezi kuleta Maazimio hapa Bungeni ya kusema ni namna gani tutawapimia Wananchi tutakaowahamisha mashamba makubwa kwenye maeneo yenye rutuba. Kwani kuna maeneo ambayo hayana rutuba ambayo wanyama wanaishi hayo tungeyaacha na tukapanua. Lakini yale maeneo ambayo tayari yana rutuba na yana limika na tunajua asilimia 80 ya Watanzania hawana kazi nyingine zaidi ya kilimo kipato chao, uchumi wa nchi unahitaji kilimo zaidi. Hiyo asilimia 20 ndio hiyo tunayosema watalii na vitu vinginevyo. Kwa nini hayo Maazimio hayakuja kwa pamoja? Ili tujue a, itakuja hivi na b itakwenda hivi. Kwa sababu Mheshimiwa Spika, kweli tutaridhia Maazimio leo Bungeni hapa lakini kutakuwa na kilio huko, hivi sasa kuna ugomvi kati ya Wananchi kuingilia kwenye sehemu za Hifadhi kwa sababu ya kukosa mahali pa kwenda na Serikali haijafanya lolote. Je, kama wanaongeza hifadhi mara mbili je, wale Wananchi waliokuwepo pale wataenda wapi? Wale Wananchi ambao tayari hata hapo walipo hapatoshi wanaingia kwenye Hifadhi, sasa hivi tumepanga waende wapi? Nakubali Tanzania ni kubwa je, Serikali hii hii imefanya nini kuhakikisha kwamba hawa Wananchi watapelekwa a, b, c, d, na watasaidiwa a, b, c, d, kusudi wao waishi, na wanyama waishi na watalii wawepo, vyote viende sambamba.

Kuna vitu vingi ambavyo vinaweza kuvutia watalii na si lazima kupanua maeneo. Nakubaliana 100% kwamba hilo la kuhifadhi maji na mimi naunga mkono hata mimi nitakuwa tayari kwenda kupanda miti huko sehemu za kwenda kuhifadhi maji. Lakini maeneo hayo kwa mfano Kilimanjaro kulikuwa half mail strip halafu ndio unaingia huko kwenye hifadhi ilikuwepo toka miaka yote na maji tulikuwa tunapata. Sasa leo hii kwenda kuwang’oa hao watu ni hatari Mheshimiwa Spika. Kwa hiyo, mimi ninachosema ni kwamba Maazimio haya nisingekuwa na tatizo nalo kama Wananchi wale wataambiwa sasa wewe ondoka hapa kaa hapa na fidia ni hii na wapate maeneo makubwa mengine yako maeneo makubwa, Tanzania Serikali ifanye hivyo.

Mheshimiwa Spika, nitoe tu mfano wa vivutio ambavyo Serikali haijavitia maanani lakini inakazania vitu vingine ambavyo sioni faida kubwa kwa mfano watalii wakija wanapanda Mlima Kilimanjaro zaidi hawaangalii wanyama walioko ndani ya Mlima Kilimanjaro, ila kuna vifutio vingine, kuna vile, kwa mfano kanisa la Kibosho Mission ambalo limetengenezwa kwa mawe makubwa ambayo ni zaidi ya tani moja ya jiwe moja watalii walikuwa wanakuja zamani huko wakati nikiwa mdogo. Lakini sasa hivi watalii hawaji hapa, kwa sababu hakuna mtu initiative yoyote ya kuonyesha au kutangaza lile kanisa. Maana vitu vya namna hiyo ndio vinafanya watalii wanakuja wanaangalia. Nimekwenda sehemu mbalimbali kwa mfano *pyramid* za Misri watalii wanakwenda huko kwa wingi wanaangalia, na kule mahoteli yote yanajaa wanaangalia zile *pyramids* tu lakini vitu kama hivyo sisi hatujapeleka huko mawazo yetu. Mimi nasema Mheshimiwa Spika, kwanza Wizara haijakuwa na uwezo wa kusimamia haya walionayo. Wizara hii haijakuwa na uwezo, kwa sababu mimi nimetembelea Mikumi, pori la Mikumi, maeneo ambayo yaliyokuwa yanapita maji simba wanakunywa yale maji, ule Mito nimechungulia imekauka, vile vimito vimekauka.

Vile vimito vimekauka lakini ukiangalia kule mito ilikoanzia kuna mito ime - *divert* imeingia kwenye sehemu nyingine ambayo siyo katikati ya pori, ningefikiri labda Wizara ingefuatilia ikaona kwamba hawa simba hawapati maji kwa sababu vimito vimekauka na ku-*divert* yale maji kuyaelekeza yaende kwenye vile vimito ili samba wale waendelee kuishi na kunywa maji na watalii waendelee kuwaona. Lakini sasa hivi ukipita pori la Mikumi maeneo ambayo tulikuwa tunakuta simba ambayo walikuwa wanakuja kwa ajili ya kunywa maji pale kwenye kile kimto, kile kimto kimekauka simba hawaji tena, sasa nilifikiri Wizara ingekuwa inaangalia hayo ya kuweka madhubuti na kudhibiti maji.

Nimekwenda Mtwara, malalamiko niliyopata ni kwamba kuna meli kubwa ilikuja ya nje ikavua Nyangumi pale na vitu vingine na samaki ikakimbia. Haikuweza kuthibitiwa, na hilo ni jambo la wazi na ushahidi upo sasa ndiyo nasema uwezo wa Wizara kwanza kusimamia hivi vilivyopo haijaweza, utakuta mtu amekaa mahali mwananchi amekaa zaidi ya miaka 20 na watoto wamezaliwa hapo sasa leo wataambiwa hapa umeingia kwenye hifadhi. Lakini Wizara ilikuwepo hakuambiwa kwamba hapa ni mahali pabaya usikae, hapa hapatakiwi kwa sababu siyo watu wote wamezaliwa na kujua hiyo sheria, leo hii Wizara inasemaje kuhusu sheria ya mtu akikaa mahali bila kubughudhiwa zaidi ya miaka 10. Unapokuja kumhamisha unamwelezaje na unampeleka wapi. Kwa sababu kila mtu ana haki ndiyo maana narudia kusema kwamba hawa wanyama wana haki ya kuishi na sisi tunapenda wawepo tupate watalii na tunaomba watalii waje kwa wingi kwa ajili ya hao wanyama na hata .

Mheshimiwa Spika, sisi binadamu tuna haki ya kuishi, tunahitaji kuishi na ongezeko letu ni kubwa tumepangiwaje kiuchumi katika kuzalisha ndani ya nchi, katika kuzalisha ndani ya Taifa hili. Wizara imechukua jukumu gani la kujipa nguvu, kujipa uwezo ili vile vitu vidogodogo ambavyo vilikuwepo na vinahitaji ulinzi ili viweze kuangaliwa kwa umakini tuweze kuongeza uchumi kwa kupitia utalii na mambo mengine kama kanisa la Kibosho.

Mheshimiwa Spika, Kwa mfano, sasa hivi utakuta kule Kilimanjaro kihamba cha eka 5 ni makaburi tu yamekaa kule, hakuna mahali pa kuishi, leo hii ukija kuongeza siyo vita hiyo jamani? lakini hatukatai kuongeza ongeza lakini na huyu naye aliyeko hapa naye apate mahali pa kwenda. Kwa hiyo, huku tumepata huku tumepata Serikali itakuwa na utajiri mkubwa sana kwa kufanya hivyo.

Kwa hiyo, mimi niseme tu kwamba, haya mapori tunayoongeza kwa wanyama mimi sikubaliani nayo, bila kujali wananchi nakubaliana na hifadhi za maji kwa sababu kwa kweli tunahitaji kunywa maji na hilo sina upinzani nalo. Lakini tuongeze kwanza mashamba watu walime, tuzalishe 80% nakubali wote tunategemea humo. Sasa tunafanyaje kiuchumi. Kwa hiyo, ninaunga mkono namna ya kutunza hifadhi Kilimanjaro na hifadhi zingine za huko Arusha kama tu endapo tutaweza kuwachukua wale wananchi pamoja na wengine ambao hawako pale ambao wana uhaba wa ardhi na kwani nyie mnasema Tanzania ina ardhi kubwa. Lakini bila maelekezo ya Serikali huwezi kujiingilia tu, huwezi kwenda pale ukarukia pale Ngawaiya amefika pale anasema

mimi nachukua hii ardhi hapa haiwezekani, mpaka Serikali ikubali, mpaka Serikali iseme sasa chukua ikupimie.

Mheshimiwa Spika, mfanotumeambiwa twende Tanga kuna maeneo lakini mpaka sasa hivi hata wale waliokwenda mwaka jana hawajaambiwa sasa hapa ndiyo kwako wameoneshwa tu lima pale lakini hawajapewa hata mipaka, hawajapimiwa, sasa Serikali inapotoa maazimio kama haya kabla ya sisi wenyewe wadau maana sisi binadamu ndiyo wadau. Sisi wenyewe wadau hatujakuwa sawa, maana hata mtu ukiwa nyumbani unahakikisha kwanza nyumbani mnakula mmeshiba halafu ndiyo mnachukua jembe mnakwenda shamba ndiyo mnaangalia na wanyama kama wamekula, lakini kama utaangalia tu wanyama wamekula lakini huangalii watoto kama wamekula hilo mimi ndiyo ninalopingana nalo.

Kwa hiyo, naomba Wizara kwa nguvu zote kwanza iangalie ulinzi wa haya tuliyokuwa nayo, tuangalie tena kwamba hawa wananchi tunawapeleka wapi, na tuangalie vile vile namna ya kutangaza vivutio ambavyo havihitaji kunyanyasa wananchi, kama nilivyotaja kanisa la kKibosho lilikuwa linaleta watalii zamani, sasa hivi watalii hawaji kwa sababu hakuna mtu anayeona kama ni kitu cha maana lakini walikuwa wanakuja watalii bila kutangaziwa. Walikuwa wanakuja watalii bila kutangaziwa, walikuwa Wahindi wanakuja kuliangalia jinsi lilivyo, namna walivyo jenga nyumba kama ghorofa kwa kutumia mawe ya kuchonga ambayo ni makubwa jiwe lingine linakuwa na uzito zaidi ya tani moja watu walikuwa wanakuja kuangalia. Sasa viko vitu kama hivyo, hiyo nimetoa mfano ambavyo Serikali inaweza ikavitangaza na watalii wakaja kwa wingi kuliko hata sasa hivi, kuliko kuanza kupima mashamba makubwa kwa wanyama badala ya kupima mashamba kwa wananchi walime tu waweze kuzalisha.

Mheshimiwa Spika, Kwa hiyo hayo ninayoyasema ya ulinzi wa viumbe vilivyo baharini, watu wanatoka Ulaya kuja kuvua samaki hapa ni aibu na wenyewe wamekiri kabisa na hata Waziri akitaka nitampa ushahidi kwamba walishindwa kukamata ile meli, na ni ngapi zinakuja namna hiyo. Sasa hivi ni vitu vyenye ushahidi kwa hiyo ninaomba Wizara iangalie hivyo nilivyovitaja hapo na ikishaangalia hivyo mimi sina tatizo kabisa na haya yanayotendeka hapa.

Kwanza tutosheke sisi wananchi, tukisha tosheka sisi hatuna ugomvi na Serikali iangalie na hivyo vingine na tusaidiane namna ya kusimamia vyote hivyo.

Nashukuru sana Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, kabla Mheshimiwa Ndugai hujaanza kuchangia namuomba Mheshimwa Simpasa aje anipokee mimi.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Eliachim J. Simpasa) Alikalia Kiti*

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa na mimi niweze kuchangia katika hoja ya Mheshimiwa Waziri ya kuanzishwa kwa hifadhi mpya za Sadani na Kitulo na kupanua hifadhi za Arusha na Kilimanjaro.

Kwanza nianze kwa kumpongeza yeye mwenyewe Mheshimiwa Waziri kwa juhudi kubwa ambazo amekuwa akifanya katika masuala ya hifadhi katika nchi yetu, lakini pia niwapongeze wasaidizi wake Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Watumishi wote wanaofanya kazi katika masuala ya hifadhi za nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshapata bahati ya kutembelea maeneo karibu yote haya isipokuwa eneo la Kitulo, kwa hiyo nitaongelea kitu ambacho ninakifahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze pale alipomalizia muongeaji aliyemaliza kuzungumza kabla yangu, kwamba moja ya mapendekezo aliyoleta hapa Mheshimiwa Waziri ni ya kupanua maeneo ya hifadhi. Nitofautiane naye kama ambavyo Mheshimiwa Waziri ametueleza katika hotuba yake kwa namna ifuatavyo:-

Kinachofanyika kwa Mlima Kilimanjaro ni kubadilisha hadhi ya kisheria ya msitu wa hifadhi ambao unahifadhiwa sasa chini ya sheria ya *Forest Conservation Act* ambayo iko chini ya Mheshimiwa Waziri tayari eneo hilo ni lake bado, anabadilisha kutoka mkono kwa kushoto kwa *Forest* analipeleka mkono wa kulia ambao uko ndani ya eneo lake ya himaya yake la sheria ya *National Parks.*

Kwa hiyo, hachukui hata robo eka ya mtu pale kwa *Arusha National Park* ni hivyo hivyo inabadilishwa *Forest Reserve* kuwa *National Park,* kwa hiyo lile la kusema kwamba wananchi wanaporwa maeneo ningependa kusema kwa uelewa wangu nilivyoelewa hoja hizi zilipokuja hapa, si la kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi ya Kitulo yenyewe ni mpya kabisa lakini nimefuatilia hapa hii itatokana na msitu wa hifadhi ya Livingstone ambao tayari ni msitu wa hifadhi, msitu wa Bonde la Numbe na sehemu ya Shamba la Mifugo lililopo hivi sasa lile la Kitulo. Kwa hiyo, maeneo mengi haya tayari ni ya Serikali kwa namna moja au nyingine.

*Sadani Game Reserve* maeneo yake mengi na yenyewe kinachofanyika Sadani ni kubadilisha kutoka sheria ya *Game Reserve, Wildlife Conservation Act 1974 a*mbayo ndiyo inaendesha ile *Sadani Game Reserve* ya sasa kubadilisha hadhi ile *Game Reserve* sasa kuwa *National Park* ili iendeshwe kwa sheria ya *National Park.*

Ila pamoja na hiyo Sadani kama ilivyo, kuna maeneo mengine ambayo yataongezeka kwa Sadani lakini nayo ni pamoja na msitu uliohifadhiwa na vijiji kama viwili vitatu si vingi. Nilitaka nipite hapo kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhifadhi wa maeneo una umuhimu wa kipekee katika nchi yetu kama tunavyojua maeneo yatu mengi ukataji miti holela umekuwa ni mkubwa sana, uchomaji moto ovyo, kilimo ambacho si endelevu mahali pengi, mifugo ya kuhamahama, kuongezeka kwa makazi ya watu katika maeneo ambayo si mazuri kwa makazi ya watu na mashamba, na tukumbuke sehemu nyingi hizi za hifadhi huwa zinaanzishwa katika maeneo ambayo si mazuri sana kwa kilimo ila ni maeneo ambayo ni mazuri kwa matumizi kama haya ya wanyama pori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hivyo, tunazo faida kadhaa ambazo tunazipata katika zoezi hili ambalo linaendelea, ambalo kabla sijafika mbali nimuombe Mheshimiwa Waziri asiisahau hifadhi ya Manyara katika siku zijazo kwa sababu ni moja ya hifadhi ndogo sana nchi hii, ina kilimeta za mraba zisizozidi 200 na ile ni Biosphere Reserve inatambuliea na *UNESCO* kwa umuhimu wake wa kipekee, kwa hiyo tunaiomba Wizara baada ya muda si mrefu sana watuletee na yenyewe iweze kuongezewa eneo vinginevyo katika miaka 20,30 ijayo hatutaweza kuwa na hifadhi inayoitwa lake Manyara.

Faida nyingi zimetajwa za hifadhi hizi kwa mfano Kitulo, ndiyo catchment area ya mito muhimu kwa ajili ya Ziwa Nyasa, lakini vile vile Kitulo pamoja na ile Milima ya Livingstone ndiyo catchment area ya Bwawa la Mtera, ndiyo catchment area ya Kidatu, Bonde la Rufiji zinategemea sana hifadhi za maeneo haya na bahati nzuri Kipengere Mpanga imekwisha hifadhiwa. Sasa ukihifadhi na Kitulo inakuwa umeshapata eneo ambalo linatosha na zuri sana kwa ajili ya chanzo cha maji kwa faida za nishati na faida nyingine za kilimo na kadhalika.

Vilevile Mlima Kilimanjaro na Hifadhi ya Arusha ambayo nayo eneo linaloongezeka ni hifadhi ya msitu itatusaidia sana katika eneo la Bwawa la Nyumba ya Mungu na pale Hale kwenye masuala ya uzalishaji wa umeme.

Lakini pia zoezi hili linaboresha mtandao wa hifadhi, wenzetu wa Kusini wamekuwa wakilalamika sana kwamba utalii si mzuri sana kwao, kwa hiyo kuanzishwa kwa hifadhi ya Kitulo kwa hadhi ya *National Park* kunaweka maeneo ya Kusini mahali pazuri sana katika masuala haya ya uhifadhi. Kuna maua ya kipekee kule wanaita Orkits na iko mimea mingi ambayo ni adimu sana kule.

Lakini vilevile Sadan *Game Reserve,* ndiyo *Sadani National Park* hii inayopendekezwa sasa ndiyo National Park peke yake itakayokuwa Pwani pale, kwa hiyo mtandao wa utalii wa Zanzibar, Dar es Salaam , Pangani, Maeneo ya kale ya Pangani, maeneo ya Kale ya Bagamoyo na Sadani inatengeneza mduara mmoja mzuri sana kwa ajili ya kuendeleza utalii katika eneo lile la Pwani. *(Makofi)*

Pia kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, wako wanyama wa kipekee kabisa pale kwa mfano hawa *green turtles* sina muda wa kuwaelezea Mheshimiwa Mwenyekiti lakini ni wanyama ambao ni very interesting wanataga mayai hapa Pwani wanaanguliwa wanaingia baharini wanakaa huku miaka 20, 25 halafu yule kiumbe aliyeanguliwa pale anarudi jike, anarudi hadi pale alipozaliwa yeye anataga mayai tena, sasa mahali pengine wakirudi wanakuta ni jiji kama Dar es Salaam na mataa ya umeme wanachanganyikiwa hawezi kujua alipozaliwa ni wapi, kwa hiyo hawezi kutaga mayai kwa hiyo wanaendelea kiusha. *(Makofi)*

Kwa hiyo, maeneo machache kama haya ya Sadani watarudi watataga mle kwa hiyo tutaendelea kuwa na viumbe hawa ambao ni adimu sana kwa sababu kuwasoma historia yao ni ngumu inabidi mtu afanye *research* ya *25 years* toka anapoanguliwa umfuatilie miaka 25 hadi atakapotaga ili upate life circle nzima, kwa hiyo ni wanyama

ambao wanaendelea kuisha na hatuna takwimu za kutosha na information kuwahusu wanyama hao. Kwa hiyo, jambo hili ni zuri, jambo hili ni zito, jambo hili ni muhimu, ningeliwaomba Waheshimiwa Wabunge kwa kweli tuliunge mkono. *(Makofi)*

Mimi nina mapendekezo yafuatayo:- Ninaomba Serikali iangalie namna ya kuboresha zaidi usafiri wa barabara na wa majini katika maeneo ya Sadani ili kama nilivyosema ili mtandao wa Tanga, Zanzibar, Pemba, Dar es Salaam pale wa kiutalii ukae vizuri zaidi.

Tumekuwa tukiongeza idadi ya hifadhi zetu kwa maana ya *National Park na Game Reserve* lakini idadi ya watumishi imekuwa bado ni ndogo, ningeliomba sana Serikali iangalie suala hilo la watumishi watakaoangalia hifadhi zetu hizi. Naomba sana wananchi wanaozunguka hifadhi hizi wafaidike sana na kuwepo kwa hifadhi hizi, kwa sababu bila Support yao siyo rahisi zikaendelea kuwepo.

Mwisho naiomba Wizara iangalie sana isisahau suala la Hifadhi ya Ziwa Manyara kwa sababu na yenyewe ina tatizo moja kubwa sana ambalo kama haitaongezeka basi itatoweka si muda mrefu.

Mheshimwa Mwenyekiti, Baada ya kusema hayo naomba niseme tena kwa mara nyingine kwamba naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia.

Kwanza kabisa nianze kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri mwenyewe na Wizara yake kwa kazi nzuri ambayo wameifanya katika Wizara kwa kipindi hiki kinachoendelea.

Baada ya kusema hayo nianze na kusema kwamba maeneo ya hifadhi nchini ni machache huo ndiyo ukweli, tuna nchi kubwa sana lakini maeneo yetu ya hifadhi ni machache na bahati mbaya maeneo hayohayo ambayo ni machache, wananchi wenye uroho na uchu ndiyo wanayafuata na kutaka kuyaharibu. Matokeo yake kesho na keshokutwa tutakuwa hatuna cha kuhifadhi.

Nasema haya kwa mifano mingi tu, kwa mfano kuna wanyama mbalimbali, mimea, ndege na hata samaki ambavyo ni adimu kupatikana na vingine huwa havipatikani mahali pengine popote duniani. Lakini binadamu mara nyingi atavifuatilia vitu hivyo kuhakikisha kwamba vinaisha na kama vikiisha tutakuwa hatuna kitu chochote ambacho tunaweza kujivunia siku za mbele.

Maeneo yanayoonekana kuwa ya Hifadhi labda yana wanyama au mimea ambayo ni adimu binadamu hufuata maeneo hayo kwa matumizi mabaya ya ardhi kwa maana ya kilimo, kujenga, kufuga na matumizi mengine mbalimbali ambapo huwa anaharibu na mbaya zaidi binadamu huyo huyo anapendelea kwenda maeneo ambayo ni ya hifadhi kwa mfano vyanzo vya maji, maeneo ambayo kuna misitu mizuri na hutunza maji ndiko

anakokwenda kuharibu. Haelewi kwamba kuharibu huko ndiko kunakosababisha kesho na keshokutwa aanze kuhangaika kutafuta maji, anaanza kuhangaika kutafuta asali, anaanza kuhangaika kutafuta mbao, anaanza kuhangaika kutafuta mizizi mbalimbali kwa ajili ya dawa zake za kumtibu, anasahau yote hayo yeye anachokifanya ni kwenda kuharibu tu.

Anakwenda kuua wanyama ovyo na kwa hiyo kusababisha wanyama mbalimbali kuisha na kesho na kesho kutwa tunapohitaji utalii wa kutuongezea fedha nchini kwa ajili ya mapato ya maendeleo yetu tutawakosa watu wa kuja kuwatazama kwa ajili ya uroho wetu wa kula leo.

Huwezi ukapata umeme kwa Tanzania eneo kubwa bila maji, maji haya yanatokana na uhifadhi mbalimbali ambao leo hii unatakiwa kufanyika katika misitu mbalimbali na mbuga mbalimbali zinazoletwa leo hii na Mheshimiwa Waziri na Wizara yake kuhakikisha kwamba tunatunza. Kama hatuwezi kutunza hatuwezi tukapata umeme wa kutosha, tunaambiwa hapa kwamba mabwawa kama vile ya Mtera yameshaanza kukauka na mito mbalimbali kwa sababu hatuna tabia ya utunzaji wa vyanzo na hifadhi mbalimbali zinazotunza maji pia.

Uchomaji wa moto ovyo, Kilimo holela na makazi holela pia yametajwa na Mheshimiwa Waziri, vyote hivyo ni matumizi mabovu ambayo yanasabisha utunzaji wa maliasili zetu kuharibiwa na hivyo kujiharibia maisha yetu ambayo tunalalamika kila siku hatuna mbao, hatuna miti ya kujengea, hatuna umeme wa kutosha na n.k . Ni sisi tunaoharibu lakini kesho tunalalamika.

Kwa hiyo leo hii inapoletwa hoja ya kusema kwamba tutunze vitu hivi baadhi ya watu wanalalamika na hapo ndipo nakuwa sielewi, kwa mfano tunapoelezea eneo la Kitulo hapa niweze kusifia kwa sababu katika eneo mojawapo tunaambiwa kwamba kilimo kisicho endelevu cha viazi kinachosababisha mmomonyoko wa udongo, uvunaji haramu wa mianzi ya asili na miti kwa ajili ya mbao, uvunaji na usafirishaji haramu wa mimea aina ya Orchard ambayo ni adimu na hupatikana katika eneo hilo tu, kwamba vinaharibiwa ndilo chimbuko lililosababisha na kuweka msukumo wa wananchi wenyewe wa Wilaya ya Makete, Rungwe na Mbeya Vijijini chini ya utaratibu wa *Regional Consultative Committee* yaani *RCC* ya Mkoa wa Iringa kufikia uamuzi huo inapenda kuwapongeza hao wote kwanza wananchi wenyewe wa Wilaya hizo zilizotajwa na pamoja na *RCC* kwamba walipoona umuhimu huo wao wenyewe wakaamu tofauti na msemaji mmoja aliyesema kwamba wananchi hao wanalalamika eti kwa viazi vyao, wao ndiyo walianzisha kwa hiyo hawalalamiki na mimi napenda kuwapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Sadani hii ni mbuga mpya inayotegemewa kuanzishwa naunga mkono na wazo jema na zuri sana, msemaji mmoja kasema kwamba anashangaa kuona wananchi wanaoishi pale hajui hatma yao ya kuwepo au kutokuwepo na akasema ni vizuri wake na wanyama wale kwa kuchukulia mfano wa Ngorongoro ambapo Wamasai wanakaa na wanyama mle labda tu hajui matatizo yaliyopo kule Ngorongoro hajui angekuwa anajua wala asingelisema hili.

Lakini kwa upande wa Wamasai wenyeji wanaoishi mle Ngorongoro kama Wamasai wenyewe wale hawana tatizo, kwanza Wamasai asili yao hawali nyama ya porini wanapenda kula nyama ya ng'ombe na kunywa damu ya ngo'mbe lakini wanyama wa porini hawana asili nao.

Mimi sina tatizo na hawa hata kama wangeishi Ngorongoro miaka 1000 mbele hawana mgogoro wenyewe hawa, wenye mgogoro ni wale wahamiaji, wahamiaji wa makabila mengine wanaoingia mle ndiyo wanaotaka kulima kwa mfano na hiyo Sadani hapa watataka kuendelea kulima na kilimo na mnyama ni vitu viwili tofauti. Ni sawasawa na maji na mafuta ukiweka pamoja vinatengana, wataendelea kulima.

Watu hao wageni ambao si Wamasai kwa mfano kwa upande wa Ngorongoro ambao si Wamasai ambao watakaa pale Sadani nadhani hadi leo kuna matukio ya wao kuwinda wanyama kwa sababu asili yao ni kula wanyama wa porini, kwa hiyo wakiendelea bado kukaa pale watakula wanyama tu.

Utatumia mbinu gani wakae ndani ya mbuga wasile wanyama ukiniambia wakae kando naweza nikakuelewa kwa sababu wakikaa kando bado *TANAPA* ina utaratibu mzuri sana wa kuweza kusaidia vijiji na wananchi wanaokaa katika maeneo yanayozunguka mbuga zetu za wanyama hilo naweza nikalielewa.

Lakini la muhimi ambalo linapaswa kueleweka ni kwamba Sadani ni eneo pekee, eneo pekee kwa Tanzania sina uhakika kama ni kwa dunia au kwa Afrika ambalo lina linakuwa na eneo la mbuga la wanyama kando kando mwa bahari ni eneo pekee.

Kwa nini isiwe ni bahati ya kutangaza kwamba ni eneo pekee na dunia ikaelewa kwamba ni eneo pekee na kwa hiyo watalii watakuja kutazama kama eneo pekee. Kwa hiyo, mimi naunga mkono na wananchi wa eneo hili wanalokaa kama wanatusikiliza tunapoongea hapa waone umuhimu si kung'ang'ania ubinafsi kwamba mimi, bali watazame kwamba sisi na siyo mimi, hapo ndipo tutakapokuwa tunajenga nchi yetu kwa usisi na siyo kwa umimi.

Kilimanjaro na Arusha ni maeneo mazuri sana bahati sana ukiruka juu ya ndege ukapita maeneo yale ya Kilimanjaro na hususani wakati wa kiangazi utasikitika, ni maeneo ambayo yanaonekana ni makavu sana machovu, mito imekauka ni hali ya kusikitisha mno. Mlima Kilimanjaro unapoteza barafu yake na wakati fulani huu mlima Meru ulikuwa unaonekana barafu lakini nao ni nadra sana kupata barafu. Mtakumbuka watu tuliokaa kule miaka ya 80,70 mvua ilikuwa takribani ni kipindi cha mwaka mzima leo hii mvua imekwisha potea kwa sababu ya uharibifu wa binadamu kufuata hata kile anachokiona cha maana kwa wakati huo ubinafsi wake unamfanya aharibu, kesho analalamika.

Sasa hatuji Kilimanjaro na Arusha inaelekea wapi kesho na keshokutwa kama siyo jangwa , kwa hiyo ni muhimu kutunza maeneo ya Kilimanjaro na maeneo ya Arusha katika Mlima Meru na ningependa wananchi wa huko wajitahidi sana kupanda miti zaidi

na zaidi katika maeneo yote ambayo wamekwisha yaharibu au yamekwisha haribika ili kusudi maji yaendelee kuwepo na sifa ya Dunia ya Kilimanjaro na Meru inayotukuka pamoja na mbuga zao zilizoko huko ziendelee kuneemeka, maana ukame ule unatishia hata wanyama kupotea katika maeneo yao na kwa hiyo utalii unaweza ukakwama.

Kwa hiyo, nilikuwa nawashauri ndugu zangu wa maeneo hayo waweze kunadi, wanalalamika Bwawa la Mungu, Bwawa la Nyumba ya Mungu linaelekea kukauka, linaelekea kukauka ukipita kwa wakati huu unaona ni jinsi gani ambavyo kwa kweli linaonekana kukauka, ni utunzaji pekee wa hifadhi ndiyo utakoweza kuwasaidia .

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapopanua uhifadhi huu au kuanzisha hifadhi, hifadhi bila kuwa na watumishi bila kuambatana na ajira maridhawa ni bure, watumishi wa Wizara hii nahisi kwamba ni wachache na ndiyo maana uharibifu unaendelea kufanyika katika maeneo mengi. Natolea mfano kwa eneo langu kwa mfano la Jimbo la Nkasi tuna hifadhi ya Msitu wa Luanfi ni mkubwa na una wanyama, una mbao, una mimea, una asali ya kutosha kwa kupitia nyuku na kadhalika, mito mizuri isiyo kauka, lakini ni maeneo ambayo yanavamiwa sana na wananchi kuvuna maliasili hizo kiholela na watu wa Maliasili wanashindwa kuwadhibiti kwa sababu ni wachache na si uchache tu hawana hata vyombo vya usafiri kuingia katika maeneo hayo.

Kwa hiyo, sambamba na uongezaji, upanuaji au uanzishaji wa maeneo mengine ninaishawishi na kuishauri Wizara ijitahidi sana kutoa ajira na Serikali ione umuhimu huo kusaidia Wizara na pia magari au vyombo vingine vya usafiri hata ikiwezekana baiskeli na vifaa vya usalama vya kulinda katika maeneo hayo. Hapo tukifika katika hali hiyo tutakuwa tumeweza kusaidia sana suala zima la kuhifadhi maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo jingine katika uendelezaji wa utalii ukanda wa Kusini ambao Mheshimiwa Waziri ameutaja kwamba Serikali ijitahidi kuweka vivutio vya utalii na nikitolea mfano kama vile Mbuga ya Katavi na maeneo mengine ya kuelekea Kigoma huko ni maeneo ambayo hayajaendelezwa hata hayo maeneo ya Iringa na Mbeya na Ruvuma bado hayajaendelezwa na watalii wengi wanakimbilia Kaskazini kwa sababu Serikali imesahau eneo la Kusini, imesahau eneo la Kusini sina uhakika *management* iliyopo katika mambo ya utalii kama ni watu wa Kaskazini tu kwa hiyo wanapendelea kwao tu au vipi.

Lakini jambo jingine hapo ni suala zima la uboreshaji wa miundo mbinu kama vile barabara, kama hakuna barabara ya lami kwenda Rukwa -Katavi mpaka kwenda Kigoma huko na maeneo ya Kusini hakuna barabara za lami unategemeaje watalii wanaopenda raha waende maeneo hayo wakapate maumivu na pengine magonjwa kwa sababu ya safari mbaya ya mabonde kwa hiyo hili ni tatizo ambalo ni la Serikali siyo la Wizara ni Serikali kwa sababu maeneo ya Kusini na kupendelea maeneo ya Kaskazini ndiyo maana siku zote watu wa Kusini tunalia, tunalia na tunalia na sijui tutalia mpaka lini, Serikali haitaki kusikia labda ni muundo wa utumishi ulioko ndiyo unaotuumiza.

Kuhusu *beacons,* maeneo mengi ya mbuga za wanyama yana matatizo ya *beacons* na *beacons* zinazowekwa nyingine ni hafifu yaani ni ndogo hazina nguvu kiasi kwamba wananchi wenye uroho wa kuingilia hifadhi mbali mbali wanafika na

kuzibomoa na matokeo yake wanakwenda kuharibu kwenye hifadhi hizo. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kwenye hifadhi mbalimbali hizi *beacons* muweke zile madhubuti na zenye nguvu, maana maeneo mengine yanauzwa licha tu ya kuvamiwa, yanauzwa kwa sababu *beacons* hazieleweki na watumishi hawafuatilii mara kwa mara kuona kama zile *beacons* zipo ama hazipo .

Mheshimiwa Waziri ametaja Milima ya Livingstone kuwa yaelekea kuwa ya tatu kwa urefu nimefurahi kusikia hili lakini pia tuliwahi kupewa mawazo kwamba au taarifa kwamba Oldonyo Lengai ambayo iko karibu na maeneo ya *Ngorongoro Crater Conservation Area* kwamba ndiyo Mlima Mkubwa wa tatu sasa sijui ukweli uko wapi. Na kwa ombi rasmi kwa Wizara nilikuwa naomba mfikirie hii Oldonyo Lengai ambayo iko mpakani kabisa na *Ngorongoro Crater* iweze kupelekwa *Ngorongoro Crater* kama hifadhi kulikoni kubakia kama ilivyo kwa sababu bado ule Mlima bado unatoa *Volcano.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la kuhimiza utalii bado Wizara haijajizatiti katika suala la utalii. Tanzania tuna tunu ya vitu mbalimbali katika suala la utalii, na kama Wizarani pangekuwa na wataalam waliobeba na wanaopenda na wanaojali suala la utalii wala tusingeweza kubabaisha katika masuala ya maduhuli ya Serikali tuna kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtalii mmoja mwezi Oktoba, mwaka huu tulipokutana naye, akasema kwamba Tanzania mnachezea sana masuala ya utalii wala msingekuwa na sekta nyingine yoyote kuhangaiki kutafuta maduhuli ya Serikali isipokuwa utalii. Akasema kwamba hata viwango tunavyowatoza sijui *dollar 15*, sijui *dollar 25,* mara gari ndogo *dollar 30* au *dollar 120* akasema *is nothing.* Sisi tukashangaa mbona tunaona ni viwango vikubwa, akasema hakuna, akasema kwa mfano ukienda Ulaya maji ya chupa ndogo ni *dollar 5,* kitu kidogo tu *dollar 10.* Sasa nyie mnapokuja kunitoza nimetoka na fedha yangu huko, na eneo lingine lolote la duniani hata katika Afrika hapa hapa wanatoza fedha nyingi, akasema nyie mnatoza fedha kidogo sana. Akasema hivi nyie mko *serious* na mambo ya utalii ukweli! Akasema aah bwana unajua mtu ambaye haoni ukishaanza kumwambia ona mwisho anaweza kukupofua hata wewe mwenyewe basi muendelee na upofu huo. Maneno haya yalinisikitisha sana. Eti tuendelee na upofu katika utalii.

Wizara kaeni na Bodi zinazohusika za Mbuga zetu na maeneo mengine ya uhifadhi na utalii kaeni mtazame viwango hivyo upya ni vidogo sana. Tena *dollar 15* upande wa Kusini kama vile Mikumi, Udzungwa na kwingineko. Kwa sababu huko ni chinichini tu. Dollar 25 kwa kila mtalii Kaskazini kama vile Manyara, Arusha na Tarangire na kadhalika. *Dollar 30* Serengeti, Kilimanjaro na gari *dollar 30.* Mtanzania sina tatizo na shilingi 1,500/= hiyo sawa. Lakini huyu wa Afrika Mashariki analipa sawasawa na mtalii mwingine wa kutoka nje nilikuwa naomba hili Wizara inayohusika na pengine Bodi zinazohusika katika Mbuga hizo na Hifadhi mbalimbali walitazame na kuliboresha kuhakikisha kwamba hawa wanaotoka Kenya na Uganda waweze kulipa *rate* moja na ile labda ya Watanzania ili kusudi tuweze kupata mapato ya kutosha.

Lakini pia katika Muungano wetu huu wa Afrika Mashariki na Kati ambao tumeuanzisha utaweza kuweza kutusaidia na kutuweka wamoja zaidi.

Mwisho, Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishukuru Wizara nzima kwa kazi nzuri ambayo wameanza kujitahidi kidogo. Naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kuunga mkono Maazimio yote matatu. Lakini baada ya kufanya hivyo ningependa nimpongeze Mheshimiwa Waziri na wataalam wake kwa kuleta mapendekezo haya matatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, adui mkubwa wa mazingira ya binadamu ni binadamu mwenyewe na kwamba mahali ambapo viongozi hawana maono watu wanaangamia: *"Where leaders have no vision the people perish."* Nashukuru Wizara ya Maliasili na Utalii inaona mbali na imeleta mapendekezo haya wakati huu muafaka. Mawazo kwamba watu watakwenda wapi yamesemwa vizuri na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge. Lakini ni vizuri tujue kwamba Mungu haendelei tena kuumba ardhi, watu wanaendelea kuongezeka, lakini Mungu haongezi tena ardhi. Kwa hiyo, njia ni sisi kukaa na kuangalia namna ya kutumia rasilimali hii vizuri. Kama tutaendelea na tabia hii ya kujenga majengo kila mahali hata maeneo ya ardhi mwisho tutakuja kukuta hakuna sehemu za kulima mashamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchambuzi wangu katika Tanzania nadhani Mkoa wa Kilimanjaro sasa ni kama wote ni Mji wenye nyumba zilizojengwa katika maeneo ya *Low Density.* Sasa swali la kujiuliza hapa ni kwamba hao wengine watajenga wapi? Swali hili halijibiwi kwa kuacha kuchukua eneo lile linalotajwa katika kupanua eneo la Kilimanjaro. Suala la msingi hapa ni kwamba ni namna gani tunaweza kutumia rasilimali hizi kwa faida kubwa zaidi. Je, tuache eneo hili kujenga nyumba utajenga nyumba ngapi? Mimi natoka Mkoa wa Iringa ambako lile eneo la Kitulo linasemwa, lakini karibu robo tatu ya mto Rufij unatoka eneo hili tunalolisema hapa Mkoa wa Iringa na Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Tanzania mjiulize Waheshimiwa Wabunge ni Mkoa gani ambako watu wanapata umeme kwa wingi zaidi katika Tanzania mnajua na maji yanatoka wapi? Tusipoangalia tunaweza tuka-adopt a Machiavellian attitude ambayo inasema: *"The end justifies the means",* kwamba hujali unapataje mradi unapata matokeo lakini unatumia njia gani hujali. Tukianza na *attitude* ya kusema watu watakwenda wapi. Wamasai kule wame *sacrifice Ngorongoro* na katika maeneo mengine kwa ajili ya Tanzania. Sasa mnasema wenzetu wa Kitulo wa-*sacrifice* eneo hilo wasiharibu mazingira kusudi maji tuendelee kuyapata sehemu ya Tanzania, lakini ukisema watalima wapi viazi, walima viazi mwisho watakaozaliwa kesho watalima wapi.

Kwa hiyo, nasema ni vizuri katika kuchambua mambo haya tusiwe *Machiavellian* kwa kusema kwamba mradi mambo nafaidika mimi basi unazuia mambo kwa ajili ya mambo mengine, lazima utoe jibu, Tanzania yote ni ya sisi wote. Lakini tukiendelea na mtazamo wa hali ya Kilosa wakulima wanagombana na wafugaji

na hajatupata *solution, solution* ni ipi? Tuseme muendelee ku-*roam around* katika Tanzania *everywhere* mnakwenda mnaua ardhi mnakwenda tu kwa sababu ya matatizo uji-*address* kwenye tatizo.

Moja ya tatizo kubwa katika Tanzania nimesema mara nyingi kwamba hizi nyumba tunazoendelea kujenga kila mahali katika nchi nzima na kutambaa katika nchi nzima mwisho itabidi tuweke X ili tupate pa kulima mashamba. Tupunguze baadhi ya majumba kusudi tuwe na mashamba vinginevyo tutakuja kujiua wenyewe tu. Kwa hiyo, katika hilo mimi nadhani Mheshimiwa Waziri hapa anatoa jibu. Hivi Kilimanjaro ingefaa kwa matumizi yapi kwa kulima kwenye Mlima Kilimanjaro au kwa utalii. Eneo lile la Wamasai je, wangelima mtama na kuacha watalii njia ipi ingewapa fedha zaidi kwa utalii au kwa njia hii ya kulima ardhi na kupanda mtama. Haya ndiyo baadhi ya maswali wanauchumi wajiulize katika *opportunity cost which is the best way* ya kutumia *resources* tulizonazo, eka hizi tuzitumie kupanda miti au tulime mtama au tufuge ng'ombe. Nadhani haya maswali yamejibiwa vizuri na Mheshimiwa Mbunge wa Nkasi na baada ya hapo niende Kitulo.

**MWENYEKITI:** Ili kuweka *record* sawa ni Mbunge wa Nkasi.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Kitulo kwa uamuzi huu tuna-*sacrifice* eka zaidi 33,000 zenye mimea ambayo haipatikani mahali pengine katika Tanzania, na kwa kufanya hivyo tunatunza kitu kinachoitwa *biodiversity* yaani mimea mbalimbali ya asili ambayo inawezekana kesho tukagundua dawa hata za UKIMWI kutokana na mimea hii. Kwa sababu asilimia 85 ya dawa tunazotumia hospitalini zinatokana na miti na asilimia 15 zinatokana na miamba. Sasa kwa kupanda hii miti ya kigeni kama misindano, mikaratusi tunaua miti ya asili ambayo ina utalii huu wa sifa ninazozisema hapa. Kwa hiyo, kwa uamuzi huu maana yake tunatunza utajiri wa mimea ndani ya nchi, na hivyo kuongeza utajiri ambayo unawezakana katika utafiti tukagundua dawa nyingine ambazo zitatufaa Watanzania. Kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuona mbali katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu nilichonacho hapa kuhusu *Plateau* wanasema kwamba Kitulo ni Bustani ya Mungu, *Gods Garden* wanasema: *"The Serengeti of natural flowers",* aina zaidi ya 350 ya mimea na maua ambayo haipatikani mahali pengine popote pale. Sasa ukiruhusu viazi wataua miti yote hii ambayo haiko mahali pengine duniani, viazi viko mahali pengine popote. Kwa hiyo, ni kwa uamuzi huu una-*preserve* hii mali ambayo iko hapa. La pili, katika maandishi haya kwa mfano, mtaalam mmoja ameandika anasema hivi: *"These will be first park in Tropical Africa to be gazetted floristic significance and such as a innovative and highly recommendable step by the Government of Tanzania."* Uamuzi huu tunaoamua sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi tunasema tena tubadilishe. Anachopendekeza hapa ni kwamba*: "The challenge will be to establish a management system which will take into consideration community requirements and needs"* wanazunguka pale kwa mfano, barabara na mahitaji mengine. Kuna njia nyingine siyo lazima ulime kwa jembe unaweza kupata raslimali kwa njia hizi. Kama kuna watu wajinga wanaangalia

wanyama tu na kutoa fedha. Wewe utasema Wamasai wakaangalia misitu ya Ngorongoro watatoa fedha kweli watakushangaa! Wamasai hawajafikia mahali hapo pa kuangalia wanyama kama simba na kulipa fedha. Kuna watu huko wamekwishachoka wanapata faraja kwa kuangalia simba, kwa nini usichote fedha hizo kwa urahisi na ukatumia ardhi hii vizuri zaidi kuliko kupanda mtama ambayo utapata debe moja tu.

Kwa hiyo kwa uamuzi huu Mheshimiwa Waziri mimi nampongeza na ningependa aharakishe na ikiwezekana hata yale maeneo mengine ambayo tulichelewa kama Hayati Mwalimu Julius Nyerere angeamua wakati ule alipoamua ku-*preserve* maeneo mengi ambayo sasa yako chini ya Hifadhi leo tungechelewa maana tungepata tungesema na wengine je? Katika msahafu wa Kikristo inasemekana kuna wakati fulani Yesu alikuwa anapakwa mafuta na Maria, sasa dada yake kwa wivu akasema, haya mafuta unayopakwa Yesu yauzwe yangetumika kwa maskini wengi zaidi kuliko huyu anavyokupaka wewe Yesu. Yesu alisema, aah umaskini mnao kila siku. Huyu anafanya kitendo ambacho kweli na wengine wote hawawezi kufaidika. Kwa hiyo, kwa ushauri huu nasema hivi sasa joto la Dar es Salaam na *humidity* ya Dar es Salaam watu wengi wanakimbia pale. Wajapan baada ya kwenda Kitulo ukapanda futi 8,000 juu ya usawa wa bahari unakwenda kukuta juu kumenyooka ni *flat.* Halafu joto kutoka *minus 6 Centigrade* mpaka *29 Centigrade* ni *temperate throughout the year,* ukienda pale unashangaa kama uko katika nchi hii. Sasa mahali kama pale kuna watu wanakimbia Dar es Salaam kwa sababu ya joto kwa wakati kama huu wanahamia kule kwenda kucheza na kufurahia hali ya hewa, ndiyo maana tunasema kwamba tu-*reserve* kwa njia hii. Kwa taarifa yenu eneo lile zamani liliachwa kwa sababu ya baridi na watu waliahamia sehemu za pembeni. Ninadhani matumizi haya sasa yatafanya eneo litumike zaidi kuliko njia nyingine zozote zile. Sasa tuamue tunataka fedha kwa ajili ya viazi au kwa ajili ya utalii hili ndiyo suala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la tatu, nilikuwa napendekeza kwamba labda pamoja na hili Mheshimiwa Waziri atazame uwezekano wa kutunza baadhi ya maeneo yenye mimea asili siyo lazima iwe miti. Kwa mfano, hizi *shot savannah Grasslands* ambazo sasa hivi zinatoweka kutokana na kilimo hiki cha kulima kila mahali. Chini ya Utaratibu wa *Equal Tourism* watu wanaweza kuangalia mbuga na nyasi nzuri ikavutia, sasa hizo zote zinatoweka tunabaki tu na mimea na mashamba jambo ambalo vilevile linaua utalii. Utalii unabadilika sasa siyo lazima wawe simba tu. Wanaweza kuangalia mimea, hali ya uzuri wa nchi nao ukaleta fedha.

Mwisho, ningependa kusema kwamba sisi Watanzania tuna bahati Kilimanjaro ndiyo Mlima pekee tulionao katika Afrika na ulio mrefu kuliko Milima yote *the roof of Africa,* lakini unatoweka . Sadani hivyo hivyo ndiyo mbuga pekee iliyo karibu na bahari. Tunachanganya mambo ya bahari na mambo ya nchi kavu na ndiyo *the nearest to Dar es Salaam* kwa Balozi wengi tu. Sasa badala ya kukumbatia wazo mzuri hili na kulikuza na kuwaelimisha wananchi walipokea tuweze kufaidika tunakuwa nyuma zaidi. Kwa dunia ya baadaye kupata eka moja itakuwa ni miujiza, kama unaweza kutunza eka 200 leo kwa ajili ya utalii hutakuwa nalo kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ufalme wa matumaini hakuna kipupwe. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kuunga mkono kwa asilimia 100 Maazimio haya na kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa tabia yake ya kuona mbele yaani kuwa *version* na ku-*intervene* pale ambapo anaona kabisa kwamba hapa siyo maslahi ya Taifa pengine ni maslahi ya watu wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri juzi alizuia magogo yasikatwe ovyo iliwachukiza wachache, lakini imewanufaisha Watanzania wengi. Leo anatangaza uanzishwaji wa Hifadhi mpya na kuongeza maeneo ya Hifadhi zilizokuwepo. Ni jambo la kujivunia. Napenda kusema wale wenzetu ambao hawaoni manufaa ya kuona mbali, nafikiri hata tukiwapa nchi hii tutafika pabaya na hizi ni dalili za kuonyesha kwamba hawako tayari. Nafikiri mmenielewa. Sasa kwa nia hiyo hiyo mimi nianze na ombi. Nimekwishaunga mkono Maazimio yote na kwa kweli ninakubaliana na yote yaliyoelezwa na Mheshimiwa Waziri. Pengine nianze pale ambapo kaka yangu Jackson Makwetta amemalizia kwa kusema tusisitize kutamka maeneo tunayoyaona yana maslahi makubwa kwa Taifa kuliko maslahi ya watu wachache. Nalizungumza hili kwa sababu miaka miwili iliyopita nilileta ombi kupitia swali hapa Bungeni la kuomba misitu iliyoko katika Hifadhi ya Milima ya Usambara hasa maeneo yaliyoko katika Wilaya ya Lushoto yachukuliwe na *TANAPA* na yaongozwe kwa Sheria ya Uhifadhi ya Taifa. Kwa bahati mbaya swali hili bado halijapata ufumbuzi. Mimi nimwombe Mheshimiwa Waziri aelewe historia ya Milima ya Usambara. Milima ya Usaramba ndiyo Milima ya jirani kabisa na ufukwe na bahari katika ufukwe wote wa Tanzania. Milima hii ukianza Amani ni karibu sana na ufukwe wa nchi yetu kutoka Bahari ya Hindi, na najua kwamba iko katika mpango wa Hifadhi lakini kijumla ya Milima ya Udzungwa pamoja na Usambara.

Lakini yapo maeneo kutokana na wingi wa watu katika maeneo haya hasa katika Milima ya Usambara na Lushoto *in particular* watu ni wengi kiasi kwamba Hifadhi za misitu ambayo ndiyo chimbuko la maji ya Mto Pangani kwa kweli sasa misitu ile imekwisha. Wizi wa mbao, uvunaji mbaya wa mbao pamoja na kwamba Serikali imepiga marufuku kwa kweli hali ni mbaya sana. Hifadhi ya miti ile asili sasa hivi imetoweka kwa kasi kubwa sana. Sasa mimi namwomba Mheshimiwa Waziri maeneo ya misitu ya Magamba, Kadelekampala, Mazubai, misitu ya Barangai, Banga, Maweni, Kwekuluge, Herukulu, misitu hii inalindwa na Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii, lakini kwa bahati mbaya sana. Mimi napenda kutamka na bahati mbaya mimi ni mwazi kwa kweli watumishi walioko katika eneo hili ndiyo chanzo cha matatizo. Hawalindi na hawafanyi kazi kama Mheshimiwa Waziri anavyoagiza na sheria inavyotaka. *(Makofi)*

Sasa ili maeneo haya yapate Uhifadhi na kama ilivyotamkwa kwa kuwa ni Sera ya Taifa kutambua na kuanzisha mfululizo wa mtandao wa maeneo ya Hifadhi ya Maliasili wakilishi narudi wakilishi yaliyohifadhiwa kisheria na kwa hadhi ya juu kabisa; na kwa kuwa Hifadhi za Taifa ni mtandao wa maeneo yaliyohifadhiwa kwa hadhi ya juu

kabisa kisheria kwa ajili ya uhifadhi wa maliasili kwa ajili ya manufaa ya jamii ya sasa na ya urithi wa vizazi vijavyo. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri hasa katika hili la kwanza kwamba maliasili wakilishi. Maeneo niliyoyataja yaingizwe chini ya *TANAPA* ili yaweze kulindwa, na kwa kweli tuwape vizazi vijavyo nafasi ya kuona sura ya Usambara ilivyokuwa vinginevyo misitu hii itaathirika sana na faida ambazo tunazipata leo na ambazo zimeanza kuonyesha madhara hasa kwa kupungua maji kwa Bwawa la Nyumba ya Mungu, hili nina uhakika litatuletea janga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba Wajerumani walipokuja katika nchi hii na Waingereza walipokuja katika nchi hii walitambua maeneo ya Usambara kwa sababu ndiyo yaliyo karibu kabisa na Pwani ambako ndiko walikofika kama maeneo ya Hifadhi na yakatunzwa sana, na ndiyo maana mandhari hata ujenzi wa nyumba katika maeneo hayo yanazingatia historia ya Wajerumani na Waingereza. Kwa hiyo, naomba ili kuhifadhi hii Mheshimiwa Waziri atamke na achukue kila njia kuwezesha maeneo haya yatangazwe kama maeneo ya Hifadhi ambayo yanalindwa kwa hadhi ya juu ya kisheria chini ya Sheria ya Uhifadhi wa Taifa. Baada ya kuchangia na kutoa ombi hilo na kuomba Serikali ichukue hatua. Sasa nije katika ushauri wa ujumla katika Maazimio haya ambayo Mheshimiwa Waziri ameyawasilisha vizuri. Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamechangia vizuri sana katika kuhimiza Serikali kutambua maeneo muhimu ambayo kwa kweli ni kwa manufaa ya nchi yetu. Bahati nzuri Wizara imechukua taratibu nzuri za kuwashirikisha wananchi wanaoishi katika maeneo hayo. Pengine mimi nisisitize tu kwamba wananchi wanaoishi katika maeneo ambayo yanapakana na misitu, wanaopakana na maeneo ya Hifadhi ya Wanyama wa Porini kwa kweli waendelea kupata faida kutokana na maeneo hayo. Kule kwetu Lushoto wananchi wameanza kushirikishwa na wamekwishaanza kuona faida ya hilo. Kwa hiyo, tunaomba na tunasisitiza Serikali iendelee kusisitiza hivyo na wananchi waendelee kupata faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambayo limeshauriwa na ninalirudia. Saadani ni Hifadhi mpya na mimi napenda kusema kwa sisi wananchi wa Mkoa wa Tanga tunaishukuru sana Serikali kwa uamuzi huu. Kuunda Hifadhi ya Saadani itaboresha sana maendeleo ya Mkoa wa Tanga na maeneo ambayo yako jirani na Pwani. Tunaomba sana barabara ya Tanga - Pangani kwenda mpaka Bagamoyo na Dar es Salaam iimarishwe kwa utaratibu huu sasa baada ya mbuga hii kuonekana kwamba inakubalika kisheria. Nina hakika sasa tunaweza kuwapata wawekezaji wa kutengeneza barabara hii kwa Mpango wa *Build Operate and Transfer* mimi nina uhakika hawa wanaweza kupatikana baada ya Serikali kuitangaza hii kama Hifadhi. Lakini siyo hilo tu, kwa sasa hivi kutokana na azma hii hii hata kabla ya Serikali kutangaza kwamba eneo hili liwe ni Hifadhi. Hivi sasa imeanza biashara nzuri sana ya utalii wa haraka wa ndege kati ya Dar es Salaam - Zanzibar na Saadani. Kwa hiyo, kuna umuhimu wa kuimarisha kiwanja kidogo cha ndege cha Saadani ili watalii waweze kwenda kwa siku na kurudi Dar es Salaam au Zanzibar kwenda kuangalia wanyama na kurudi. Kwa hiyo, biashara hiyo imeanza kuwapatia Watanzania walioko Zanzibar, walioko Dar es Salaam mapato. Kwa sababu watalii wanapokwenda wanakodisha ndege, wanawapata *tour guards,* wanasaidia sana maeneo haya. Tunaomba sana Serikali iliangalie hili kwa kuimarisha

kiwanja kidogo cha ndege kilichoko Sadani ili watalii waweze kwenda kwa haraka na kurudi katika maeneo wanayotaka au kupitiliza kwenda kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningeomba sana Serikali iliangalie kwa kweli ni ujumla kwa hizi Hifadhi zetu. Hifadhi ni kitu muhimu sana na wale wanaoishi kufanya kazi katika Hifadhi wanaishi katika mazingira magumu sana, wanaishi mbali na maeneo ya binadamu wengine, wanaishi karibu sana na wanyama wakali. Kwa bahati nzuri sisi tuliwahi kutembelea maeneo hayo. Tunaomba tuwaenzi wafanyakazi wanaofanya katika maeneo ya hifadhi. Kweli *TANAPA* wanafanya kazi nzuri kuwaenzi na wanafanya kazi nzuri kuwapa mishahara mizuri na kuwapa huduma muhimu kama afya, kuangalia elimu, lakini tunaomba wale ambao wako katika hifadhi hasa chini ya Serikali yenyewe ambao bado hawajatawaliwa na sheria ya hifadhi za Taifa, tunaomba Serikali iendelee nao kuboreshea maslahi yao na kuwapa ulinzi na kuwapa haki za ziada ili waweze kuishi kwa amani na kuishi kwa furaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, mimi napenda kurudia tena kuunga mkono Maazimio na kumtakia kheri Mheshimiwa Waziri kwa mawazo yake ya kuona mbali. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nashukuru kunipa nafasi nizungumzie maeneo haya ya Hifadhi ya Misitu yaliyoongezwa. Kwanza, naunga mkono Hifadhi zote zilizoongezwa. Lakini nizungumzie Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro kwa sababu uko katika eneo langu na kwa hiyo naifahamu sana. Ningependa kusema kwamba naunga mkono kabisa mia kwa mia kuunganishwa misitu yote miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kurudia alivyosema Mheshimiwa Job Ndugai kwamba Msitu wa Kilimanjaro hakuna eneo lililoongezwa au lililomegwa kwa sababu zote zilikuwa Hifadhi za Serikali. Serikali ndiyo imeunganisha misitu yote miwili ambayo ilikuwa chini ya Serikali. Siyo kweli kama alivyosema mwenzangu kwamba Hifadhi za Msitu wa Kilimanjaro eti zinahifadhiwa kwa ajili ya wanyama siyo kweli. Kuna wanyama kweli, lakini mimi nadhani ni tofauti na maeneo mengine kama yalivyo maeneo ya *open area* zile *blocks* zenye wanyama wanaowindwa kule na watalii. Kwa hiyo, ni kweli Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro ni urithi wa dunia, lakini sana sana ni urithi wa Tanzania. Sisi wenyewe ndiyo tunafaidi zaidi na inabidi sisi wenyewe tuwe wahifadhi wakubwa. Kwa hiyo, naungana kabisa na suala hili la kuhifadhi msitu wa Kilimanjaro. Lakini ningependa kusema machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msitu huu unafaidisha Wilaya zote zinazozunguka Mlima wa Kilimanjaro, ndiyo maana nasema na mimi nimo kwa sababu Jimbo langu linafika katika msitu huo wa Kilimanjaro. Ningependa tu kuiambia Wizara ili tuweze tukahifadhi msitu huu vizuri ni afadhali sasa kuteremsha maji yote yaliyoko misituni. Wananchi wapate maji wasiwe na kigezo tena cha kufuata maji msituni, kwa sababu huwezi ukatuzuia tusifuate maji msituni kama hatuna maji huko vijijini. Kwa hiyo yateremsheni maji hayo yaliyoko kwenye vyanzo vya maji tupate huku chini tuweze na

sisi tukawa wahifadhi. Kwanza, Jimbo langu ni wahifadhi wakubwa wa Msitu wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi tukajidai kwamba tuna Mlima Kilimanjaro. Mlima Kilimanjaro hatakuwa nzuri kama hatuhifadhi msitu ule. Huo msitu ndiyo sifa ya Mlima Kilimanjaro. Kwa hiyo, ningependa kusema kwamba kwanza Wizara kwa upande mwingine mimi bado nasema Wizara hawako macho sana kwa ulinzi wa msitu huu. Kwa sababu inavamiwa kila wakati Mheshimiwa Waziri anafahamu kesi nyingi zilizoko Mahakamani. Kuna kesi nyingine za mwaka 2002 mpaka sasa bado zinapigwa tarehe sijui Serikali inafanya nini hapo? Watu wamevamia misitu mwaka 2002 bado tarehe inapigwa sijui mpaka lini? Kwa hiyo, ningependa kuiambia Serikali kwamba wawe macho sana katika Mlima huu wa Kilimanjaro.

Jambo lingine ambalo ningependa kusema ni *Beacons* katika mipaka ya misitu nilitaka wananchi waelimishwe sana wajue mipaka ya misitu. *Beacons* iko wapi kwa sababu kutoelewa wakati mwingine wananchi wanaweza tu wakavamia wakasema kwamba sisi hatujui mipaka ya misitu. Hiyo mipaka waelimishwe wananchi wanaozunguka katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti lingine ningependa kuipongeza sana hifadhi ya msitu wa Kilimanjaro *KINAPA* ambayo wao wanalinda msitu ule. Napenda kuwapongeza kwa misaada mikubwa sana wanayosaidia vijiji vinavyozunguka msitu huo. *(Makofi)*

Kwa kweli kwa hilo ndiyo maana sisi tunalinda msitu huo wao ndiyo wanatusababisha tulinde msitu huo. Kwa sababu msaada tunaopata ni msaada mkubwa sana hatuwezi sisi tukasema kwamba tutapinga au tatafanya nini. Tunaelewana nao na tunaelewana kwa sababu wanatusaidia kwa hiyo ningeomba ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge kama hifadhi kama hizi zinaanzishwa katika maeneo yenu msiyakatae na mimi naomba kama alivyoomba mwenzangu Mheshimiwa Henry D. Shekiffu kwamba nina msitu mkubwa sana ulioko mlima longido naomba na huo mlima uwekwe chini ya hifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nasikia Wabunge wakitaja tu kwamba wanyama wako Ngorongoro kwa sababu wamasai hawali wanyama pori na sio hao tu walioko Ngorongoro hata katika maeneo mengine wanyama wako sana sana Kiteto wako Simanjiro wako na Monduli kwa sababu hatuwali wanyama pori. Lakini sasa na sisi tumekuwa wajinga kutowala hao wanyama pori na sasa tunaanza. *(Makofi/Kicheko)*

Tunaanza kwa sababu wawindaji wote katika maeneo mengine wanakuja kuwinda wale wanyama ambao tunahifadhi hata baadaye tukitaka na sisi kula hatuta wapata watakua wameisha ni afadhali na sisi tuanze sasa. Nasema hivyo kwa uchungu sana kuna twiga kumi na mbili waliouwawa Monduli yaani wameuwawa twiga kumi na mbili kwa wakati mmoja kwa siku moja lakini nashangaa najaribu kusikiliza kila siku kwamba hawa watu wamefanywa nini sijawahi kusikia. Kwanza hakuna leseni ya kuwinda twiga sijui kama imetoka mwezi uliyopita au wakati huo hao twiga walipowindwa. Sasa

Serikali inakaa kimya ndiyo maana mimi nina wasiwasi hawa wanyama wataisha kwa muda miaka mitano sijui kama kutakuwepo na wanyama.

Kwa hiyo, naomba Serikali ichukue hatua ya kutunza hifadhi ya taifa wanyama ni rasilimali ya taifa lakini naona tumeachia waiunde kiholela. Naomba Mheshimiwa Waziri ni kwamba hujapata nafasi ya kuwafuatilia hawa twiga kwa sababu ukifuatilia kama ulivyofuatili magogo lazima utakomesha na hao. Kwa hiyo, na mimi nachukulia kabisa hao twiga waliyowindwa kama ule Uvamizi wa misitu walipo vamia misitu na kukata mapori ndivyo ninavyoona.

Mheshimiwa Mwenyekiti jambo lingine ni suala la kuwasaidia wananchi wanaolinda misitu. Kuwasaidia wananchi hao na kuwasaidia kwa upande wa ulinzi siyo kwa upande wa miradi kwa sababu mnasaidia hilo nimekwisha washukuru kwa upande wa ulinzi. Mapori hayo yanavamiwa sana na baya zaidi mlima wa Kilimanjaro upande mwingine hawa ndugu zetu majirani zetu wa Kenya wako karibu sana na mlima huo. Sasa kuna *corridor* la Kitende *corridor* ndiyo wanyama wanapita kutoka Kilimanjaro kwenda Emboseli ambayo Emboseli iko Kenya na kutoka Emboseli kwenda mlima Kilimanjaro.

Sasa wenzetu kule hilo *corridor* wameanza kugawagawa na kuweka mashamba kwa hiyo wanyama wanapoteremka kwenye mlima wa Kilimanjaro hawana tena nafasi ya kupita au wakitaka kutoka Emboseli kwenda mlima wa Kilimanjaro wanakosa nafasi ya kupita. Naomba muwasiliane na watu wa Kenya hilo *corridor* wanyama wapewe nafasi ya kuteremka kutoka mlimani na kupanda kwenda mlimani. Naomba mtusaidie kwa hilo kwa sababu ni mgogoro mkubwa sana na kulinda hilo *corridor* kwa sababu hilo *corridor* ndiyo mapito ya wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru kwa kunipa nafasi ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Rhoda Kahatano tusikie na upande wa kina mama wanasemaje. Karibu kuchangia.

**MHE. RHODA L. KAHATANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti napenda kukushukuru kunipa nafasi ili niweze kuchangia machache katika hoja hii. Kabla ya yote naunga mkono hoja, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na wafanyakazi wenzake katika Wizara kwa kuleta mambo muhimu ambayo sisi wengine tulikuwa tunayangoja kwa miaka mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti nitazungumzia sehemu mbili na ya tatu itakuwa ni jambo kidogo jipya haliko kwenye mazungumzo ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti kuhusu hifadhi ya Sadani nampongeza sana waziri kwamba ameleta suala hilo lakini nilikuwa namuomba Waziri aangalie jinsi ya kuwalipa wananchi wanaokaa katika sehemu ambazo sasa zitakuwa hifadhi, wawalipe fidia kwa sababu kuna malalamiko kwamba wananchi hawajalipwa fidia wawalipe fidia tena haraka itakavyowezekana ili wasiweze kunung'unika kama wanavyonung'unika. Kuinung'unikia Serikali kwa sababu Serikali inafanya jambo jema kufanya hifadhi ya

Sadani iwe hifadhi ambayo itaweza kuvutia watalii na kwa sababu iko karibu na Dar es Salaam wageni wengi watakwenda kutembelea sehemu hiyo na sisi tutapata fedha za kuweza kutusaidia katika maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, ambaye najua yeye ni Mtaalam wa wanyama pori ametueleza mambo ambayo kasa wa Sadani wanayo katika hulka zao jinsi walivyoumbwa na Mwenyezi Mungu. Lakini vile vile sijui jambo hili kama la wanyama wa Sadani kwamba ni wao wanyama pekee katika nchi yetu ambao wanakunywa maji ya chumvi. Wanyama kutoka Sadani maji ya bahari ya *India (Indian Ocean)* ni aghalabu sana wanyama na binadamu kunywa maji ya chumvi kwa hiyo hilo pia nadhani watalii watavutiwa kwenda kuona wanyama wa namna hiyo. Kwa hiyo, naomba hilo liende haraka kutunza eneo lile, kutengeneza barabara ili ziweze kuvutia watalii ndege tunasikia zipo sasa watu wataweza kusafiri kwa urahisi lakini barabara zivutie kwa sababu watu wengine wanapokwenda kule wanarudi magari yao yameharibika barabara ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti ninashukuru sana kwa kukumbuka bonde la Rungwe. Bonde la Rungwe lina vivutio vingi sana lakini kama watoto yatima watu wa mkoa wa Mbeya hawakufikiriwa kabisa habari za utalii sasa kama Mheshimiwa Waziri ameleta hapa turidhie mapendekezo haya na tuweze kuwa na matumaini kwamba mkoa wa Mbeya hautakuwa kama yatima sasa wana vitu vingi vizuri lakini hakuna mtu anayevithamini.

Unajua mtoto yatima nyumbani hata angeleta ndoo ya maji ambayo inamzidi kimo chake ni nadra mtu kushukuru, anamwambia tua weka hapo hata wasimsaidie kutua na mkoa wa Mbeya unavivutio vingi sana lakini inaonekana Serikali ilisahau; kabla ya uhuru na hata baada ya uhuru. Labda kabla ya uhuru wazungu walipanda tu samaki wakigeni katika mto Kiwira peke yake nadhani ndicho walichopanda na walikuwa wanakimbilia sana kwenda kupumzika katika ziwa lile la volcano la masoko.

Lakini baada ya hapo hakuna kitu kilichoendelea tena kwa hiyo sasa mimi nampongeza Mheshimiwa Waziri kwamba Rungwe watu waende wakaone daraja la Mungu wageni kutoka huko nje waweze kuona maji yanayopita katika mitungi ambayo Mungu mwenyewe ameiunda katika miamba ile ambayo iko katika mto Kiwira. Mitungi mikubwa ya maji, maji yanaingia kwenye mtungu lijito lizima linaingia kwenye mtungi linakwenda kutokea kwenye mtungi mwingine na kadhalika.

Kwa hiyo, tunafikiri kwamba tunaanza kupanua maendeleo ya utalii na watalii wengi watavutwa bila shaka kwenda Rungwe. Lakini ninachoomba pia barabara kuna hoteli kule Matema ni nzuri katika milima ya Livingstone lakini sasa barabara wakati mwingine inakuwa na matatizo. Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri kwa kushirikiana na Waziri mwenzake wa Ujenzi barabara za kwenda kwenye maeneo hayo ziimarishwe hasa kwa mwanzo ambapo watalii watakuwa wanapenda kuona vitu hivi ambavyo mtakuwa sasa mnavitangaza katika vitabu vyenu basi waende vizuri wasifikirie namna gani.

Nilikutana na mzungu mmoja Mbunge *South Africa* aliniambia unajua Tanzania naipenda sana lakini kila akifiri kwenda kwenye mbuga zingine anafikiria jinsi mafigo yake yatakapo pata shida. Nikasema figo zitapata shida namna gani? Akasema kwa sababu ya kuruka hivi barabara ni mbaya sana sehemu nyingine akasema hata hoteli tu ile ya Kunduchi kufika pale unajihoji lazima uamue je mtafika, anaamua na mafigo yake nasikia, akasema alafu ndiyo unakwenda mke wake akamwambia usimwambie hivyo lakini akasema huyu ni Mbunge lazima tumwambie ukweli wa nchi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mambo kama haya ya barabara ni lazima yaimarishwe. Kuhusu sehemu nyingine kule katika mkoa wa Mbeya sehemu nyingi zina vituo vya utalii kule Mbozi, kule Ileje kuna mambo mengi yakuvutia ya chemchem za maji yanayochemka ambazo ziko mahali pengi nadhani kwa sababu sehemu kubwa ya nchi ya sehemu ile iko katika bonde la ufa. Kwa hiyo, vinaweza kuvutia kule Kipengele gasi iko watu wanaweza kwenda kuona jinsi mlima ule wa Kipengele ulivyo na mlima Rungwe ni wa tatu lakini kupanda kwake ni rahisi sana mimi nimepanda mara sita nikiwa katika shule ya msingi.

Kwa hiyo, ni mlima ambao watalii wanaweza kupanda na kuteremka kwenda kuangalia mambo mengine muhimu jinsi vijito vinavyotoka mahali pamoja viwili hapa huu unakwenda huku na huu unakwenda kule. Mmoja unakwenda Iringa na mwingine unakwenda kwenye Wilaya ya Rungwe ni mambo ya kuvutia.

Mheshimiwa Mwenyekiti jambo lingine ambalo nilitaka kuzungumzia ni sehemu ya Kitulo ambayo sitazungumzia zaidi kwa sababu Mheshimiwa Jackson M. Makwetta amemaliza mambo mengi ambayo nilitaka kuyazungumza. Lakini ninalotaka kusema ni kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ukizungumza habari za Kitulo kwa kuwaambia Waheshimiwa Wabunge hivi hivi hawawezi kulielewa ni bora kufika Kitulo mtu aweze kuona mandhari ya Kitulo yalivyo ni mazuri ni kitu ambacho kinataka wewe mwenyewe ukione kwa macho. Kwa hiyo, ninadhani wakati mwingine Mheshimiwa Waziri atapanga kwa awamu Waheshimiwa Wabunge wapate kufika Kitulo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo nilikuwa nasema nitamwomba Mheshimiwa Waziri ni zile *Plateau* za Chunya ambapo unaangalia bonde la Usangu na unaangalia upande mwingine milima ya Kitulo. Ile *plateau* zamani wakati wa ukoloni ilikuwa *the highest area* ambapo barabara ilipita katika Tanganyika wakati ule lakini sasa najua kuna barabara nyingi zimepita katika maeneo mengine kwa sababu zamani tulikuwa na barabara mbili tu ya kutoka Iringa kwenda Mbeya na kutoka kule Chunya.

Sasa katika plateau ile ambayo kuna na misitu ya Kawetere na uzuri wa ile plateau ya Chunya unapoangalia bonde la Usangu na unapoangalia milima ya Kitulo nilikuwa namuomba Mheshimiwa Waziri ni ombi aliweke katika mawazo yake wakati mwingine muda ni mfupi uliyobaki Wabunge ili kuisha lakini si mfupi kwa kuweka mawazo aiweke hili nalo baadaye liweze kuingia katika hifadhi ili nalo liweze kufikiwa

na watalii kwa ajili ya faida ya nchi yetu. Kwa hiyo, hili ni ombi kwa Waziri nina muomba sana akaweze kuliweka katika matarajio yake ya baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti nilikuwa na machache hayo ya kumwomba Mheshimiwa Zakia H. Meghji na wewe ulisema unataka kusikia kwa mwanamke na kwa sababu yeye ni Mbunge mwanamke lazima atafuatilia mambo haya, nakushukuru Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Parseko Vincent Kone, malizia kipindi cha leo.

**MHE. PARSEKO VINCENT KONE:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia na moja kwa moja naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze umuhimu wa muswada huu, wenzangu wameeleza lakini na mimi nasisitiza kuchukua msitu wa mlima Kilimanjaro na Meru kuweka ndani ya hifadhi, hakuna watu wanao hamishwa hilo lifahamike. Ilikuwa inahifadhiwa na Serikali sasa inapandishwa daraja la uhifadhi kuwa mkubwa zaidi na kila mtu atakiri kwamba maji tunayopata kutoka mlima Kilimanjaro na mlima Meru tukiyakosa miji hiyo mizuri na hawa watu wazuri wanaoishi maeneo hayo watahama. Niseme tu kwamba mlima Kilimanjaro ni urithi wa dunia ni mlima pekee katika eneo la *equator* ambalo lina theluji. Wanaosema kwamba hawa wananchi wataenda kulima wapi hivi sasa hawalimi katika msitu huo na hata wangelima unaweza kupata shamba lenye rutuba popote Tanzania na unaruhusiwa kwenda. Lakini huwezi kupata mlima Kilimanjaro kwingine kote. *(Makofi)*

Huwezi kupata mlima Meru kwingine kote huwezi kupata mimea inayopatikana katika misitu hiyo kwingine kote. Mbega wanaoishi katika misitu ya Kilimanjaro na Arusha ni wa aina yake lakini shamba hata ukienda Tunduru unaweza kupata shamba zuri. Nenda Lindi utapata shamba zuri lakini mlima Kilimanjaro huwezi kupata hata Ulaya ni Tanzania tu ndiyo maana ni urithi wa dunia. Mlima Kilimanjaro Mheshimiwa Lekule Laizer ameeleza hapa maji ya Kitenden ukifyeka msitu huo Kitenden hapatakuwa na maji ile mito yote ya Wilaya Hai haitakuwa na maji na hata daraja kama lile la Siha halitajengwa ikikosekana hifadhi kama hiyo kwa hivyo kwa kusema kweli ni wananchi wameamua wenyewe kwamba msitu huo uhifadhiwe kwa hali ya juu. Hifadhi ya Saadani ni hifadhi ya aina yake huku kuna *beaches* huku kuna kuona wanyama pori lakini pia kuna aina ya miti ambayo haipatikani kwingine kote Tanzania inayopatikana katika hiyo misitu ya pwani pale Saadani. Hifadhi ya Kitulo, nimetembea katika hifadhi nyingi duniani lakini unayoweza kulinganisha na hiyo ni moja iliyoko Afrika Kusini inaitwa *Golden Gate.* Huwezi kuona kwingine na hii ya Kitulo itazidi hata hiyo ya Afrika ya Kusini. Kwa hivyo, wanaosema maeneo haya wananchi tutawapeleka wapi kwani hivi sasa kuna wananchi wanaoishi Kitulo? Hakuna nadhani labda wanashawishiwa na hawa wanaojua kwamba tutashindana nao ili walete vikwazo lakini sidhani kama kuna anayeleta kikwazo ila wanahitaji elimu. Kama kuna wakati Serikali yetu imewashirikisha wananchi katika kupata maeneo haya ya uhifadhi ni wakati huu. Ilianza kujadiliwa miaka minne iliyopita kwa mfano kuweka msitu wa Kilimanjaro kwenye hifadhi ni toka mwaka 1993 nikiwa *DC* Wilaya ya Hai hasa wakati mioto ilipozidi na nawashukuru wananchi wa Hai walivyokuwa wanashiriki sana kuzima mioto hiyo. *(Makofi)*

Tukaanza kupendekeza msitu huo uwe kwenye hifadhi lakini kwa sababu Serikali ilitaka kupata maoni wa wananchi tulienda polepole mpaka wananchi wameridhika na wameridhia. Mlima wa Meru umeanza wakati huyu *RC* wa Kigoma. Ndugu Mahawa akiwa *DC* Arumeru, ndiyo wananchi walianza kuomba msitu huo uwe hifadhi. Sijawahi kuona mito hii ya Arusha imekauka lakini sasa imeanza kukauka kwa sababu misitu inafyekwa. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa mawazo yake ya kuwashirikisha wananchi mpaka kuridhia katika kuhifadhi misitu hii nampongeza sana Waziri Zakia H. Meghji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti wananchi wanaotazama mbali wanakubaliana na maeneo haya kufanywa hifadhi na naomba tukubaliane kwa sababu hatuishi tu kwa kulima peke yake maeneo hayo wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro wanafaidi sana kwa kitu kinachoitwa *Cultural Tourism* na sisi tunaoishi karibu na hifadhi za taifa kama Tarangire tunafaidi sana kwa hifadhi hizi kutujengea shule, zahanati, maji lakini kwingine huwezi kupata hizo kwa kilimo tu peke yake na hata wakulima hebu mtuambie shule gani imejengwa na wakulima wakubwa. Mimi ninao wakulima wakubwa Simanjiro wanaolima ekari 2000/5000 lakini ni shule moja tu ya Maberera wamewahi kujenga lakini tuna shule nyingi tumejengewa na hifadhi za taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba tuzingatie pia kwamba leo tukiharibu mazingira na watoto wetu wasione tunayoyaona sisi tunafanya dhambi kubwa ya kuwaibia watoto wetu ambao hawajazaliwa. Wizi ni dhambi kubwa sana lakini nadhani dhambi kubwa kuliko yote ni kumuibia mwanao ambaye hajazaliwa. Kila mmoja sasa hivi atazame maeneo anamoishi yeye alipokuwa mtoto mdogo labda alikuwa anaona digidigi pale alikuwa anaona kanga alikuwa anakata kuni kwa karibu alikuwa anapata maji kwa karibu hivi leo mnayapata? Ni kwa sababu sisi wenyewe tumeharibu mazingira hayo, sasa ili tusiwe kati ya watu watakao hukumiwa baadaye na watoto wetu tukubaliane moja kwa moja hizi ziwe hifadhi na tupendekeze maeneo mengine yanayofaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala hili la uwindaji wa kienyeji najua wengine hawatapenda lakini naomba nilisema hili sisi Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro tumeomba Serikali Kuu isitolewe tena leseni za uwindaji wa kienyeji. Kwa sababu Serikali inatoa kwa nia njema mtu anapewa kibali cha kuwinda Swala wawili lakini naua Swala ishirini/thelathini sisi kama mlivyosikia hatuli nyama pori sasa tunakosa nyama tunakosa fedha ambazo tunajengewa shule kwa kuwa na hawa wanyama pori. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri pamoja na kuleta ombi hili la haya maeneo kufanywa hifadhi ukiona pia hilo ombi letu kweli tunaomba kwa dhati kabisa kwetu kusirusiwe uwindaji wa kienyeji walau kwa mia minne/mitano ijayo wanyama waongezeke.

Kwa sababu alivyosema Mheshimiwa Lekule Laizer hata twiga wanawindwa sasa na ni kutokana na uzushi kwamba eti Mifupa *marrows* za Twiga eti inatibu ukimwi nani kasema hivyo ndivyo hivyo pia Faru walivyotoweka kwa kuaminiwa pembe ya Faru inamanufaha kwa mwili wa binadamu hasa mwanaume. Faru wote wakamalizika ambayo

ni uongo lakini nao Twiga sasa wanaisha kwa hivyo naomba suala hili la uwindaji wa kienyeji, uwindaji wa kitalii uendelee lakini uwindaji wa kienyeji usimamishwe kwetu kwa sababu wala hawawindi kwa ajili ya kitoweo kama wanavyosema wanawinda kwa biashara na biashara ya nyama pori huko inafanyika zaidi Wilaya ya Rombo na Wilaya ya Same siyo Wilaya hata ya Simanjiro. Kwa hiyo, Mwenyekiti naomba niunge mkono muswada huu suala hili la kuhifadhi maeneo hayo na kwa kweli limekuja kwa wakati muafaka. Naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Parseko Vincent Kone kwa orodha tuliyokuwa nayo tumemaliza na napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Dr. James Mnanka Wanyancha kunielewa. Tukirudi Mheshimiwa Waziri atafanya majumuisho halafu tutaendelea na Agenda nyingine ambayo ipo kwenye *Order Paper.* Kwa hiyo, tunasitisha shughuli za Bunge mpaka hapo saa kumi kamili.

*(Saa 06.55 mchana Bunge lilifungwa hadi saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa juhudi kubwa inayofanya katika mapambano ya kupunguza maambukizi ya ukimwi.

Azimio lililo mbele yetu ni mwendelezo wa vita hii. Ni kweli kwamba magonjwa ya kuambukiza hayaheshimu mipaka ya kijiografia. Watu wanaoishi pande mbili za mpaka ni watu wa aina moja. Mila ni zile zile, wanatembeleana, wanashiriki shughuli za harusi, misiba, magulio n.k. Hivyo, kuna urahisi mkubwa wa maradhi yoyote kuvuka mipaka, kwa maana hiyo hatuna jinsi ni lazima mapambano yashirikishe majirani.

Mkataba huu unahusisha Tanzania na nchi 5 jirani. Lakini nchi jirani zinazoizunguka Tanzania ni 8, hivyo, ipo haja ya kuwa na mkataba kama huu na nchi za Zambia, Malawi na Mozambique, na ikibidi hata na nchi zote za *SADC.*

Pili, ugonjwa wa Kifua kikuu unafuatwa na Ukimwi kama kivuli. Ingependeza kama Azimio hili lingejumuisha magonjwa haya mawili ili Serikali zisipate shida ya kutayarisha Azimio lingine linalohusu ugonjwa wa kifua kikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono.

**MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Hoja iliyopo hapa mbele yetu sote ni ya muhimu sana na imekuja katika muda muafaka na hasa kwa

kuzingatia kuwa nchi za maziwa makuu zimeamua kuridhia mkataba wa pamoja dhidi ya Ukimwi.

Sambamba na Azimio hili, bado ipo haja ya kuainisha kwa kina jinsi gonjwa hili la Ukimwi lishughulikiwe kwa maslahi ya wananchi husika. Licha ya jitihada za Serikali kupambana na vita dhidi ya Ukimwi, bado kuna haja ya kuangalia jinsi gani mila na desturi zetu hazizingatiwi. Aidha, fedha nyingi sana zinatumika katika mambo ya semina, makongamano na warsha badala ya kuelekezwa zaidi katika kupambana na Ukimwi. Matangazo mengi sasa yanapotosha badala ya kusaidia kupiga vita Ukimwi. Elimu ya ukimwi inatolewa bila kuzingatia maadili mbadala ya wananchi na badala yake huja mila potofu ndani na nje ya makanisa na misikiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Azimio.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakupongeza kwa kuleta azimio hili muhimu. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono napenda kuchangia/kushauri yafuatayo:- Kwanza, Fedha zinazotolewa kama misaada zitumike kama zilivyokusudiwa na zitumike nchi nzima kwa kuwa janga la Ukimwi ni la nchi nzima. Pili, fedha hizo zisaidie kutunza watoto yatima, kuwasomesha na matumizi mengine, pia kusaidia waathirika lishe bora zitakazosaidia kurefusha maisha na kununua madawa kwa ajili ya waathirika, pia elimuya kutosha itolewe kwa wananchi wote kuhusu athari za ukimwi

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio hili limeletwa wakati muafaka na Serikali yetu ipongezwe kwa kuona janga hili ambalo limetikisa mataifa yote. Kupambana na janga hili kunahitajika nguvu za ushirikiano na nchi zote pamoja na nchi jirani. Naunga mkono kwa dhati Azimio hili. Ukimwi sasa sio utani na zana ya kulionyesha janga hili kwenye vyombo vya habari kama *TV,* Magazeti na Radio ni kupotosha umma kwa hali mbaya inayoendelea kulinyemelea taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kukosoa kwa nia nzuri kuhusu jinsi Serikali yetu inavyolichukulia janga hili kama ni tatizo dogo na la kawaida tu katika jamii yetu:-

(i) Serikali yetu haitengi fedha za kutosha katika bajeti za kila mwaka kushughulikia janga la Ukimwi kuanzia elimu kwa wananchi, kuhudumia walioathirika *(tested positive),* wagonjwa wa Ukimwi, huduma za kupatikana kwa wingi na kwa bei nafuu za madawa ya kurefusha maisha kwa wagonjwa wa Ukimwi, kuwasaidia wajane na watoto yatima walioachwa kwa sababu ya vifo vya Ukimwi.

(ii) Mpaka sasa Serikali imechukua hatua nzuri ya kuanzisha Taasisi ya *TACAIDS* lakini taasisi hii haijazamia vya kutosha kuwafikia wananchi walio wengi waliopo vijijini. Taasisi hii inaendesha semina na makongamano mengi mijini tu na si vijijini. Pia taasisi ya *TACAIDS* haipeleki uwezo wa kutosha wa kifedha na utaalam kwa Halmashauri zetu ambazo ndizo zinawahudumia wananchi walio wengi vijijini na ambapo elimu haipo kabisa.

(iii) Katika kupambana dhidi ya Ukimwi Serikali isilione janga hili ndani ya jamii yetu kama suala la jumla tu. Itakuwa busara kubwa kama maeneo yanayoathirika zaidi na kwa haraka zaidi yapewe kipaumbele. Kwa mfano, vijiji kando kando ya barabara kuu kama vile barabara ya Dar es Salaam-Dodoma-Singida-Nzega-Shinyanga-Mwanza. Kwa sababu ya ubovu wa barabara hii kuanzia Dodoma kuendelea Singida-Shinyanga-Mwanza, magari makubwa yanatumia muda mrefu kukamilisha safari zao, matokeo yake wananchi walio kando kando ya barabara kama hii wanaathirika sana na maambukizi ya Ukimwi. Ninalojaribu kusema hapa Serikali ione umuhimu wa kupanga maeneo yanayoathirika na janga la Ukimwi kufuata hatari zaidi kwa wananchi *(priority ratings of areas prone to be infected by HIV-AIDS)*

(iv) Suala zima la kutokusambaza madawa na vyakula vya kurefusha maisha kwa waathirika vijijini na kwa bei nafuu linawafanya wananchi wa vijijini kama kuachwa kupukutika kama majani posipokuonewa huruma na Serikali. Ningeshauri Serikali sasa itazame hali halisi ya Ukimwi katika kila Wilaya. Katika Wilaya ya Iramba sasa tatizo la Ukimwi ni kubwa mno kwani barabara kuu kutoka Dodoma kwenda Mwanza imegawanya Wilaya hii katikati kwa mfano katika Wilaya ya Iramba sasa hivi kuna wagonjwa wa Ukimwi karibu 108, walioathirika *(positive)* 158, watoto yatima 368 ambao kati ya hawa 220 hawana uwezo kwenda shuleni.

Naomba kama Serikali kwa kupitia *TACAIDS* wapeleke msaada wa haraka katika Wilaya ya Iramba na mipango kabambe ianzishwe kuinusuru Wilaya ya Iramba kutoka kwenye janga hili. Nitakuwa tayari kabisa kutoa taarifa zaidi kuhusu janga la Ukimwi kwenye wilaya ya Iramba.

Mheshimiwa Naibu Spika namalizia kwa kuunga mkono Azimio hili muhimu.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Azimio hili ni zuri sana lina unganisha nchi mbalimbali katika kupambana na ugonjwa huu. Ni vizuri sana kwa janga kubwa kama hili nchi iwe na wenzake. Nchi moja peke yake haliwezekani kabisa kupambana na nchi nyingi, mbinu huwa nyingi na uwezo huwa mkubwa. Ninawatakia kila la kheri, naliunga mkono.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kuhusu Maazimio manne ambayo tuliyawasilisha asubuhi hii ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliozungumza na kuunga mkono hoja zetu. Waliochangia kwa kuzungumza walikuwa Waheshimiwa Wabunge tisa na ningependa kuwataja. Kwanza kabisa ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Hassan Khatib, Mheshimiwa Salim Omar Ali, Msemaji wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Ngawaiya, Mheshimiwa Ndugai, Mheshimiwa Nyami, Mheshimiwa Makwetta, Mheshimiwa Shekiffu, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Rhoda Kahatano na Mheshimiwa Kone. Wako wale waliochangia kwa maandishi nao walikuwa, Mheshimiwa Ndunguru Ngwatura, Mheshimiwa Janet

Kahama, Mheshimiwa Phillip Marmo, Mheshimiwa Mulyambatte na Mheshimiwa Semindu Pawa. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli napenda kutoa shukrani sana kwa sababu kilichozungumzwa hasa hasa ni kuunga mkono lakini pia wale wote ambao waliochangia wametoa maelezo zaidi ya hoja hizi na kuweza kujibu masuala mbalimbali yaliyozungumzwa na Kambi ya Upinzani, lakini pia na Mheshimiwa mmoja ambaye hakuunga mkono Mheshimiwa Mbunge Ngawaiya. Kwa hivyo, hoja hizi zimejibiwa sababu gani maeneo haya yawe hifadhi, yaongezewe maeneo na suala zima la Saadani pia limejibiwa. Napenda kusema kwamba kwa kweli hoja hizi na umuhimu wa kuridhia umejibiwa. Lakini labda nielezee hilo moja ambalo nimekuwa na wasi wasi na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge nalo kuhusu fidia. Napenda kufafanua kuwa fidia kwa upande wa Saadani ni kwamba wananchi wameanza kulipwa fidia na mara baada ya kikao hiki fidia hizi zitamalizwa. Wiki iliyopita tu Bodi ya *TANAPA* iliketi na kuweka fedha zote ambazo zitahitajika kwa ajili ya fidia. Kwa hiyo, hakuna matatizo yoyote katika suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyoeleza ni kwamba katika upande wa Kilimanjaro ni kuchukua eneo lile la hifadhi ya misitu ambalo liko chini ya Wizara yangu. Hivyo, hakuna suala la kusema kuchukua maeneo ya wananchi. Kwa sababu hata misitu ile ya Serikali itabakia kutumiwa katika utaratibu uliokuwepo kati ya wananchi na Serikali. Kwa hiyo hakuna tatizo. Niseme kwamba ni wananchi wenyewe kwa kweli wamependelea kuwa na hifadhi hizo. Utaratibu wa kuanzisha hifadhi hizi hivi sasa umebadilika tofauti na utaratibu uliokuwepo zamani. Hifadhi hizi sasa kwa kweli zinazungumzwa na wananchi wenyewe ama wanaleta mapendekezo yao na mpaka wanakubaliana kwa asilimia kubwa ndipo tunaleta masuala haya Bungeni.

Nasema kwa bahati Mheshimiwa Ngawaiya ambaye ni Mbunge wa Moshi Vijijini labda hakulielewa hili suala. Lakini labda ningependa kusema kwamba ni vizuri kama Mheshimiwa Mbunge wa Moshi Vijijini pengine angeelewa kwamba suala hili ni la wananchi wenyewe wamelileta na ni suala ambalo litasaidia wananchi, aweze kuwa na mtazamo wa mbali zaidi kuliko kuwa na mtazamo wa karibu. Tulipokuwa katika Kamati Mheshimiwa Ndesamburo ambaye pia ni Mbunge wa Upande wa Upinzani kutoka Kilimanjaro aliunga mkono mia kwa mia na akasema kwamba labda pengine tumechelewa tungelifanya hili kabla ya hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda kuna maeneo Mheshimiwa Ngawaiya ameyaleta ambayo yalikuwa hayahusiani sana na hoja hii. Kwa mfano masuala ya uvuvi, labda nijibu tu kwa taarifa ya Waheshimiwa Wabunge ni kwamba katika upande wa uvuvi hasa hasa *deep sea* si kweli kwamba Serikali imeachia meli kuondoka hivi hivi. Serikali imekamata meli 17 na meli hizi zimetozwa faini na fedha zilipatikana karibu shilingi bilioni moja.

Lakini pia katika suala zima la utalii Mheshimiwa Ngawaiya naye halielewi. Hata jana tu kama anasikiliza redio ataona kwamba Serikali imeingia Mkataba na

Serikali ya Sweden katika kuendeleza maeneo ya kihistoria ya Kilwa, Bagamoyo na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niseme kuna wengine waliulizia kuhusu Azimio la Upanuzi wa Hifadhi ya Manyara. Napenda kusema kwamba Azimio hili lingekuwa lije pamoja na Maazimio haya lakini kumetokea matatizo kidogo na ambayo tunamalizia. Kwa hiyo, tunatumaini kwamba Azimio hili la hifadhi litaletwa hapa kwa sababu bila ya kuwa na Azimio hilo au kupanua hifadhi hii ya Manyara bado tunaweza kusema muda si mrefu hifadhi hii ya Manyara inaweza kutoweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo narudia kushukuru Waheshimiwa Wabunge wote natumaini tutashirikiana katika shughuli hizi na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kama mnavyoona pale kuna Maazimio manne, kwa hiyo, kila moja tutalipitisha kwa wakati wake.

Azimio la Kuridhia Upanuzi wa Hifadhi ya Arusha

*(Azimio lililotajwa hapo juu liliridhiwa na Bunge)*

Azimio la Kuridhia Kuanzishwa kwa Hifadhi Mpya ya Taifa ya Kitulo

*(Azimio lililotajwa hapo juu liliridhiwa na Bunge)*

Azimio la Kuridhia Upanuzi wa Hifadhi ya Taifa la Kilimanjaro

*(Azimio lililotajwa hapo juu liliridhiwa na Bunge)*

Azimio la Kuridhia Uanzishaji wa Hifadhi Mpya ya Taifa ya Saadani

*(Azimio lililotajwa hapo juu liliridhiwa na Bunge)*

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Maazimio yaliyotajwa hapo juu yaliridhiwa na Bunge)*

**Azimio la Kuridhia Mkataba wa Ushirikiano wa Nchi za Maziwa Makuu Katika Kupiga Vita Ugonjwa wa UKIMWI**
***(The Convention Establishing The Great Lakes Initiative on AIDS (GLIA)***

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kuwasilisha Mkataba unaoanzishwa Ushirikiano wa Nchi za Maziwa Makuu Katika Kupiga Vita Ugonjwa wa UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala pamoja na Waheshimiwa Wabunge wa Kamati hiyo waliowezesha kuupitisha na kuuchambua Mkataba kwa nia ya kuuelewa na kuuboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni nchi mwanachama wa Umoja wa Mataifa ambao umedhamiria kupiga vita janga la UKIMWI. Baada ya kutambua uzito wa athari mbaya za UKIMWI Mkutano Maalum wa Wakuu wa Nchi *(United Nation General Assembly 1st Session)* uliitishwa mwezi Juni 2001 kuzingatia suala hilo. Kati ya Maazimio ya Kikao hiki Azimio Namba 42 lililenga kupanua na kuimarisha ushirikiano kikanda kama *(GLIA)* inavyokusudia. Umoja wa Mataifa umeanzisha *UNAIDS* na Mfuko wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria *(Global Fund to Fight AIDS, Tuberculosis and Malaria)* kwa ajili ya kusaidia na Kuratibu vita dhidi ya UKIMWI.

.

Mnamo mwezi Agosti 1997 Mawaziri wa Afya wa nchi za Maziwa Makuu yaani Burundi, Kongo, Kenya, Rwanda, Tanzania na Uganda walikutana Kigali ambapo waliazimia kushirikiana katika kudhibiti magonjwa yanayoambukiza. Mnamo mwaka 1998 nchi hizi pamoja na *UNAIDS* zilikubaliana katika Mkutano wa Kampala kushirikiana kwa karibu sana kudhibiti UKIMWI. Ndipo ilipoanzishwa Sekretarieti ya *(GLIA)* kwa msaada wa *UNAIDS* na Rwanda ikakubali kuwa mwenyeji wa chombo hicho. Katika Kongamano lililofanyika Nairobi mwezi Mei, 2003 Benki ya Dunia ilionyesha nia ya kugharamia na kusimamia chombo cha Kanda cha Kudhibiti UKIMWI. Wawakilishi wa nchi hizo sita walitoa tamko rasmi la kuiafiki dhana ya ushirikiano wa muundo *(GLIA)* uliobuniwa. Benki ya Dunia imekubali kutoa shilingi dola milioni 15 kwa miaka mitatu na matayarisho ya Mkataba yakaanza.

Bodi ya Benki ya Dunia itakayokutana mwezi Desemba 2004 inatarajia kuidhinisha matumizi haya iwapo nchi zote ikiwemo Tanzania pamoja na nchi zingine tano wanachama zitakuwa zimeridhia Mkataba huu. Kwa hiyo, katika kuridhia Mkataba huu hakuna gharama yoyote isipokuwa nchi husika zinaweza kuchangia gharama za Sekretariet katika siku za usoni. Itakapotokea mchango wa aina hiyo utawekwa katika makadirio ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania. Chombo hiki hakina muundo mkubwa kitakuwa na Kamati Kuu *(Central Committee),* Baraza la Mawaziri *(Council Ministers)* na Kamati ya Utendaji *(Executive Committee)* ni Watendaji Wakuu wa Kamisheni au Tume za Kudhibiti UKIMWI za kila nchi. Katika hali hii Sekretarieti lazima itakuwa na maafisa 7 na uratibu unaohusisha fedha na nyenzo nyingine utaendeshwa zaidi na chombo kisichofungamana na nchi yoyote, hii itarahisisha pia mawasiliano na wabia wa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kwamba virusi vya UKIMWI havitambui mipaka ya utawala. Chombo hiki kitawezesha kukabiliana na janga hili katika eneo lolote la Maziwa Makuu kwa utaratibu madhubuti na endelevu. Tutaweza kuratibu

operesheni, kitashughulikia utawala na kitafanya tathmini katika eneo lote. Vile vile katika uhusiano wa Kimataifa kitakuwa na sauti ya Kanda katika udhibiti wa UKIMWI baada ya kuratibu mawazo na maoni ya nchi husika. Mpango huu utatuwezesha pamoja na majirani zetu kuyashughulikia maeneo tunayochangia, kwa mfano maeneo yenye Wakimbizi ambayo sisi tuna maeneo mengi.

Njia kuu za usafirishaji hasa barabara (nchi nyingi za Maziwa Makuu wanatumia barabara zetu hasa kusafirisha mizigo kutoka Bandari ya Dar es Salaam) na mitandao ya waathirika katika matibabu ya UKIMWI pale ambapo raia wetu wanachanganyika. Mpango wa *GLIA* hautarudia mipango na wala hautakuwa mbadala wa mipango au miradi ya nchi hizo sita. Utakuwa nyongeza kwa jitihada za kila nchi.

Sera ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI inatuhimiza tuwe na ushirikiano wa Kimataifa. Kujiunga na mpango huu ni moja ya utekelezaji wa sera yetu. Kwa hiyo, kwa kuzingatia umuhimu wa kudhibiti UKIMWI na faida ya kushirikiana na mataifa mengine ya jirani, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wake wa Kumi na Saba, linaoombwa liazimie kwa mujibu wa ibara 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kuridhia Mkataba unaoanzisha Ushirikiano wa Nchi za Maziwa Makuu katika kupiga vita UKIMWI (*The Convention Establishing the Great Lakes Initiative on AIDS (GLIA).*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kusoma Azimio lenyewe kama ifuatavyo:-

KWA KUWA nchi yetu ni mwanachama wa Umoja wa Mataifa ambao katika Kikao chake maalum cha mwezi Juni, 2001 uliazimia kupiga vita ugonjwa hatari wa UKIMWI;

NA KWA KUWA nchi yetu ni mshiriki katika Ushirikiano wa Nchi za Maziwa Makuu ambazo zimekumbwa na janga la UKIMWI kwa viwango mbalimbali;

NA KWA KUWA kutokana na ushirikiano wetu na mifumo ya jamii ya wananchi wa nchi za Maziwa Makuu ambayo inaruhusu wananchi wetu kuvuka mipaka na kutembeleana kwa ajili ya shughuli ya kijamii, kiuchumi na pia kutokana na mwingiliano wa tatizo la Wakimbizi, mambo ambayo huwezesha kuenea kwa virusi vya ugonjwa huu hatari kutoka nchi moja hadi nyingine;

NA KWA KUWA ushirikiano kati ya mataifa jirani una umuhimu wa kipekee katika kudhibiti ugonjwa huu hatari wa UKIMWI;

NA KWA KUWA Tanzania ikijiunga na *GLIA* itafaidika kwa kushirikiana na nchi wanachama katika kudhibiti UKIMWI katika maeneo tunayochangia kama vile njia kuu za usafirishaji hasa barabara na pia katika tiba, maeneo ambayo yana waathirika wengi;

KWA HIYO BASI, kwa kuzingatia umuhimu wa Mkataba huu na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977, Bunge hili

katika Mkutano wake wa Kumi na Saba linaazimia kuridhia Mkataba unaoanzisha Ushirikiano wa Nchi za Maziwa Makuu katika kupiga vita UKIMWI (*The Convention Establishing the Great Lakes Initiative on AIDS (GLIA)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS (k.n y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kan. Na. 70(2), Toleo la 2004, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Ushirikiano wa Nchi za Maziwa Makuu katika kupiga vita ugonjwa wa UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuipatia Kamati yangu kazi hii ya kujadili Azimio hili, Kamati ilikutana leo tarehe 5 Novemba, 2004 na kupokea maelezo ya Serikali yaliyowasilishwa na Mheshimiwa William Lukuvi, Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera).

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupokea maelezo ya Serikali napenda kutamka kuwa kimsingi Kamati yangu inaliunga mkono Azimio hili kwa sababu kama alivyoeleza mtoa hoja linalenga kuwasaidia wananchi wetu katika nchi za Maziwa Makuu na kwamba Kamati yangu inaamini kuwa misaada itakayotolewa ina umuhimu mkubwa kwa nchi zetu katika kupambana na vita dhidi ya janga la UKIMWI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono kuna maelezo machache ambayo Kamati yangu ilitaka ipewe ufafanuzi. Kubwa lililojitokeza linahusu sehemu ya tafsiri na maudhui ya Mkataba kwa jumla ambayo

Kamati yangu ilihoji ni kwa vipi msisitizo zaidi umewekwa kwenye Ziwa Victoria ukilinganisha na Maziwa mengine yaliyopo karibu na Ukanda huu. Kamati ilitaka kujua mantiki ya tafsiri hiyo kwa kuzingatia kuwa nchi nyingine zinazopakana na Maziwa mengine hasa Kusini mwa Afrika hazikutajwa. Mheshimiwa Naibu Spika, ninafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali ilitoa maelezo yake ya kina kuhusu suala hili ambayo Kamati yangu iliafikiana nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema awali, Azimio hili lina umuhimu mkubwa kwa wananchi wote wa ukanda huu na litasaidia sana kuimarisha jitihada za nchi yetu kupambana na UKIMWI. Kwa sababu hiyo Kamati yangu haioni sababu kwa nini isiunge mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha maoni ya Kamati. Aidha napenda niwashukuru

Mheshimiwa William Lukuvi, Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera) na Meja Jenerali (Mstaafu) Herman Lupogo, Mwenyekiti Mtendaji wa Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI pamoja na timu ya wataalamu wao kwa ushirikiano wao na kwa maelezo ya kina na ufasaha waliotoa mbele ya Kamati.

Aidha, napenda niwashukuru wajumbe wa Kamati hii kwa busara zao walizozionesha kuliunga mkono Azimio hili katika wakati huu ambao wananchi wetu wanakabiliwa vikali na janga hili la UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Athumani S. Janguo, Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa George Lubeleje, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa Chifu Abdallah S. Fundikira Mheshimiwa George F. Mlawa, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Rosemary Nyerere, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba na Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Khamis Salum Ali, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Ramadhani Khalfani, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Nimrod Mkono na mimi, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis.

Aidha, naishukuru Ofisi ya Bunge kwa kutoa ushirikiano wa kutosha wakati wa kujadili Azimio hili bila ya kuwasahau Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Charles Mloka na Ndugu Ernest Zulu, kwa kutayarisha maoni ya Kamati haraka ilivyowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naiunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. GRACE S. KIWELU (k.n.y. MHE. WILFRED M. LWAKATARE-MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA OFISI YA WAZIRI MKUU):** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni Namba 43(5)(b) na (c), Toleo la mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inatoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri kwa kuleta Azimio hili kwa ajili ya kuridhiwa na Bunge hili. Kimsingi Tanzania ilikwishakubaliana na mambo yote yaliyomo kwenye Mkataba wenyewe. Hivyo utekelezaji wa Mkataba huu utaisaidia Tanzania katika harakati za kupambana na janga kubwa la UKIMWI. Aidha, Mkataba huu utatoa fursa kwa nchi wanachama kushirikiana na kupambana na ugonjwa huu hatari kama tunavyoshirikiana kwenye biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaipongeza Serikali kwa kuchukua uamuzi huu kwani ni wakati muafaka kwa sababu kasi ya maambukizi ya

virusi vya UKIMWI nchini mwetu inatisha sana kwani maambukizo yanatishia Nguvu Kazi na uchumi wa Taifa kwa jumla. Vita vya kupambana na ugonjwa wa UKIMWI si vya watu, familia au Taifa moja, ni vita vinavyohitaji kuhusisha watu wote na mataifa yote kwani hakuna Taifa ambalo halijaathirika na janga hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inajua kabisa pia kuridhia kwa Mkataba huu kutaanzisha chombo kitakachosimamia na kuratibu vita dhidi ya UKIMWI kwa nchi wanachama. Aidha, Taasisi za Kimataifa kama vile *UNAIDS, Global Funds to Fight to AIDS, Tuberculosis and Malaria* na Benki ya Dunia zimeonyesha nia ya kutoa fedha kwa ajili ya kusaidia na Kuratibu vita dhidi ya UKIMWI. Benki ya Dunia imekubali kutoa jumla ya dola 15,000,000 kwa ajili ya kazi hiyo pindi mkataba huu ukisharidhiwa na nchi wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na lengo zuri la kuingia kwenye Mkataba huo Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali ichukue hatua madhubuti za kudhibiti utumiaji wa fedha zitakazotolewa na taasisi hizi.

Matumizi ya fedha hizi yalenge waathirika wa UKIMWI na sio zitumike kwa ajili ya semina, warsha na makongamano huku tukiwaacha waathirika wa UKIMWI wakiwa hawana msaada. Wale wote watakaobainika kutumia fedha hizo vibaya wachukuliwe hatua kali za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa Wabunge, hapa tumemaliza wale wasemaji wakuu. Ninao Wabunge walioomba wanne nitawasoma na nitawaita kwa utaratibu huo. Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai na Mheshimiwa Dr. James Wanyancha.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii kuchangia katika hoja hii ya Waziri Mkuu.

Kwanza niipongeze sana Serikali kwa jitihada zake kabisa za kupambana na ugonjwa huu wa UKIMWI na vile vile katika kujihusisha na Mataifa mbalimbali duniani katika kupambana na janga hili ambalo limetupata.

Katika jitihada hiyo ugonjwa wenyewe ni mzito na umemaliza maisha ya watu sana na umeleta huzuni sana. Tuliona picha zile za Makete zilikuwa zinatisha sana. Nadhani wale wanaohusika wangeonyesha picha zile mara kwa mara zingesaidia sana.

Kwa kuwa unaona ni ugonjwa mzito na unahitaji nguvu ya pamoja ukipigana peke yako huwezi. Kwa hiyo, Serikali inapoingia kwenye Mikataba kusaidiana au nchi inapoingia kwenye Mikataba kwa kupambana kusaidiana na nchi zingine hili ni jambo ambalo tunafikiri ni jambo zuri na muhimu na tunapongeza sana juhudi zote hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua sasa hivi katika ulimwengu wa leo dunia imekuwa ndogo mno. Ukiingia Dar es Salaam utakuta Wazambia wako pale wamejaa, Wazimbabwe wamejaa, wanatembea kwa mabasi tu kiasi ambacho dunia nzima watu sasa wanatembea *everywhere*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mkiwa na juhudi za pamoja kama mnafanya kwa pamoja itawasaidia sana kwa sababu itakuwa kama unaongea kama *block* moja. Kwa hiyo, ni vizuri kabisa tuiunge mkono Serikali katika hili.

Kabla ya tatizo niseme kwamba kwa kweli inahitaji elimu. Mimi naona sasa jambo la msingi ni elimu zaidi. Utoaji wa elimu tunaoutoa kuhusiana na ugonjwa huu tunapoingia kwa wenzetu ni kama vile tunaingia kwenye timu kucheza mpira.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama unakwenda kucheza na wenzako ambao tayari wanaelewa namna ya kucheza wewe unaweza kuwa mshangiliaji tu, yaani unakimbia kiwanja kizima wenzako wanakupiga chenga tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, tunapoingia kwenye mambo kama haya ni lazima tujiangalie sisi, hatua zipi tumezichukua na za makini ambazo tukijumuisha na za wenzetu kwa pamoja tunaweza tukapambana na UKIMWI.

Mimi naona elimu ndiyo kitu cha kwanza. Watu wakishaelimika wakajua sana mpaka kule kwenye *grassroot* isiishie mjini tu, isiisishie kwa watu wanaofahamu tu itakuwa ni matatizo. Maana ugonjwa huu ni ajabu sana. Mimi nadhani kule vijijini kuna nafuu kuliko mijini, ni vijiji vichache sana vinaanza kuathirika kwa sababu ya maingiliano *(movements)*. Kuna minada watu watoke Mbeya waende wakafanye mpaka kwenye vijiji vya Msamba. Minada hii walale huko. Magari yapo vijiji mbalimbali barabarani yako hapo na unakuta sasa watu kama wameathirika eneo fulani ndio wanazidi kutembea katika nchi nzim , basi unakuta ugonjwa unazidi kuenea. Ndiyo maana kwenye vituo vya magari ugonjwa unaenea sana hasa yale magari makubwa, malori. Kwa hiyo, elimu hii sisemi hii elimu ya kujua *a, b, c,* na *d.* Naongea juu ya elimu ya watu wenyewe hata mimi kubadilika kupata elimu tofauti ile ya kujua kusoma na kuandika hii bado. Kuna baadhi ya vijiji hali inaweza kuwa nafuu kuliko sisi ambao tulikwenda shule. Maana watu wakisoma wanajifanya wanajua, wanatafuta mbinu kwamba unaweza ukafanya hivi ukakwepa hili tukatafuta sisi mbinu kwa sababu tunajua tumekwenda shule. Kwa hiyo elimu itolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka nisisitize kuwa elimu inayotolewa ni lazima ilingane na mazingira na utamaduni. Kitu kingine unaweza ukaita kero. Unataka kuwaambia watu kitu cha msingi kabisa lakini ukaleta kero kwa wenzako. Hili suala la UKIMWI limeingia lakini kumejitokeza vikundi vingi sana vinajaribu kutoa elimu ya mambo ya UKIMWI. Nilikuwa nikitaniana na Meja Jenerali Lupogo sasa hivi, nikasema, “loh! utapambana na vikundi vingi sana.”

Lakini nataka nimweleze kabisa sisi Wabunge ndugu zake tunatembea sana katika nchi hii na kwenye makongamano mbalimbali. Sehemu nyingine imeonekana kwamba huu ugonjwa wa UKIMWI umebadilika kuwa ni mradi wa hali ya juu. *(Makofi)*

Sisi tumehudhuria semina nyingi. Wabunge tunatembea sana ndugu zangu. Tunakuta sehemu zingine ambako hawafanyi kama, mradi wa watu binafsi *(self financing project),* hawakufanya hiyo, walifanya ni shughuli ya kwenda vijijini, ni shughuli ya kumlenga anayehusika, kule walifanikiwa. Uganda *being a very good living example* wamejitahidi sana. Lakini hawakufanya ajizi, hawakuwafanya *(dance),* hawakuchezea UKIMWI, hawakuwa wanaimba wanacheza, wamevaa vinguo tu wanacheza hapana! Huwezi kuwa unacheza *dance* tu pale unanengua tu unasema unahubiri UKIMWI, unanengua, ni kweli maneno ni ya UKIMWI, lakini sasa vitendo havionyeshi *sense of seriousnes*s, hakuna umakini, ni kama vile kuna kamzaa hivi. *(Makofi)*

Halafu ukitaka kuwashauri watu wanakuja juu. Sasa watu ni wasomi, watu wanakwenda na watu mbalimbali, wanasema katika *drama* hili la kucheza hivi watu hawawezi kuona kwamba kuna *seriousness* yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, *you can compare* kile kipindi cha Mama Betty Mkwasa wapo vipofu nadhani wawili au watatu au wanne wanaimba kuhusu UKIMWI. Wanasema fulani amekwenda, amekwenda kaburini na kwa kweli wale unakuwa *captured* kwa tendo kusikiliza kwamba kweli hapa nafikiri lazima mambo haya niyafikirie mara mbili jamani. Maana inatisha wanavyoimba wale watu. Sasa yule ndiye anayefanya kazi nzuri ya kupiga vita mambo ya UKIMWI. *(Makofi)*

Ile ndiyo shughuli maana inatakiwa mtu imletee simanzi aone kwamba sasa hapa hili jambo ni baya, yaani linaingia inaondoa (*devil in your head)*, shetani anaondoka. Lakini kama itaonekana tunakumbatiana, tunapigana kisi, halafu tunaelezana kitandani, sijui wanalala, sijui wanafanya nini, halafu mkishauriwa vijana wanasema *aah!* Sisi bwana hii ni sisi wenyewe tumeamua wazee na waende zao, *ahaa!* nchi gani ambayo watu hawashauriwi? kwanza vijana wanaweza kujenga nchi? Nchi gani ambayo vijana wanajenga nchi? *(Makofi/Kicheko)*

Wanasema *what can be seen by an old man, while siting can not be seen by a child while standing.* Mtu mzima akitazama jambo akaliona ameketi chini, mtoto mdogo hata akisimama hawezi kuliona, haya unayoyafanya wenzako yalishapita wana *experience* wanapinga. Mimi nadhani *Major General* Lupogo atusaidie tu, hapa hamna haja. Kwanza, nataka niseme uwazi humu Bungeni, sidhani kama lile tangazo la *Ishi* lile la *ku-dance* pamoja na hili la watoto kukumbatiana wale, mimi sidhani kama ni tangazo la maana pale, mimi naona ni la kipuuzi. *(Makofi)*

Pamoja na ugumu wa mioyo ya watu kwamba linafaa, mimi naona lile halifai na kweli mimi wala siwaungi mkono katika hilo, namuunga mkono Betty Mkwasa na lile tangazo lake la wale wanaoimba vipofu na kwa kweli yangeletwa hapa tukalinganisha tukaanza kuangalia la Betty Mkwasa likaimba kwenye *Video* pale tukaona halafu wale

wanaosema *Lelele! Lelele, hayaa yebaaa! There is not sense of seriousness there* hakuna, ni upuuzi. *(Makofi/Kicheko)*

Lakini wanasema *aah!* Tuacheni, ndiyo tunachomeka mle nasema wanaweza wakafanya vile vile isifundishe, maana mimi mwalimu wa *literature,* ni mwalimu wa *drama they can do that* lakini *in the end* yule mwanamke akatae, aondoke moja kwa moja "sitaki!" "sitaki" akakimbia, *(the end is hopeless)*, ile mwisho wake wa ule mchezo ni upuuzi mtupu. Basi ifike amkumbatie kama mnataka wakumbatiane ndiyo imekuwa biashara basi wakumbatiane basi, lakini ifike mahali yule binti amkatalie tena kwa nguvu siyo tu hivi hivi, mbona ni kitu cha kawaida jamani, si ndiyo kawaida, kuna watu wanakimbia mbio hata kufanya hivi, umefuata unakimbia, unaanguka ndiyo mtindo wa zamani huo, mbona ni kitu cha kawaida. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa eti kakafanya tu hivi basi eti pale ndiyo amekataa! Sasa sijui amevaa kondomu sijui amefanya nini, halafu wanacheza, wameshamaliza sijui nini. Kwa kweli mimi nasema wazi, lile tangazo nalichukia na kila TV linapoonyeshwa mimi huwa nazima kwa sababu ni upuuzi tu. Mwalimu mzima niliyesomea mambo haya waseme lile ndiyo tangazo zuri, pale halafu mkiwaambia vijana wanasema mtuachie. *(Makofi/Kicheko)*

Nimemwambia Mheshimiwa Mng'ong'o kashindwa kutatua, nikamwambia Waziri wa Habari ndugu yangu Muhamed Seif Khatib, kashindwa kutatua, tumezungumza na wanaohusika akina Nguma walisema *ahaa!* tutazungumza. Nikasema mimi kama Mwenyekiti wa Maadili Bungeni, hili tangazo kwa sababu haliendani na mila zetu kwa hiyo watu wanalichukia na watu wote wanalichukia. Wanaochangamkia ni waswahili wa kawaida tu. Mimi nadhani hiyo *seriousness* lazima tuwe nayo. Lakini fedha kama ni mradi huo, kama kondomu zimekuwa ni mradi, kama *dance* hizo zimekuwa ni mradi *then* UKIMWI wenyewe hauwezi kuondoka. *(Makofi/Kicheko)*

Kama fedha zitaendelea kukaa mijini tu, semina, kongamano tu, then UKIMWI hauwezi kuondoka. Haiwezi kuwa kama Museveni alivyofanya, ni lazima ziende huko. Mimi nilikuwa namwambia, rafiki yangu hivi kama unachonga *(coffin)* kama biashara yako ni masanduku ya kuzikia watu, tija yake ni watu kufa wengi si ndiyo? *(Kicheko)*

Mimi nilimuuliza mtu mmoja pale Manzese ee! Bwana unachonga masanduku hapa akasema umeshapata bwana kuna watu wangapi wamekufa? Nikamwambia mimi nilikuwa nauliza tu bei, hili laki ngapi sijui hili, nikasema sasa biashara namna gani, akasema bwana hii biashara ni ngumu sana mpaka watu wafe bwana. Sasa kwa hiyo, biashara ile ukienda kusali unaomba watu wafe. Kwa sababu tunapoomba huwa shughuli tunazozifanyia kila siku katika nyumba zetu tunataka Mungu azibariki, kwa hiyo ninapokwenda kulala kama huyu anachonga masanduku ya watu nadhani angesema *eeh* Mwenyezi Mungu umeona nimechonga masanduku kama 1000 hapa naomba bwana unibariki sana masanduku yale yaweze kununulika. Kwa maana nyingine watu waweze kufa, si ndiyo maana yake? Sasa kama UKIMWI unageuka kuwa ni mradi tena halafu watu wazima wanaunga mkono kwamba haya ni mambo ya maana hapo kuna kitu kingine tofauti na *sense of seriousness* haipo pale, umakini haupo pale. *(Makofi)*

Nasema hili ni lazima tulipige vita, tunataka tuendane na utamaduni wetu, tufundishe mambo yale yale lakini kwa utamaduni ambao tumeuzoea. Huu utamaduni ambao tunataka kufanya hauwezi kutusaidia. Halafu ni vizuri kushauriwa. Jamani mimi nachukia mtu ambaye hataki kushauriwa. *Anybody* ambaye unataka kumshauri anakuwa mgumu *ngangari* kwamba hivi ndivyo ilivyo mimi huwa namchukia *naturally*, kwa sababu hafai, mwisho utakuja kubaki peke yako. Watu wanasema mwacheni.

Nilikwishawaambia hapa Wanyamwanga wanasema, "*Kantasundwa, kaile na mavi kuukoi"*, haambiliki alikwenda na mavi ukweni matakoni maana amekalia mavi hapa. Sahamani kutumia lugha hiyo amekalia uchafu. Sasa yeye akiguswa na watu kwamba wewe umekalia uchafu kasema acha, sitaki mtu kuniambia kitu chochote mimi ndiyo najifahamu, amekwenda mpaka kwenye ukwe na unajua kwenye ukwe ukienda na vitu kama hivyo ukionekana ndiyo umeathirika kupita kiasi. Amekwenda kugundua ameketi kwenye kiti akinyanyuka hivi mchumba wake akaondoe kile kiti aingize ndani, akasema alikuwa ameketi nani? Wanasema mchumba wako ndiye aliketi hapa. Anasema *loh*! anajisaidia anapokuwa ameketi pale pale tu, *that was the end of the* uchumba sasa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka wenzetu wasijidai kwamba wao ndiyo peke yao wanapigana na mambo ya UKIMWI, sisi sote tunapigana na mambo ya Ukimwi. Tukiwaambia hili halifai watuambie kwamba halifai, tumewaambia kwamba hilo tangazo halafai watu wameng'ang'ana kwamba linafaa. Nawauliza Waheshimiwa Wabunge lile tangazo la watoto kukumbatiana ndiyo linapiga UKIMWI? Hamna kitu pale. Kwa sababu tunawaambia watu hawataki, eti vijana wamekataa, tumewazaa wamekataa? Sisi tunasema sisi hatutaki kuliona hapo, kama redio inang'ang'ana na watu wa sera futa, *full stop,* kwa nini mnakuwa na vitu kama hivyo? *Let us end there with a sense of seriousness* kwenye mikataba hii. Wenzetu wakija kuona matangazo haya wanaanza kutucheka wanasema hiki ni kitu gani, lazima tuweke mambo ya maana. Pamoja na hayo kweli mambo mengine mazuri yamefanyika, tunawapongeza matangazo yamewekwa mengine, wamejaribu kusambaza vibao kila mahali, hapo tunaipongeza kabisa ile *commission* yetu, wamejitahidi kusambaza vitu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mambo madogo tunataka kusahihishana na wao wasiwe *ngangari,* wajue kwamba baadhi ya watu wote ni wazima tumeshaona mambo tunaambizana mambo ya ukweli. Wewe unasema naelewa ni sawa, mimi linanikera sana. Nataka kile kikundi cha *Ishi* kwa utaratibu ule mimi, wala mimi sikipendi, *I declare just like this*, kinasaidia kuleta matatizo mengi, napenda cha akina Betty na vingine vyote vinafanya vizuri. Lakini kile kama ndiyo cha *American* au cha nini *it is no seriousness. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono. *(Makofi)*

**MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia katika hiyo hoja ya Azimio la kupambana na UKIMWI. Awali ya yote naomba niwapongeze sana hawa Mawaziri wa

hizi nchi zetu waliokaa wakajadili na wakafikia makubaliano haya. UKIMWI ni janga ambalo hatuwezi kulifumbia macho na lazima tukeshe tukilifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna yeyote katika Tanzania ambaye anaweza akatamba kwamba UKIMWI haujamgusa aidha katika familia yake au katika marafiki zake. Wote tumeguswa aidha kwa ndugu zetu au kwa watoto wetu au kwa marafiki zetu. Kwa hiyo, ni janga ambalo lazima tupigane nalo kikamilifu. UKIMWI umesababisha tupoteze Nguvu Kazi kubwa sana katika taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, UKIMWI umetufanya tupoteze tija kubwa katika nchi yetu. UKIMWI umefanya kuwe na yatima wengi sana ambao sasa wanalelewa na vikongwe ambao hawawezi kuwajengea maisha ambayo wanayostahili. Kwa hiyo, naomba niseme moja kwa moja kwamba ninaunga mkono hili Azimio kwa asilimia mia kwa mia na naomba Wabunge tuliridhie. *(Makofi)*

Lakini pamoja na hayo naomba niende moja kwa moja katika *Article 7* ya haya makubadiliano *in principle* Mawaziri wamekubaliana juu ya mambo watakayofuata katika kupambana na UKIMWI katika hili eneo la Maziwa Makuu. Wamesema vizuri sana katika *Article 7(3),* naomba niisome kwa Kiingereza halafu nitafsiri. *"To guarantee respect for human rights, gender and cultural sensitivity as well as commitment to the elimination of all forms of stigmatization and discrimination* ya watu wenye UKIMWI *and other vulnerable groups!!* Ni neno refu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama msemaji aliyetangulia alivyosema hawa Mawaziri waliokaa wakafanya makubaliano haya wanaona umuhimu wa kuwa na *cultural sensitivity*, umuhimu wa kupambana na UKIMWI ndani ya utamaduni wetu si nje ya utamaduni wetu. Lakini kitu ambacho kimetokea na ni kosa kubwa ambalo limefanyika ni kwamba tumekuwa tunapambana na UKIMWI nje ya utamaduni wetu. *(Makofi)*

Wiki iliyopita Maaskofu wa Anglican wa Afrika katika mkutano wao Lagos, yuko Askofu mmoja aliyetoka Canada nilimsikia akiomba msamaha kwa utamaduni wa Magharibi kupotosha utamaduni wa Afrika. Mambo ya Usenge na mambo ya ushoga, ameomba msamaha kwa sababu kanisa limejikuta linajadili mambo ya ushoga badala ya kujadili mambo ya dini kwa sababu ya *openness* ya *society* iliyokuwa huko kusema kwamba ni haki ya watu kuwa mashoga na sisi tukarithi hivyo hivyo. Lakini tukumbuke hata wao wenyewe wanaotuletea huo utamaduni hawaukubali, la sivyo Marekani juzi Kerry angechaguliwa lakini kwa sababu alikuwa anaunga mkono ushoga, kwa sababu alikuwa anaunga mkono utoaji wa mimba, Wamarekani wamemkataa. Wale wanaoleta utamaduni wao huku tunauona ni wa maana wao kwao wanaukataa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo hasa kwa sababu ya *concern* ambayo amei-*raise* msemaji aliyepita tuchague maneno ambayo tunatumia huenda ikawa hayalingani na utamaduni wetu. Kwa mfano lile tangazo la usionee soo sema naye, linaweza likawa na nia nzuri sana, waliotunga wakawa na nia nzuri, lakini hawakufikiria watu watalitafsiri namna gani. Sasa usione soo sema naye maana yake sasa inatafsiriwa usionee soo mtongoze, sema naye, useme naye kivipi sasa? Mtongoze. Sasa matangazo

wanayotoa katika kufikiria kwamba wanatusaidia yamekuwa ndiyo chanzo cha kuhamasisha ngono zembe. *(Makofi/Kicheko)*

*Major General* Herman Lupogo, hili naomba unisamehe lakini ni jambo ambalo lazima lizingatiwe sana sasa tunahamasisha ngono waziwazi, kwamba tumia kondomu ukishindwa usione soo mwambie tu, sema naye. Badala ya kumwambia usifanye, badala ya kumwambia ukifanya utapata madhara, sema naye bwana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri ikiwa kampeni yetu dhidi ya UKIMWI itafuata *Article 7, sub-article 3* ya haya, makubaliano hatutaona matangazo ya namna hiyo tena katika *television* zetu. *(Makofi)*

Lakini ni jambo la kushangaza na naomba niseme nasikitika sana hii *attitude* ya biashara kwamba lazima nitangaze kondomu kwa sababu naziuza kwamba lazima niweke hili tangazo kwa sababu nimepewa pesa niweke, ndiyo *attitude* ambayo inafanya tunapotosha Taifa letu kuliko kulijenga. *(Makofi)*

Nafikiri ni lazima tuwe na *censorship* kama wao wameshindwa kufanya *censorship,* kama wao wameshindwa kutuambia maadili ya Mtanzania, ni lazima ifike wakati tufanye *compulsory censorship.*

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu ni kwamba katika kupigana dhidi ya UKIMWI ni lazima tuwe na kiwango cha chini cha namna ya kushauri watu wetu. Lazima tuwe na njia ya kusema hatuwezi kwenda zaidi ya hapa. Mimi siwezi kukaa sebuleni natazama *television* naona wanangu wa kike na wavulana wanashauriwa waseme, wanashikana viuno. Wazazi wengine wamekimbia *television* kwa sababu hiyo. Katika shule za msingi sasa hivi kuna watoto wa darasa la nne, la tano, wanajua mambo kuliko watu wazima sisi. *(Makofi)*

Naomba nitoe mfano pale Kunduchi yuko mtoto mmoja alilala nje, mama yake akaja kulalamika kwa mwalimu wake, yule mtoto akaitwa akaulizwa ni kweli ulilala nje? Akamjibu Mwalimu Mkuu akamwambia ndiyo, ulilala wapi? Nililala kwa bwana wangu, mtoto wa darasa la tano. Huko kwa bwana wako mnafanya nini? Ahaa, si nafanya kile mama anachofanya na baba! Mtoto wa darasa la tano! Lakini hiyo, *openness* ya namna hiyo, ni *openness* ambayo tunajaribu kuleta mila za watu wengine tuna-*superimpose* kwenye mila zetu bila kujua madhara yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima turudi kwenye *moral values* za Mtanzania, ni kitu gani kiko *moral* kwa Mtanzania, ni kitu gani kiko *immoral* kwa Mtanzania. Je, kufanya mapenzi hadharani ni sawa? Kwa sababu mapenzi hadharani kwa mila ya Kiafrika ni tangu kushika kiuno au kupigana mabusu. Hiyo sisi tunasema ni kufanya mapenzi hadharani. Je, sasa tumeshafikia hatua ya kukubali hivyo? Kuonyeshana picha za watu wanaotongozana au mwanaume anakula kidole ndani ya daladala tumeshafikia hatua hiyo, mimi nafikiri hatujafika hatua hiyo na hatuhitaji tufike huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ziko *NGOs* nyingine ambazo kwa kweli hazina nia ya kupiga vita UKIMWI, bali zina nia ya kujikusanyia mapesa. Kazi wanayofanya ni kukaa kwenye mikutano, kukaa kwenye semina ambazo haziishi na hizi *NGOs,* hizi hizi ndiyo zinapata misaada kutoka nje ku-*import* zile mila potofu katika Taifa letu. Naomba Ofisi ya Waziri Mkuu inayosimamia *NGOs* pamoja na ofisi ya *TACAIDS* iweze ku-*monitor* hizi *NGOs* wajue wanafanya nini na wasiruhusu hawa waendelee kupotosha Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nimalizie kwa kurudia tena kuwa tumechelewa kuwa na chombo cha maeneo yetu ya Maziwa Makuu cha kupigana na UKIMWI na tunaomba Tanzania sasa iige Uganda jinsi ilivyopigana na *AIDS* tunaweza tukafanikiwa kama Uganda ilivyofanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namaliza kwa kusema naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja hii. Kwanza nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuleta Mkataba huu ili tuweze kuuridhia. Nafikiri umekuja wakati muafaka. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Lakini kitu ambacho tunakiwa kujiuliza hasa sisi Waafrika ni kimoja tu, kwa nini huu ugonjwa hasa Kusini mwa Jangwa la Sahara umeamua kutumaliza? Kwa sababu zaidi ya asilimia 75 ya wagonjwa wa UKIMWI katika dunia nzima wako Kusini mwa Jangwa la Sahara. Ugonjwa huu si kwamba mwaka jana ilikuwa asilimia 75 haupungui bali unaendelea kuongezeka. Sasa ni kwa nini unaongezeka? Lazima tupate hilo jibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu yenyewe ni moja tu ni elimu ndogo ndiyo inayotufanye tupate matatizo haya ya ugonjwa huu. Sasa tunawezaje kupiga vita huu ugonjwa? Kitu cha kwanza kama Mheshimiwa Eliaachim Simpasa, alivyosema ni kuhamasisha watu wetu. Bila kuhamasisha na kuwapatia elimu tutaisha. Sasa ambavyo tumehamasisha, tumehamasisha watu mijini tu na hata ukienda kule Wilayani semina itafanyika katika Mji Mkuu wa Wilaya ama miji mikubwa mikubwa. Lakini kwenda vitongojini hatufiki.

Sasa tukienda kwa njia hizo kwa kweli hatutafika, ugonjwa huu tunatakiwa twenda kitongoji hadi kitongoji. Kama tunaweza kutafuta kura kutoka kitongoji hadi kitongoji, je, huyu adui kwa nini tusimwendee hivyo? Watu wengine hawana habari huko vijijini, ukimwambia mtu kondomu kwanza anashangaa, ama UKIMWI hajui. Watu wanaoa wanawake hata watano lakini hajui hata maana ya kondomu ni nini.

Kwa hiyo, tunaomba kwamba elimu ndiyo itolewe kwanza na ipelekwe vijijini semina zimezidi mjini. Ukienda Dar es Salaam sasa hivi hoteli zimejaa watu semina za UKIMWI. Mfano tuna chama chetu cha Wabunge, chama hicho mimi nilisema siku moja semina zimetosha twende vijijini, hatujaenda vijijini. Tumepewa semina mpaka

tumechoka. Lakini Wabunge hatujawezeshwa hata kwenda vijijini hakuna hata semina tumefanya hata kijiji cha Chamwino hapo. Tunajifanyia semina wenyewe. *(Makofi)*

Pesa nyingi imemwaga tunafanya sisi wenyewe Chama cha Wabunge. Hivi tumeshindwa kwenda hapa Chamwino tukahamasishe UKIMWI na ndiyo hivyo hela zimetawanywa, wakubwa wanakula, lakini watu vijijini huko hawana habari na UKIMWI wanakufa, kwa hiyo, twende vijijini tukahamasishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu kitu ambacho kimeshangaza kweli kwa akili yetu tunatengeneza Bajeti, inatengenezwa na Wizara ya Fedha kila Wizara inapewa pesa, ukiangalia ya Wizara ya Nishati na Madini Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha wanapata, Wizara ya Maliasili na Utalii inapata lakini hizo hela mmezipangia namna ya kutumia? Mna wataalam wa kwenda kuzitumia huko? Siyo kugawa tu hela umewahi kufanya *indicate* maana yake lazima uweke vigezo hizi hela nimezipeleka pale umewahi kuzifuatilia ukaona kama zime-*achieve* lolote? Huwezi kutawanya hela, hela haziendi kwenye Wizara ya Afya. Hela nyingi utakuta haziendi huko. Kweli unawezaje mtalaam kabisa, mchumi unatoa hela zinasambaa huko? *(Kicheko)*

Ukienda hospitali zile hela hazipo, wale wagonjwa wanakwenda kule hospitali, *three quarter* ya hela haziendi huko. Badala yake tukisaidiwa na watu kama ni *NGO* hela zinatoka nje, wajanja tu wanakwenda pale wanapewa hela. Je, huyu mtu kweli anayepewa hela ana utaalam wa kuweza kuhamasisha watu wasipate UKIMWI. Kwa hiyo, lazima tuwe na *well organized plan.* Mtu anayepewa zile hela awe ni mtu anayeweza kufanya ile kazi, siyo mtu anachukua hela kienyeji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine vitu ambavyo tunatakiwa kufanya kitu kama *condom* ni *very cheap* tutoe bure. Kuna watu na akili zao wanasema hakuna kutumia kondomu sijui nini, bwana jiangalie sana hakikisha unatumia kondomu hayo mambo sijui nani anasema hivyo. Hiyo imani achana nayo utaokoa maisha yako. *(Makofi)*

Kitu kingine ukichukua *regression* ukifanya *epidemic* na zinaa na ukachora ile *regression R2* inaweza kuwa kuja 90 yaani ziko *very close.* Sasa tunapiga vita UKIMWI lakini magonjwa ya zinaa watu hawajui kwamba kama una ugonjwa wa zinaa na ukatembea na mtu mwenye UKIMWI *chance* ya kupata UKIMWI ni *about 100%* kwa hiyo, magonjwa ya zinaa nayo yapigwe vita, watu waambiwe kabisa kama una ugonjwa wa zinaa na ukakumbana nao, umekwenda.

Halafu kuna watu sasa hivi madawa, utasikia madawa ya kupunguza makali yamejaa Dar es Salaam, Serengeti umewahi kuleta hata tembe moja, nikienda kuhutubia wanasema hivi mnafikiri ninyi huko Da re Salaam, ndiyo mnajua kuishi, sisi tunamalizika hapa dawa ziko wapi, unabaki kushangaa, kwani hakuna huwezi kuchukua gari kupeleka madawa huko Serengeti? Watu wanakufa, mnaokoa mjini mnategemea mjini. Tunaomba madawa yaende vijijini kuanzia leo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu madawa si ya kufanyia majaribio, kwamba eti wanafanya majaribio Mikoa hii hiyo siyo hela ya *TASAF.* Hela ya *TASAF* naweza kuisamehe ni hela nyingi zinamwagika unakuta Wilaya inapewa milioni 700 kando yake

pale, haipewi, hiyo *TASAF* naweza kuisamehe lakini mambo ya UKIMWI tunafanyia majaribio unaokoa hawa na hawa wanateketea, siyo mambo ya kufanya mzaha. Majaribio ya madawa haya yaende kila mahali, kila kijiji, kila kitongoji, tusidanganywe hapa eti yanafanyiwe majaribio. Toeni madawa Dar es Salaam yapelekwe vijijini, tumetumia hela nyingi kuyanunua halafu mnaweka Dar es salaam. *(Makofi/Kicheko)*

Pia watoto wanahangaika, unakuta mama, baba, wamekufa, sasa tunahitaji Serikali ianzishe *social security,* ifahamike kabisa kwamba watoto wamefiwa na baba na mama, kwa hiyo, zitafutwe hela kwa makusudi kabisa wale watoto wasaidiwe siyo kwenda pale tunachangia hela.

Kama siku moja mtoto amekuja tukamchangia hela tukalia, *that is not way of doing things.* Wenzetu huko nje hata kama huna kazi unalipwa lakini uwezo hatuna lakini tuna uwezo wa kuweza kuwalipia hawa watoto kuhakikisha kwamba wana-*center,* kuna mahali wanapewa chochote, hela zipelekwe tu Wilayani bwana, kwa sababu watoto yatima wanafahamika wanapewa.

Kuhusu elimu tunashukuru kwamba tumeanza kwamba watasoma bure kuanzia darasa la kwanza mpaka *Ph.D.* Mtoto kama ni yatima alifiwa na baba yake Serikali imlipie tangia akiwa *kindergarten* mpaka *Ph.D.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nawaambia kabisa *this HIV will decide the destiny of a black man. Is more serious!* Tutilie maanani kabisa! Tuwe na programu ambazo zinafahamika. Kwanza mwaka kesho sitaki kuona Bajeti ambayo ina mahela yanatawanywa tu, wale wakubwa wanakwenda kutembelea *per diem.* Unakuta hakuna mtu anafanya kitu kimoja yaani tunacheza na kitu cha hatari namna hiyo!Tunaomba sana jamani tuje na programu nzuri.

Kuhusu mambo ya maonyesho tunayofanya, hivi wewe kweli unawezaje kutengeneza lile tangazo ambalo mtu anakuja kushikana na msichana hivi! Lile tangazo linakuja saa 2.00. Siku hizi saa 2.00 mimi siendi kutazama televisheni na watoto wangu. Unaona mvulana anakuja anasema usiona soo sijui, mambo gani! Angalia matangazo ukienda nchi nyingine, hayafanyiki hivi! Msifanye mzaha, Ukimwi utatumaliza. *Don't play with HIV, it will kill us.*

Siku hizi ukipita pale Kinondoni saa hizi watu wamejaa. *Frequency* za mazishi zimekuwa kubwa! Sasa hivi pamejaa, nenda kesho wamejaa! Watu wamekufa wamekwisha, programu safi sijaiona! Halafu watu wanao-*deal* na mambo ya Ukimwi lazima wawe ni watu ambao damu zinachemka. *We don't include* watu *oldest* kwenye kazi. Wafanye wale ambao kwa kweli akitoa hoja anakuwa anaheshimika. Kwa hiyo, tunaomba Serikali ije na programu safi kwa sababu bado sijaridhika na programu ya Ukimwi. Ukimwi utatumaliza tusipokuwa waangalifu!

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kabla ya yote, kwanza niunge mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sekta ambayo imesahaulika katika nchi yetu ninavyoona mimi. Imesahaulika kabisa katika kupata huduma katika maradhi haya ya Ukimwi, nayo ni Magereza yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Magereza hali ni mbaya sana na wale waliokuwemo mle ni binadamu. Wako mle ndani kwa mujibu wa sheria lakini wana haki zote kama binadamu yeyote aliyeko nje na ndani ya Gereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Magereza yetu yana mchanganyiko wa wafungwa pamoja na mahabusu. Huwezi kujua anayefungwa baada ya hukumu ya Mahakama na yule anayepelekwa kila siku baada ya kufanya uhalifu na kukosa dhamana kwa sababu huwa anapelekwa katika Gereza hilo hilo na anakumbana na wale ambao tayari wamekwishahukumiwa kama wafungwa. Kinachotokea wakati wanapoishi katika Gereza lile huwa wanachanganywa katika sehemu moja, wanalala sehemu moja na hakuna anayefahamu ni yupi ameathirika na yupi ambaye hakuathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, maisha ya Gereza hakuna mtu anaombea afike kule, lakini hali ni mbaya sana hasa tukizingatia kwamba hivi sasa kuna huu ugonjwa wa Ukimwi. Basi, yule anayeingia ambaye hakuathirika anaweza akatoka ameathirika kwa sababu ya yale mazingira anayoishi ndani ya Gereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuzungumzia hii hoja iliyoko mbele yetu na hizi nchi za Maziwa Makuu, katika mipaka yetu inayopakana na nchi jirani za Burundi, Rwanda na Kongo, wale wakimbizi wanaoingia katika nchi zetu tunakuta wakimbizi ambao wamefanya uhalifu katika nchi yetu na wamekamatwa na kesi nyingi za wakimbizi walioko nchini ni *criminal case,* ni *murder case* ambazo kesi zake huchukua muda mrefu. Sasa hawa wanakuwa ni watu kama ameingia ameathirika anakuwa ni mtu ambaye anaeneza Ukimwi katika Gereza lile. Wanafungwa watoto wadogo pamoja na watu wazima, watu ambao wameshazoea kuua katika nchi zetu nyingine kama Burundi na Rwanda, unakuja unawaunganisha na Raia wa Tanzania ambao wamefungwa au wako mahabusu kwa makosa ya kawaida ya kupigana, matusi au kuiba, lakini wanachanganywa na wakimbizi ambao wana kesi za mauaji na wana kesi za kubaka katika Makambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli ningeiomba Serikali kupitia vikao vyake mbalimbali na nchi jirani walizungumzie suala hili la Magereza yetu hasa kuweza ku-*detect* wale ambao wameathirika katika Magereza yetu ili waweze kutenganishwa na wale wafungwa au na mahabusu ambao bado hawajaathirika. Ni rahisi sana kuweza kuwajua na kuwapima wote. Liwe ni suala la kutokuwa na hiyari kama tunavyozungumzia huku nje. Lakini ndani ya Magereza ukitumika utaratibu maalum kwamba ni lazima kila mfungwa na kila anayepelekwa pale kama mahabusu apimwe damu kujulikana kama ameathirika au hakuathirika ili aweze kujulikana na hatimaye

kama ni suala zima la kupeleka matibabu, basi na hawa wafikiriwe kuanza kupewa dawa za kurefusha maisha kwa sababu na wao wana haki kamili kama wengine ambao wako nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika katika makambi ya wakimbizi, pia hizi athari za Ukimwi zimeenea. Kuwe na utaratibu basi wa kupeleka dawa za kutosha kwa vile hili suala linahusisha nchi za Maziwa Makuu, kwamba nchi hizi ziweze kuchangia fedha na kuweza kupeleka dawa za kutosha katika Makambi ya Wakimbizi angalau na wao waweze kupata dawa za kuweza kurefusha maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nimeguswa sana na suala hili la Magereza kwa sababu tumewakuta hawa wafungwa na mahabusu jinsi wanavyolala katika Magereza. Kunakuwa na kama amri moja ya kugeuka kulia na amri ya pili ya kugeuka kushoto.

Kwa hiyo, kama wataingia ndani ya selo saa 12.00 jioni, amri ya kwanza ya kugeuka itakuwa ni saa 6.00 usiku ndio wanageuka upande wa pili mpaka inafika masaa sita mengine ndio wanaamka na kuanza kushughulika na mambo mengine. Sasa unaweza ukafikiria mtu amelala katika Gereza hakuna hata nafasi ya shubiri moja kati ya mtu na mtu na huruhusiwi kulala chali au kulala kifudifudi, unatakiwa ulale ubavu mmoja na nyote kama mmeelekea kulia, mmeelekea kulia na awamu ya pili mnaelekea kushoto. Huo ndio utaratibu ambao unatumika kwa sababu Magereza yetu mengi yamefurika kwa sababu ya matatizo mbalimbali.

Sasa hili suala la kuweza kushughulikia wafungwa na mahabusu ndani ya Magereza kuhusu suala la Ukimwi, naiomba Serikali ichukulie maanani kwa sababu kuna watu wanaathirika. Umekwenda kwa kesi ya kutukana lakini utatoka na janga la Ukimwi. Ni bora basi huyo mtu akatoka nje ili aweze kufanya shughuli mpaka hapo kesi yake itakaposikilizwa. Hii inawezekana kwa sababu zile Kamati ambazo zimepewa majukumu ya kushughulikia kesi mbalimbali ndani ya Magereza hazifanyi kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya zetu wanaohusika wapo, Mwenyekiti anakuwa ni Hakimu, anakuwepo *DAS,* Afisa Magereza, Afisa Polisi, wale wanaweza wakaenda katika Magereza yetu wakatazama zile kesi ambazo zinaweza zikatolewa dhamana watoke nje ili kupunguza msongamano katika Magereza yetu ili hatimaye tusije tukazalisha athari nyingine badala ya kupelekwa kule wafungwa, lakini vile vile tunawatoa ili wawe raia wema nje lakini tunawatoa wanakuwa ni wagonjwa ambao tayari wameathirika na Ukimwi na hii ni hasara kubwa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na hayo ya kuzungumza na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MARGARETH J. BWANA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia na mimi kwa kutoa maoni yangu kuhusiana na hoja hii iliyoletwa mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na wenzangu waliotangulia kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha hoja hii mbele yetu. Nami pia niseme kwamba kwa kweli ninavutiwa sana na utendaji wake mzuri wa kazi na majukumu mbalimbali anayoyafanya katika kutekeleza majukumu yake kama Askari wa Mwavuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika hoja hii kuna maeneo nilikuwa napenda niyazungumze na ninafikiri kwamba hoja hii imeletwa wakati muafaka kwa sababu ni mambo ambayo tumekuwa tukikutana nayo katika maeneo mbalimbali na tumekuwa tukishauriwa na kuelezwa na wananchi wetu katika maeneo yetu tunayoyafanyia kazi huko tunakotoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Ukimwi ni suala ambalo kwa kweli sio geni masikioni mwetu na wananchi wetu wanajua na wanajua athari mbalimbali ambazo zinapatikana kutokana na Ukimwi huu na tumeguswa raia wetu kwa namna moja au nyingine katika kushuhudia kwa kuuguza na hatimaye kwa kuzika ndugu zetu ambao wamepoteza maisha kutokana na janga hili la ugonjwa wa Ukimwi. Tumeshuhudia vijana wetu wengi wenye nguvu wamepoteza maisha, tumeshuhudia ongezeko la watoto yatima katika Vituo vyetu vya Kulelea Watoto, tumeshuhudia akina mama na wazee ambao sasa hivi wanashughulika na kuwalea wajukuu wao kutokana na watoto wao wengi kupoteza maisha kutokana na huu ugonjwa wa Ukimwi. Lakini pia Serikali yetu na Taasisi mbalimbali wamekuwa wakishiriki kwa namna moja au nyingine katika kutoa semina na makongamano mbalimbali kuelezea masuala ya ugonjwa huu wa Ukimwi. Lakini cha kusikitisha ni kwamba idadi ya maongezeko imekuwa ikiongezeka siku hadi siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kabla ya kuja hapa, nilikuwa na ziara Mpanda. Nimefanya ziara katika Wilaya ya Mpanda karibu Majimbo yote ya Mkoa wa Rukwa. Nimesomewa taarifa nikaelezwa, wakanitolea mfano mdogo tu kwamba mwaka jana akina mama 487 ambao walikuwa wanahudhuria mafunzo ya *Clinic,* asilimia 58.2 ya akina mama hao wa Wilaya ya Mpanda walikutwa wameambukizwa ugonjwa wa Ukimwi. Kwa hiyo, ni wazi kwamba hata hao watoto watakaozaliwa kutokana na akina mama hao walioambukizwa, kwa kweli ni watoto ambao baada ya muda tu na wenyewe watakuwa wanazidi kuongeza idadi ya maambukizi, kwa sababu wamezaliwa wakiwa tayari wameambukizwa na idadi ya watoto yatima itazidi kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii inanisikitisha sana kutokana na hayo tunayoyaona huko na inatia simanzi kutokana na elimu ambayo tunadhani kwamba ingeweza kusaidia katika kuepuka maambukizi hayo ya ugonjwa wa Ukimwi inavyotolewa kupitia vyombo vyetu vya habari. Limezungumzwa na baadhi ya wenzangu Waheshimiwa Wabunge na pia lilizungumzwa katika Kikao cha Bajeti iliyopita kuhusu suala la aina ya elimu inavyotolewa kwa wananchi kuhusiana na kinga dhidi ya ugonjwa wa Ukimwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, matangazo mbalimbali ya biashara ambayo yamekuwa yakitolewa kwenye vyombo vyetu vya habari ni matangazo ambayo kwa kweli badala ya

kusaidia kuepuka ugonjwa huu, yanachochea. Kwa mfano, utakuta unaelezwa kwamba, "Kwa raha zaidi tumia Salama Kondomu." Sasa vitu vya namna hiyo kwa kweli hata kama mtu alikuwa hana nia ya kufanya nini, inamhamasisha akanunue ile *Salama Condom* akajaribishe kwamba anadhani anakula raha maalum atakayoipata wakati atakapokuwa anatumia ile *condom.* Lakini kibaya zaidi ni kwamba aina ya matangazo ya biashara yanayotoka hayamtahadharishi mtu hata kidogo badala yake yanamhamasisha mtu kwenda kufanya hili zoezi la ngono.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunadhani kwamba mapendekezo yalitolewa wakati wa Kikao cha Bajeti, Wabunge wengi tu humu ndani walichangia na wakashauri kwamba kwa kweli aina ya matangazo hasa hili la "Usione Soo," halifai, linatakiwa liondolewe. Lakini bado chombo kinachohusika wameling'ang'ania hili tangazo kama vile sijui kwa sababu ipi na kila baada ya muda mfupi unaliona linatokeza kwenye *ITV* mpaka imekuwa ni kero. Inafikia mahali sasa watu wanaamua kuzima na hiyo *TV* yenyewe basi. *(Makofi)*

Sasa kama inafika mahali watu wazima wanazungumza kwamba aina fulani ya matangazo hayafai katika jamii yetu, kwa nini kuna kikundi kimoja tu cha watu wanaling'ang'ania hilo tangazo wanaliona linafaa? Wananchi huko tunakotoka hawalitaki hili tangazo, wanalalamika linawatia aibu. Kwani hakuna aina nyingine ya tangazo ambalo linaweza likazungumzwa zaidi ya hili "Usione soo"? Yale matangazo ya kushikana pale, hivi yanamhamasisha nani? Linatoa fundisho gani? Linamsaidia nani kama hao wanaofaidika nalo hilo tangazo hawalitaki, wanaliona kwamba halifai! Halionyeshi wala halisaidii kumkanya mtu, badala yake linamhamasisha kutokana na aina ya wale wanaotangaza. Kwa nini hili hatulielewi? Mnataka sasa Wabunge tufike mahali tufanyeje sasa? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mama Tere.

**MHE. MARGARETH J. BWANA:** Tushauri mara ngapi? Tufanyeje ili muweze kutuelewa kwamba hilo tangazo halifai na hatulitaki? Mtueleze! *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Waambie!

**MHE. MARGARETH J. BWANA:** Maana sisi ndio Wawakilishi wa wananchi na haya tunayoyazungumza hapa ndiyo hayo tuliyotumwa na wengi. *(Makofi)*

Tunaomba, tunapokuwa tunatoa ushauri wa namna hii wenzetu watuelewe. Tunatoa ushauri ule kwa nia njema kabisa.

**MBUNGE FULANI:** Na mavazi.

**MHE. MARGARETH J. BWANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo mimi nashauri lile tangazo linaloimbwa na wale vijana wanne kutoka Makete, lile tangazo linafaa sana. Lina mafunzo! Lile tangazo linapotokea kwenye *TV* kila mtu anakaa anakuwa *attentively* na kusikiliza, anaanza kutafakari mwenendo wake katika ujumla wake. Lina mafunzo makubwa sana tangazo lile. Lile tangazo kama lingekuwa

linatoka kila wakati, lingeweza kubadilisha hata mwenendo wa watu. Lakini sio lile la usione soo. Halifai! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nilikuwa napenda nilizungumze hilo. Aina ya matangazo ya biashara hayasaidii kupunguza kasi ya kuenea kwa Ukimwi na matokeo yake yanahamasisha. Ndiyo maana pamoja na semina na makongamano na warsha ambazo zimekuwa zikifanyika kila wakati, lakini ongezeko la ugonjwa wa Ukimwi linazidi kuongezeka. Kwa nini hatujiulizi? Maana kama ni suala la elimu tayari ipo na kama ni suala la kuzungumza, tayari limezungumzwa sana. Kama ni suala la makongamano na warsha na semina mbalimbali zimeshafanyika sana; kwa nini ongezeko la ugonjwa wa Ukimwi linazidi kuongezeka kila siku?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba hilo lizingatiwe, lifanyiwe utaratibu. Wale vijana wanne wapewe nafasi kubwa zaidi kutoa matangazo na hilo tangazo la "Usione soo," lifutwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa William Lukuvi, sisi tunamuunga mkono sana anafanya kazi nzuri sana. Wabunge wote hapa tunamuamini mno na tunaamini kabisa kwamba hilo halijamshinda kufanyia kazi. Kwa hiyo na yeye asione soo kulitolea maamuzi. Hilo la kwanza, tunamwomba na Mheshimiwa William Lukuvi, naye asione soo katika kulifanyia maamuzi ya haraka tangazo hili. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni hizi fedha zinazotumika kwa ajili ya makongamano, semina na warsha. Mimi naomba fedha hizi sasa kama ni semina zimetosha. Fedha hizi zielekezwe katika kusaidia kwenye vile Vituo vya Watoto Yatima.

**MBUNGE FULANI:** Naam!

**MHE. MARGARETH J. BWANA:** Wale watoto wanahitaji sana msaada, wana hali ngumu sana kule. Sisi ndio tunakaa nao tunawatembelea na kuona matatizo yao. Wana hali ngumu. Serikali imeshatenga fedha nyingi sana katika eneo hili, tunaomba fedha hizo sasa zipelekwe kwenye kile Kituo cha Katantalamba kule Sumbawanga Mjini, kituo kingine kiko Busega, mwenzangu ananieleza hapa na maeneo mengine kule Iringa, Makete wanahitaji sana msaada, hali ni ngumu. Wale watu wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Tulikuwa tunaomba hata hizi dawa ambazo zimeletwa kwa ajili ya kuongeza nguvu jamani, zielekezwe zaidi kwenye vile Vituo vya wale watoto. Kuna watoto wadogo wana miaka mitano tayari wamezaliwa wakiwa wameambukizwa. Zile fedha zipelekwe kule ziweze kuwasaidia kuokoa maisha ya wale watoto. Naomba sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa kweli kero yangu ilikuwa ni hayo. Nimeyazungumza na nina uhakika hata leo nitapumua, nitalala na usingizi. Ninaunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, hapo ndio nimeishia kwa wachangiaji. Sasa namwita mtoa hoja. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nishukuru sana kwa michango mbalimbali iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Nianze kwa kuwatambua wachangiaji waliosema, hasa wa kwanza aliyeanza kusema kwa niaba ya Kamati, Mheshimiwa Zahor Khamis, wa pili, aliyesema kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Grace Kiwelu, wa tatu, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, wa nne, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, wa tano Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, wa sita Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah na wa mwisho kwa kusema ni Mheshimiwa Margareth Bwana. *(Makofi)*

Lakini wako pia waliochangia kwa maandishi, nao ni watano. Mmoja ni Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, wa pili, Dr. Chegeni Raphael Masunga, wa tatu, Mheshimiwa George Lubeleje, wa nne, Mheshimiwa Semindu Pawa na wa tano, Mheshimiwa Leonard Shango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, kwanza kwa kuunga mkono Azimio ambalo tumelileta hapa. Nataka kuwahakikishia kwamba sisi kwa sababu ni miongoni katika Baraza lile la Mawaziri, mimi ni mwakilishi wenu, lakini pia Mwenyekiti wa *TACAIDS* kwa *Commission* ile ni mwakilishi wetu. Kwa hiyo, tutajitahidi kusimamia kuhakikisha kwamba malengo yaliyowekwa yanazingatiwa na yanatekelezwa.

Pili, nataka nikubaliane na michango karibu yote ya Waheshimiwa Wabunge. Nataka niseme kwamba wengi na wote mmetoa ushauri, kwa sababu katika Taasisi ambazo zimeonekana zina msimamo na zimeanzisha ukereketwa wa mwanzo kabisa wa mapambano dhidi ya Ukimwi, sisi Bunge tulikuwa wa kwanza kwa kuanzisha umoja wetu. Mnakumbuka tulipozindua ile *TAPAC* alikuja Rais Mstaafu wa Ghana hapa, Mheshimiwa Jerry Rawlings na Mheshimiwa Rais alizindua hapo na Taasisi zote za Kimataifa, wanatuheshimu sana Wabunge kwa sababu ya msimamo wetu dhidi ya vita hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa naunga mkono wazo la Mheshimiwa Dr. James Wanyancha kwamba hatujapiga hatua na *TAPAC* yetu, tumekuwa tunaboreshana, tunafanyiana semina wenyewe kwa wenyewe na mimi naunga mkono maelezo ya Mheshimiwa Dr. James Wanyancha kwamba sasa twende nje ya sisi. Tutafute fedha ili twende tukawawezeshe wenzetu zaidi badala ya kuwezeshana wenyewe kwa wenyewe, maana na mimi ni mwanachama vile vile.

Lakini pia naunga mkono maelezo yote yaliyoanza kuchochewa na Mheshimiwa Eliachim Simpasa na kuungwa mkono na kila mtu. Ni kweli yapo baadhi ya matangazo ambayo yanachochea ngono. Sasa kwa sababu tunasema chanzo kikuu cha Ukimwi ni ngono, basi ni kweli matangazo haya hayafai. Kwa hiyo, na mimi naunga mkono matangazo hayo pamoja na kwamba vyombo hivi vinavyotangaza ni vyombo binafsi, lakini naamini *TACAIDS* kwa sheria tuliyowapa wanao uwezo wa kuratibu mambo haya

ili kusimamia yale yote ambayo hayastahili kutolewa katika eneo hili la nchi yetu. Wanao uwezo wa kusimamia.

Kwa hiyo, nafikiri tumeelewa na bahati nzuri na *Chairman* wa *TACAIDS* yuko hapa. Nafikiri hizi ndio *agenda* za kuzungumzia kwenye *Commission* yao. Kama kuna jambo la uratibu, basi na hili waratibu pamoja na matangazo. Maana tunaweza tukawa tunahamasisha vijana wasishiriki katika vitendo vya hovyo lakini wakiangalia kwenye vyombo vya habari wanaona vitendo vile vinahamasishwa kwa nguvu.

Kwa hiyo, nashukuru kwa maoni yenu. Nataka kusema kwamba tutaangalia na tutazichukulia hatua nyimbo zote na matangazo yanayochochea ngono. Ziko nyimbo na matangazo yanayochochea ngono. Sasa hivi kumefumka nyimbo mbalimbali, wala sio matangazo tu, lakini mkiangalia hata zile nyimbo, maudhui yake mengine hayana maana. Lakini pia tutaangalia matangazo na nyimbo ambazo zinaongeza unyanyapaa.

Kwa mfano, katika hayo matangazo wengine Waheshimiwa Wabunge mmeyasifu, hata mimi nimewasikiliza wale vijana wanaoimba, lakini kuna maneno ukifuatilia hayafai. Wanawaita wenye virusi marehemu watarajiwa. Hili haliwezi kuvumiliwa kwa sababu hata wenyewe wenye virusi wameshatuandikia kulalamika, hawapendi kuitwa marehemu watarajiwa. Huwezi kusema unaondoa unyanyapaa halafu mtu mwenye virusi vya Ukimwi unamwita marehemu mtarajiwa. Halafu tunahimiza wananchi waende kupima kwa hiari, atakwendaje mtu kupima kwa hiari ili ajulikane yeye ni marehemu mtarajiwa? Hawezi kukubali!

Kwa hiyo, wakati tunashughulikia tatizo la kuondoa matangazo yanayohamasisha ngono, lakini tutashiriki vile vile na kushirikiana kuhakikisha kwamba matangazo na nyimbo zote zinazowanyanyapaa, zinazowabagua nazo tutazishuhulikia vile vile kwa sababu moja ya tatizo kubwa ni stigma. Unyanyapaa ni tatizo sana. Hivi sasa hata dawa tunazotoa kama watu hawaendi kupima kwa hiari atakunywa nani? Maana mtu anaogopa akishapima halafu anaanza kunyooshewa vidole. Usimwone hivi marehemu mtarajiwa ana gonjwa lile la hatari kabisa. Sasa gonjwa la hatari mnalileteaje dawa? Kwa hiyo, ana miwaya, ana hivi na lugha kama hizi zinapunguza kasi ya elimu yetu kuwafikia wananchi.

Kwa hiyo, yako mawili ambayo tutayaangalia sambamba na ushauri wenu. Lile la matangazo na nyimbo zote ambazo zinahamasisha vitendo vya ngono waziwazi.

Hivi majuzi mnajua Waziri wa Habari alipiga marufuku magazeti fulani kwa sababu ya vitendo hivi hivi. Unaona picha zile na mambo yao yaliyokuwa yanaandikwa hayafai, yamefungiwa. Lakini pia tutakwenda zaidi kuangalia yale matangazo na nyimbo ambazo kwa kweli lazima tusimamie. Tusikilize nyimbo zile tuone kama kweli zinakwenda sambamba na vita yetu. Hatutaki kubana sana maana tuko kwenye soko huru lakini tutajitahidi angalau malengo ya mila na desturi yanayoambatana na vita hii ili tushinde. Tutayasimamia.

Kwa hiyo, kwa ufupi Waheshimiwa Wabunge nataka kukiri kwamba na mimi najua baadhi ya matangazo kwamba kweli yanahamasisha ngono na tutajitahidi

kushirikiana. Sio jambo la kesho, kwa hiyo msiangalie *TV* kesho kwamba tutasimamisha. Yale matangazo yameshalipiwa na watu na mengine yameshalipiwa na Mashirika ya Kimataifa. Kuna watu wameshapewa pesa. Nasema tutachukua hatua lakini kwa utaratibu unaokubalika. Maana kauli yangu mimi naweza nikasema hapa nitajidanganya au nikawadanganya Waheshimiwa Wabunge kwamba napiga marufuku yakionekana kesho! *(Kicheko)*

Mimi nakiri tu kwamba tutayashughulikia na tutayachunguza... *(Kelele/Fujo)*

**NAIBU SPIKA:** Tumsikilize Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Itakuwa ni kazi yetu sasa ya kudumu kuhakikisha kwamba matangazo tunayotaka kweli yawafikie wananchi yawe yale ambayo tumeyakubali na nyimbo vile vile ziwe zinakwenda sambamba na maadili.

Lakini pia naendelea kuunga mkono maelezo mbalimbali ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge kwamba fedha hizi sasa zinazokuja katika mapambano dhidi ya Ukimwi zisitumike sana kwa warsha na semina. Nyingine mmesema zinatumika vibaya, sasa nataka niwakumbushe kwamba kwa mwongozo ambao umeshatolewa na TAMISEMI mpaka kwenye Halmashauri, kwa fedha hizi za Serikali ambazo nyinyi mnabajeti humu ndani, kwa kweli *TACAIDS* hawatoi hizi pesa mpaka mipango itoke Wilayani.

Mimi naomba kabisa Waheshimiwa Wabunge, ukali tulioutumia humu leo, hebu tukautumie kwenye Halmashauri kwa sababu mipango yenu yote inayotoka kwenye Halmashauri ni warsha na semina tupu.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi mimi nilikuwa Mkoa wa Kilimanjaro nikamwita Mkurugenzi wa Hai, amepewa fedha katika Wilaya chache ambazo zilipewa fedha za *Global Fund.* Hai tumewapelekea shilingi milioni 122. Nimemwuliza hivi kwa nini hujatumia? Anasema ndiyo nimeanza, nimewapa kila Kata milioni moja, moja, nimeshapeleka milioni 122.

Juzi tumesimamisha fedha za Makete. Tumewapelekea *over a hundred million.* Lakini mipango yao ni ya posho, posho tu na ukisimamia sasa wafanye haya ambayo tunayajua ya watoto yatima pale wawasomeshe, hawana nguo ndogo, ndogo, hawana chakula na kadhalika.

Wale watu ni wakali sana, kuna utaratibu na utaalam, watu wameshazoea. Unajua kama mnavyosema, hii miradi sasa *NGO* nyingi zimesajiliwa na huu ni mradi wa kudumu na kila watu wanapata fedha sehemu mbalimbali mambo wanayoyajua ndiyo yale wameyazoea na kila siku wanataka kuandika hayo. Kwa hiyo, lazima tujitahidi na sisi tusimamie tubadilishe kule kwenye Halmashauri. Hata kama hatushiriki kwenye zile Kamati za Ukimwi ambazo tumeshaziunda kwa mujibu wa Sera tumeshaziunda na kila Kamati kila Wilaya lazima iwe na Kamati. Lakini angalau kwenye *Full Council* zile

mnazokutana hebu waambieni. Wilaya zote karibu tunaendelea kuzipelekea fedha na tutaendelea kuzipelekea fedha kila mwaka maana tumeshaamua.

Lakini watoe taarifa wamefanya nazo nini, muone katika yale matumizi je, kuna fedha ambazo zinaweza zikakamatika, miradi ambayo inaweza kukamatika, inaweza ikaelezeka? Mtakuta ni vikao tu. Sasa tuanze kusimamia Halmashauri, tupunguze vikao, semina na warsha na mnajua fedha za warsha huwezi kutathmini kwa kweli. Inaweza kuwa warsha ya watu watano, ukapata sahihi 20. Tusipoendelea kudhibiti hizi warsha kunakuwa na udanganyifu mkubwa sana wa pesa. Maana mahudhurio hamkuwepo, hivyo wakiandika kule, rafiki yangu Magu kule wamehudhuria wananchi 500 katika warsha lakini walifika 20, utajuaje? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kweli kwenye warsha kuna udanganyifu mkubwa. Mimi nakubaliana na ninyi kwamba lazima tudhibiti fedha hizi na tudhibiti mambo yanayoambatana au yanayotakiwa kutumika na fedha hizi kwenye kampeni za ukimwi. Zipo fedha za Serikali, zipo fedha za wahisani. Lakini kwa mujibu wa sheria yetu sisi Halmashauri ina mwongozo, Halmashauri sasa ndiyo mratibu wa shughuli zote za mapambano katika Wilaya. Kwa hiyo, katika *cluster* ile ya Wilaya, Halmashauri ina uwezo wa kuita na kupata taarifa kutoka *NGOs* na Taasisi zote zinazosimamia mapambano dhidi ya ukimwi, hata kama fedha wanatafuta wenyewe. Lakini mwongozo lazima utoke kwa Halmashauri kujua pamoja na kwamba wanatafuta fedha mwenyewe, lakini tungependekeza vita tuelekeze katika *line* fulani katika Halmashauri. Kwa hiyo, lazima tusimamie vizuri.

Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliozungumzia eneo hili na sisi ambao tunagawa hizi fedha huku juu ikifika wakati wa Bajeti tujitahidi kutoa ushauri kama hivi, lakini sisi tunaoangalia huku juu tutajitahidi kupunguza kidogo, hasa miradi inayotoka kwenye Halmashauri za Wilaya ili kupunguza eneo ambao si rahisi sana kulidhibiti. Elimu lazima tuendelee kuitoa. Lakini kwa namna gani lazima tushirikiane. Kwa vyovyote vile ukiacha elimu kwenye ukimwi, hupambani na vita ya ukimwi lakini ya namna gani? Tunatoa elimu ya namna gani? Kwa akina nani? Ili kama ukienda kuwaona wamebadilika, tuwe na uwezo wa kuwapima, kujua kwamba hao tuliowapa elimu wamebadilika.

Kwa hiyo, tushirikiane, tubane kule kwenye Halmashauri na sisi tutabanana huku kwenye Kamisheni ya *TACAIDS* ili wawe wasimamizi wazuri sana wa fedha zao si suala la kutoa tu lakini lazima wafuatilie na kusimamia, na sisi kwenye kila Wilaya kama mlivyosema kila Wizara ina Bajeti yake. Kwa hiyo, kila Wizara lazima, isitoe tu pesa lakini lazima ihakikishe matumizi ya pesa zake na tutajitahidi kadri tunavyokwenda kuhakikisha kwamba tunapata uzoefu na shughuli mbalimbali za mapambano ya ukimwi tunaamua tunaelekeza fedha katika maeneo ambayo yatakuwa na *impact* zaidi.

Lakini pia Mheshimiwa Dr. James Wanyancha amezungumzia habari ya uhamasishaji mdogo na pia hili la fedha za ukimwi zitumike vizuri. Lakini hasa nataka kuzungumzia juu ya madawa. Tumeanza kununua dawa kwa fedha zetu, hatujapata msaada, tunazo fedha tumetenga hapa kwenye Bajeti, bilioni 2. Tumeshanunua tayari na tulinunua hapa, nilitaka kusema kidogo kwamba Mheshimiwa Dr. James Wanyancha

amesema dawa ziko Dar es Salaam. Hapana, hazibaki Dar es salaam. Tumeainisha vituo karibu 33 vya kuanzia au utakuta kuna vituo viwili au kimoja kwa sababu tumeanza kwa fedha zetu kidogo.

Lakini wahisani kwa mfano, kuna mfuko wa Clinton, tuko njiani tunazungumza nao watatoa hizi fedha na *Global Fund* na kila mwaka Serikali tumeamua kupanga hizi fedha kwenye Bajeti ili angalau twende kwenye hospitali zote. Hizi dawa haziko Dar es Salaam. Tumeshawafundisha watu wa Afya, maana haya mambo ni mapya watoaji wa dawa hizi wameshafundishwa kwenye vituo vyetu hasa vile ambavyo vimeshapewa hizi dawa na tumeshaainisha watu wa kutumia hizi dawa kwa sababu uwezo wetu ni mdogo na tunataka wale tunaoanza kuwapa tusisite kuwapa dawa hata mara moja kwa sababu dawa hizi ukishaanza kumpa leo lazima umhakikishie unampa maisha yake yote. Ukisita umemwua. Kwa hiyo, si vizuri kutawanya dawa za bilioni 2 kila mtu anaonja mwezi mzima halafu anaacha kutumia utamwua. Kwa hiyo, tumeanza kidogo lakini ni nia ya Serikali kwa kushirikiana na wadau wetu wa maendeleo kuhakikisha kwamba hizi kwa kadri ya uwezo zitafika katika hospitali zote na tumelenga kabisa kwamba ikiwezekana basi walengwa wote kwa baadaye wale walioathirika na wale tu ambao wanastahili kutumia hizi dawa maana si kila mtu mwenye virusi vya ukimwi anastahili kutumia hizi dawa. Tunao watu kwa mfano, hata hapa tumekuwa tunasikia kwenye magazeti na kwenye *TV* wanaishi na virusi zaidi ya miaka 15 lakini hawajatakiwa kutumia dawa. Miili yao peke yao na chakula na maadili yao wanaishi na virusi ni ugonjwa ambao ni virusi wanaishi navyo, virusi wanavyoishi navyo kama wagonjwa wa kisukari na wagonjwa wa presha. Kwa sababu kunywa dawa lazima uwe umeshauriwa na Daktari kwamba kinga yako imeshuka kiasi fulani, ndiyo unaruhusiwa kutumia dawa. Siyo kwamba kila mwenye virusi lazima atumie dawa.

Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallaah, amezungumzia habari ya Magereza. Najua Magereza wanajitahidi sana na Bajeti yao ilivyo finyu, wanajitahidi sana na wanao mkakati maalum wa mapambano dhidi ya Ukimwi. Lakini ushauri wako tumeusikia na najua na wewe pamoja na kutembelea Magereza unajua si nia ya Serikali kuwalaza chali wale wafungwa au kuwabananisha vile au kuwalaza kiubavu ubavu kama ulivyowaona, lakini uwezo mdogo. Uwezo mdogo, hatuna uwezo wa kujenga magereza, maana hatujui hata hivyo, idadi ya wafungwa na idadi ya magereza itakayotosheleza mahitaji ya wafungwa. Maana hatujui hata hivyo. Hatuwezi kubajeti wafungwa watatokea kesho. Lakini tatizo la wakimbizi nalo katika maeneo fulani limetujazia magereza yetu. Lakini hata hivyo, tutajitahidi kuimarisha mikakaati katika maeneo hayo ya magereza. Hivi sasa tathmini mpya imeshafanywa na Serikali kwa kushirikiana na wadau. Kulikuwa na timu ya wataalam ambao imepewa kazi ya kufanya tathmini ya hali halisi ya gonjwa hili katika nchi hii. Naamini katika wiki hii tutajitahidi kutoa hiyo tathmini ili tujue Kitaifa hali ya mapambano na hali ya gonjwa hili kitaifa ikoje kulingana na tathmini ambayo tayari imeshafanywa na taarifa zote tunazo.

Kwa maelezo hayo, naomba kurudia tena kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao na hasa kwa *mood* ya uwakilishaji wa michango yenyewe, inaonyesha kabisa jinsi tunavyojali lakini pia nataka nikiri kwamba yale yaliyo ndani ya uwezo wetu

tutayasimamia na tutaendelea kushirikiana lakini niombe yale ambayo yapo ndani ya uwezo wetu sisi kama Wabunge kwenye maeneo yetu tusimamie. *(Makofi)*

Kwenye Halmashauri zetu kwa sababu tumepewa uwezo wa kuratibu shughuli zote katika maeneo yetu basi tusimamie vitendo ambavyo hata ambavyo hatuvioni kwenye televisheni na magazeti. Vile vitendo vinavyosababisha ongezeko la gonjwa hili katika maeneo yetu tujitahidi kutumia mbinu zetu na Kamati zetu mbalimbali za ukimwi kuyadhibiti yale ambayo yako kwenye ngazi yetu sisi tutajitahidi kutumia mamlaka tulizopewa kwa sheria, kuyadhibiti ili angalau gonjwa hili kama alivyosema Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, tulipige lakini kwa kuzingatia maadili ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Kuridhia Mkataba wa Ushirikiano wa Nchi za Maziwa Makuu katika Kupiga Vita Ugonjwa wa UKIMWI liliridhiwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Azimio hili limepitishwa rasmi na Bunge. Hapo ndipo tumefikia mwisho wa shughuli za leo. Lakini kabla sijaahirisha shughuli za Bunge kuna tangazo dogo. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini anatukumbusha kwamba ile Semina ipo kesho na itafunguliwa saa tatu kamili. Itafunguliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na kutokana na shughuli nyingi alizonazo Mheshimiwa Waziri Mkuu angependa saa tatu kamili ifunguliwe ili yeye kama kuendelea na shughuli zingine aweze kupata nafasi ya kuendelea na shughuli hizo. Kwa hiyo, Semina kesho saa tatu kamili.

Waheshimiwa Wabunge, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka Jumatatu saa tatu asubuhi.

*(Saa 11.40 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu*
*Tarehe 8 Novemba, 2004 saa tatu asubuhi)*